

17 JUNI 2013

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Hamsini - Tarehe 17 Juni, 2013**

*(Mkutano Ulianiza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. SAADA MKUYA SALUM  
(K.n.y. WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA):**

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Wakala wa Wakulima wadogo wadogo wa Chai Tanzania kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2012 (*The Annual Report and Accounts of Tanzania Smallholders Tea Development Agency for Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012*).

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Bodi ya Chai Tanzania kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2012 (*The Annual Report and Accounts of Tea Board of Tanzania for the Financial Year ended 30<sup>th</sup> June, 2012*).

**MHE. ANDREW J. CHENGE - MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa Mwaka 2013/2014 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2012/2013 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

17 JUNI 2013

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza maswali na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Na. 401

### **Miundombinu na Huduma za Jamii kwa Wananchi Waliopolekwa Pugu Kinyamwezi**

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA** Aliuliza:-

Mwaka 2010/2011 Wananchi wa Kata za Kipawa na Kigilagila walihamishiwa Kata ya Pugu Kinyamwezi ili kuitisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwl. Julius K. Nyerere, lakini kule walipopelekwa hakuna miundombinu na huduma za kijamii za kutosha:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka miundombinu ya barabara, umeme, maji na huduma za afya kwa Wananchi hao?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua tatizo la migogoro iliyojitokeza kwa kutoa kiwanja kimoja kwa watu wawili huko walikohamishiwa?

**SPIKA:** Kanuni inasema Mheshimiwa Spika, naomba swali namba fulani lijibiwe, hayo maneno yote hayahitajiki.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, Mbunge wa Ukonga, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma za jamii katika eneo la Pugu Kinyamwezi walikohamishiwa Wananchi wapatao 2094, Serikali imefanya jitihada mbalimbali ambapo katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012 na 2012/2013, imetumia

shilingi bilioni 1.2 ili kuboresha miundombinu ya huduma za kiuchumi na kijamii katika Kata za Majohé, Chanika na Pugu. Miundombinu hiyo ni pamoja na kupandisha hadhi Zahanati za Pugu na Chanika kuwa Vituo vya Afya, kujenga Ofisi ya Serikali za Mitaa - Kata ya Majohé, kujenga Kituo cha Polisi - Daraja B Kimwani (Chanika), ujenzi wa kilomita 2.5 za barabara Mtaa wa Bungulo na uchimbaji wa visima vitano vya maji katika maeneo ya Mgeule, Mji Mpya, Majohé na Kimani Pugu.

Mheshimiwa Spika, kwa upandewa elimu, Serikali imejenga shule mbili za sekondari katika eneo la Pugu Kinyamwezi, Majohé na Nyeburu. Pia imekarabati vyumba tisa vya madarasa na kutengeneza madawati 729. Aidha, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali imeidhinisha shilingi bilioni 1.72 kwa ajili ya kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu, afya na maji katika Kata za Pugu, Majohé na Chanika.

(b) Mheshimiwa Spika, katika eneo la Kigilagila na Kipawa walikohamishiwa Wananchi kutoka Kinyamwezi, ipo migogoro ya ardhi 17 ambayo imeripotiwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilala. Hadi sasa, Halmashauri hii imetatua migogoro 11 na hatua za ushughulikiaji wa migogoro iliyobaki zinaendelea.

Migogoro hiyo kwa kiasi kikubwa inatokana na uvamizi wa maeneo ya viwanja viliviyovamiwa na visivyopimwa na matumizi ya nyaraka za kugushi na migogoro ya mipaka.

Natoa wito kwa Halmashauri na Wananchi kwa ujumla, kuzingatia Sheria zinazosimamia masuala ya ardhi ili kuepuka migogoro isiyokuwa ya lazima.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambayo imefanyika katika Kata hizo ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri, mimi nataka niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i)Kwa kuwa swali langu la msingi lilijikita zaidi katika eneo la Pugu Kinyamwezi; na kwa kuwa mpaka hivi sasa ninavyozungumza katika eneo hilo wana changamoto kubwa

sana ya barabara pamoja na maji. Naomba Mheshimiwa Waziri anijibu *specific* katika eneo nililotaja katika swali langu la msingi Pungu Kinyamwezi; je, Serikali ina mpango gani angalau kuchonga zile barabara pamoja na kuwapelekea umeme watu hao wa Pugu Kinyamwezi?

(ii) Kwakuwaniukweliusiopingikakuwasualala migogoro ya ardhi katika eneo ambalo nimelitaja la Pugu Kinyamwezi, kwa sehemu kubwa Serikali inahusika; kwa sababu baada ya kwenda kutathmini walikaa muda mrefu takribani miaka 12 bila kurudi kwenda kuwagawia tena Wananchi maeneo hayo; na kwa kuwa Wananchi sasa walianza kuyauza maeneo yale; na kwa kuwa Wananchi waliobaki kwenye migogoro hawazidi saba: Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu angalau hao Wananchi kwa kuwa na wao ni Watanzania wapatiwe maeneo mengine kwa sababu walikwisha kuendeleza maeneo hayo?

**SPIKA:** Eee, swali refu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eugen E. Mwaiposa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, takwimu nilizozitoa hapa ni za jumla kama anavyosema Mheshimwa Mbunge, nakubaliana naye na kwa mwaka wa 2011/2012 tulikuwa tumetenga shilingi bilioni 1.2. Kwa mwaka huu wa fedha, fedha hizi ambazo tumepitisha hapa ni shilingi bilioni 1.7. Kuhusu barabara anayozungumza hapa, sijajua vizuri kipande hiki anachokisema. Takwimu nilizonazo hapa zinaonesha kwamba, tumetenga fedha kwa ajili ya barabara, *tuta-compare* na Mheshimiwa Mbunge, kilomita 2.5 ambazo zimetengwa shilingi milioni 33.5, *whether* hicho anachoniuliza ndicho hiki nitachokisema. Nitaomba tukimaliza hapa, tuweze kufananisha haya mawili.

La pili, hili analogzungumzia kuhusu suala la *compensation* kwa maana ya fidia, ni kweli nakubaliana na Mheshimiwa Mwaiposa kwamba, kumekuwa kuna mkorogo na mkanganyiko na vitu vingine, yuko mtu ameachia eneo lake likachukuliwa,

akapewa fidia zake na kila kitu, lakini mle ndani alishamwuzia mtu eneo lile na yule mtu ndani ya moyo wake ana kitu kinachoitwa *declaration of ownership*, yaani anajisikia kwamba ni kwake. Halmashauri imekuja imepima pale, kunatokea kitu hiki anachokiita *double allocation*, yaani kwa maana kwamba eneo moja linaonekana ni la watu wawili. Tumefanya zoezi pale, matatizo haya yote yanayozungumzwa hapa, yalikuwa ni watu kama 17, ndiyo wenye matatizo kama hayo, 11 tumeyaondoa na haya mengine yaliyobakia bado tunaendelea nayo kwa msingi huo anaouzungumzia pale.

Sasa kwa suala la *compensation*, kwa sababu hapa najua ni lazima niwe mwangalifu mpaka niende nikaangalie taarifa vizuri, nisije nikasema ndiyo tumetoa fidia, watu wakapiga makofi huko waliko halafu wasema mimi nimejibu hivyo. Nitakwenda kuangalia.

Nataka aniambie hawa anaosema hawakufidiwa, kwa sababu watu hawa walipisha Uwanja wa Ndege, wakaondoka wakaenda kule kwenye lile eneo, sasa kama kuna waliobaki, ninataka kujua msingi wake ni nini; kwa nini walibaki na nini kilichosababisha hivyo! Kwa hiyo, naomba niishie hapo, nita-check na Mheshimiwa Mwaiposa ili niweze kumpa jibu sahihi zaidi.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea, sikuona watu wengine. Naomba nimwite Mheshimiwa Desderius Mipata, aulize swalilinalofuata.

Na. 402

### Kujenga Daraja la Mto Kisa

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Wananchiwa Vijijivya Myula, Chalatila, Chongana Nchenje wamekuwa wakiomba kujengewa Daraja la Mto Kisa uliopo kati ya Vijiji vya Nchenje na Chonga na wamekuwa wakijitolea kulima barabara na kutengeneza daraja la kienyeji:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu ombi hilo la Wananchi?

17 JUNI 2013

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius J. Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Mto Kisa umeingizwa kwenye Mpango na Bajeti ya mwaka 2013/2014 na kutengewa kiasi cha shilingi milioni 38.3, baada ya kujadiliwa kwenye Vikao vya Halmashauri na kukubalika kwamba ni moja ya vipaumbele vya Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Ilibidi maombi haya yaingizwe kwenye Mpango wa Bajeti ya mwaka 2013/2014, baada ya kuwa ombi hili lilitolewa baada ya mchakato wa bajeti ya 2012/2013 kupita.

Mheshimiwa Spika, Wataalamwa Halmashauri wamefanya upembuzi yakinifu na usanifu wa mradi na kupata kiasi hicho cha fedha ambacho kimetajwa hapo juu.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwakuwa Halmashauriza Wilaya ndizozinazohudumia barabara za vijiji; na kwa kuwa vijiji vingi havijaunganishwa kwa barabara na hutegemeana kwa huduma za kiuchumi na kijamii; na kwa kuwa lipo katazo la Serikali kwa Halmashauri kutotumia fedha za Mfuko wa Barabara kuanzisha barabara mpya; je, Serikali bado ina msimamo huo huo?

(ii) Mheshimiwa Waziri umekuwa ukiitembelea Wilaya yetu na ziara zako zimekuwa na mafanikio makubwa. Mara ya mwisho ulipotembelea tulikuomba uitembelee Kata ya Wapembe ili kujionea Barabara ya Kitosi - Wampembe na Nkana - Kala, ambazo zina changamoto kubwa sana na zinahudumiwa na Halmashauri. Je, uko tayari kupanga ziara katika Tarafa ya Wampembe? (*Makof*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Desderius J. Mipata, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Barabara, *Amendment Act No. 2* ya mwaka 1998 na mabadiliko yake ya mwaka 2006, hakuna kifungu chochote kinachozua fedha za Mfuko wa Barabara zisitumike kwenye barabara mpya.

Sheria ile inazungumzia kwamba, fedha zote za Mfuko wa Barabara ni lazima zitumike kwa ajili ya matumizi ya barabara tu na si kwa matumizi mengine. Kwa hiyo, napenda kumhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama wana barabara mpya na kupitia Halmashauri husika wameamua kutumia fedha za Mfuko wa Barabara, kwa mujibu wa Sheria niliyoitaja ya Mfuko wa Barabara, inaruhusu kutumia fedha hizo za Mfuko wa Barabara katika matengenezo ya barabara. (*Makof*)

Kuhusu swalii lake la pili la barabara alizozizungumza ambazo ziko chini ya Halmashauri ya Wilaya; nataka nitoe wito kwa Waheshimiwa Wabunge wote, Halmashauri nyingi Tanzania, hazitumii vizuri fedha za Mfuko wa Barabara. Katika fedha ambazo zilitolewa, zaidi ya bilioni 36 katika *quarterya* tatu, Halmashauri zimekuja kuonekana nyingine hazijatumia hata senti tano katika fedha za Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo, nitoe wito kwa Wakurugenzi ambao wengi wanashindwa kuzitumia vizuri fedha za Mfuko wa Barabara, wazitumie kulingana na matakwa ya Sheria.

Sijajua katika Halmashauri yake ni kwa namna gani wametumia hizo fedha za barabara, lakini zipo pia Halmashauri zingine ambazo zimetumia vizuri sana fedha za Mfuko wa Barabara. Bahati nzuri, taarifa hizi tutawapa Waheshimiwa Wabunge, muweze kufuatilia vizuri namna fedha hizo zitakavyotumika kwa ajili ya kutengeneza barabarazinazohusika. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri jibu kama utakwenda, maana amekukaribisha kama uko tayari kwenda.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la pili la Mheshimiwa Desderius J. Mipata, kama

17 JUNI 2013

ifuatavyo:-

Kwanza, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa John Magufuli, kwa sababu katika *Policy issues* na nini, ndiye mhusika mkuu, hata kupandisha madaraja na hadhi ya barabara yeye ndiye anayetusaidia; nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, hili la pili, nilipokuja hapa Bungeni nimetoka kwake, yaani hivi ninavyozungumza hapa natokea Nkasi. Mheshimiwa Mipata ni mtu anayehangaika na Wananchi wake, anakwenda na kupanda na hii barabara anayoisema hapa ya Nkasi, hii barabara inaitwa Kitosi - Wampembe nayo pia alizungumzia na tulikwenda naye tukaiona sehemu fulani ya hiyo barabara.

Nataka tu nimwambie kwamba, nitakachofanya hapa sasa nitatuma watu wangu waende kule, maana kumwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Hawa Ghasia, nirudi tena kule, itakuwa ni ngumu kidogo. Nitatuma watu pale tuiangalie kwa uzito, kama anavyozungumza Mheshimiwa Mbunge na tutafanya yale yale; vinginevyo, ikibidi niende nitakwenda wala sina tatizo.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Samson Rweikiza atauliza swali hilo.

Na. 403

### **Huduma ya Mawasiliano ya Simu Bukoba**

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA** aliuliza:-

Vijiji vya Ibossa katika Kata ya Nyakato, Butainamwa katika Kata ya Kisharu, Nsheshe katika Kata ya Rukoma na vinginevyo, havina mawasiliano ya simu kutokana na kutokuwepo kwa mtandao wa kampuni ya simu:-

Je, ni lini vijiji hivyo vitapatiwa huduma hiyo muhimu sana?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jasson S. Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijiji, kama ifuatavyo:-

Sehemu kubwa ya Jimbo la Bukoba Vijiji inapata huduma ya Mawasiliano isipokuwa baadhi ya maeneo kama Vijiji vya Ibossa, Butainamwa na Nsheshe. Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imeyaainisha maeneo yote hayo na itashauriana na watoa huduma za mawasiliano kuhusu namna bora ya kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo. Aidha, pamoja na kuzishauri kampuni hizo kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo, Serikali kupitia Mfuko huo, imeyaingiza maeneo hayo kwenye Awamu ya I (A) ya Mradi wa Mawasiliano Vijiji, utakaotangazwa mwezi huu wa Juni, 2013. Mradi huu wenyе thamani ya Dola za Kimarekani milioni 14.3, sawa na shilingi bilioni 23.6, unasimamiwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCAF*); na inakusudiwa kuwa, ifikapo mwezi Oktoba, 2013 taratibu za zabuni zitakuwa zimekamilika na kazi ya kupeleka mawasiliano katika maeneo hayo itakuwa imeanza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza yafuatayo:-

(i) Wananchi hawa wa vijiji hivi vya Ibossa, Butainamwa, Nsheshe na vingine ambavyo havina huduma ya simu, hawakosi tu huduma ya simu, wanakosa pia huduma ya fedha; hizi huduma za *M-Pesa*, *Tigo-Pesa*, *Altel Money* na nyingine za mzunguko wa fedha; na kwa kuwa kukosekana kwa huduma hii kunazorotesha ukuaji wa Sekta ya Fedha ambayo nafikiri huzorotesha ukuaji wa Uchumi wa Taifa. Je, Serikali haioni kwamba ni vizuri kufanya haraka kusudi huduma zipatikane na huduma ya pesa iweze kupatikana haraka katika maeneo hayo?

(ii) Katika jibu lake Mheshimiwa Naibu Waziri amesema, Mradi huu una Dola milioni 14.3, ambazo ni sawa na shilingi

bilioni 23.6. Sijui maana yeke ni nini; una dola milioni 14; zipo tayari zinapatikana au ndiyo Bajeti yenyewe? Ningelipenda kupata ufanuzi zaidi na kama pesa hizo zipo na Mradi huu kuanza mara moja au ndiyo Bajeti hiyo?

**NAIBUWAZIRIWAMAWASILIANO, SAYANSINA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jasson Rwekiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tunapopeleka mawasiliano, siyo tu simu na *SMS*, vilevile na huduma za ziada, wanaita *Value Added Services*, ikiwemo huduma za kutuma pesa. Kwa hiyo, ni imani yetukwamba, kwa kadiri tunavyosogeza mawasiliano vijijini, siyo tu tunawasaidia Watanzania kupata huduma ya kupiga simu, lakini vilevile kupata huduma ya fedha.

Mheshimiwa Spika, wastani wa umbali kutoka mtu kwenye Benki ni kilometra hamsini kwa nchi yetu. Kutokana na huduma hizi za simu, wastani wa huduma ya fedha, kutuma, kupokea na kuweka, sasa hivi ni chini ya kilomita moja. Kwa hiyo, ni sahihi kabisa kwamba, tutapeleka huduma hizi ili huduma za fedha zipatikane.

Kuhusu sehemu ya (b) ya swali la Mheshimiwa Rwekiza, hizi fedha ambazo nimezitaja, dola milioni 14.3, ni fedha zote tulizopanga katika Awamu ya Kwanza (A) ya Mradi huu, ambao ni kata 168, vijiji zaidi ya 700, ndiyo ruzuku tuliyopanga kwa ajili ya kuyapatia Makampuni ya Simu, kupeleka huduma kwenye maeneo ambayo hayana huduma, ikiwemo maeneo ya Ibosa, Butainamwa na Nsheshe. (*Makof*)

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza hii Wizara, imejitahidi sana kufikisha mawasiliano ya simu katika nchi yetu kwa ujumla; lakini kuna Wananchi wanaoishi milimani ambao huduma hii hawajaipata. Je, Mheshimiwa Waziri unaweza kuniambia nini leo kuhusu Wananchi wanaoishi milimani na

17 JUNI 2013

wewe unaishi milimani pia? (*Makofi*)

**NAIBUWAZIRIWAMAWASILIANO, SAYANSINA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne K. Malecela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwa maeneo ya milimani, ambapo ndipo anapotoka Mheshimiwa Kilango na ndipo ninapotoka mimi, kuna changamoto mahususi kabisa za mawasiliano. Unaweza ukauona mnara uko pale, lakini simu yako haina mtandao kutokana na mawimbi yanavyokwenda na wanaita *dark pockets*.

Kwanza, tumekuwa tunaongea na Makampuni ya Simu ambayoyamepeleka mawasilianokwenyemaeneoya milimani, yajaribu kuboresha *signals* zao ili maeneo mengi yafikiwe zaidi. Vilevile katika utaratibu huu wa *UCAF*, tumeongea na *Engineers* wetu kule, waangalie utaratibu kwa sababu tunapata tatizo; unakuta eneo ni dogo, ambalo kwa hali ya kawaida kama lingelikuwa ni tambarare, lingelihitaji minara mitatu, lakini kutokana na hali ya milima linahitaji minara mpaka minane.

Kwa hiyo, tunaangalia na *Engineers* pale wa *UCAF* kuona teknolojia rahisi zaidi ya kupeleka mawasiliano, ikiwemo minara midogo inayoweza kupeleka mawasiliano kwa kijiji, kwa watu wachache. Utakapofika mwezi Agosti na Septemba, watakuja na jawabu kama wenzetu wa Makampuni ya Simu watakubali kushirikiana na watu wanaotoa teknolojia rahisi ya namna hiyo, kuliko ile minara yao mikubwa inayofanana nchi nzima, ingawa mazingira ya nchi yetu hayafanani.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo. Kwa kuwa katika majibu yake, Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza jitihada ambazo zinafanywa na Serikali na tayari Kandarasi zilikwisha tangazwa. Mwaka 2012 Kandarasi zilitangazwa na kwa bahati mbaya sana katika Mkoa wa Rukwa hakuna Mkandarasi aliyejitokeza hata mmoja:-

Je, Serikali ina mpango gani wa makusudi kuhakikisha

17 JUNI 2013

kwamba mawasiliano yanafika Mkoa wa Rukwa? (*Makofi*)

**NAIBUWAZIRIWA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kadege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, tulitangaza kuanza zabuni ya majaribio (*Pilot*), mwaka 2011 siyo mwaka 2012, bahati mbaya, zabuni ile haikufanikiwa, kwa sababu hakuna makampuni yaliyojitokeza. Mwaka 2012 tukatangaza zabuni mpya kupitia fedha hiziza Benkiya Dunia katika Kata 152 ambazo tulitangaza, Kata 52 peke yake ndipo wazabuni walijitokeza na baadhi ya maeneo hawakujitokeza kabisa; na kule ambapo walijitokeza tuliwaandikia Wabunge rasmi kwamba, tumepata wazabuni na makampuni ili na wao wasaidie kufuatalia.

Sasa katika hiyo Awamu ya Kwanza (B), ambacho tumefanya ni kuchukua yale maeneo ambayo Wazabuni hawakujitokeza na kuongeza ruzuku na kuongea nao kujua vitu gani havikuwavutia kwenda kule ambako tulitangaza mwanzo. Kwa hiyo, siyo tu kuongeza ruzuku, bali tumekuwa tunafanya mazungumzo na Makampuni ya Simu haya, yatuambie na yatusaidie kutushauri kuhusu namna ya kuboresha huu Mfuko. Kwa hiyo, tuna imani kwamba, hii awamu tunayoitangaza sasa, ambayo ni kiasi kikubwa cha fedha na Kata nyingi zaidi, maeneo yote watajitokeza.

Licha ya juhudzi za Mfuko, Makampuni ya Simu nayo tumeyahimiza kwamba nayo yatupe mipango yao ya kupeleka mawasiliano vijijini katika miaka mitatu ijayo. Maeneo hayo ni mengi, bahati nzuri wametuletea; ni mno kuliko maeneo ambayo sisi tunapeleka kama Mfuko.

Waheshimiwa Wabunge, ambao watapenda kujua maeneo hayo, kwa sababu taarifa hizi ni za Makampuni ya Simu, ni taarifa binafsi za kibiashara, hatuna ruhusa ya kuzitangazal; kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ambaowangelipenda kujua kuhusu maeneo yao, kama Makampuni ya Simu yataenda nje ya utaratibu wa Mfuko, basi tuko tayari kuwaonesha orodha hiyo. (*Makofi*)

17 JUNI 2013

Na. 404

### **Hitaji la Mawasiliano Kilolo**

**MHE. PROF. PETER M. MSOLA** aliuliza:-

Wananchi wa Kijiji cha Nyanzwa Wilayani Kilolo ni Wakulima na Wafanyabiashara lakini wanakosa mawasiliano ya simu kwa muda mrefu licha ya kufikisha maombi yao kwa wahusika:-

Je, Serikali itawasaidiaje Wananchi hao kupata huduma ya mawasilino hasa kwa ajili ya Vijiji vya Nyanzwa, Irole, Isagwa, Kising'a, Kimala, Ibumu na Ilamba Wilayani Kilolo?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter M. Msolla, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, imekuwa ikiendelea na mpango wa kuhakikisha kuwa, maeneo yote yasiyo na huduma ya mawasiliano hususan yaliyoko vijijini na maeneo ya mipakani mwa nchi yetu, yanapata huduma hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Vijiji wa Nyanzwa (Kata ya Mahenge), Irole na Isagwa (Kata ya Ilula), Kijiji cha Kising'a (Kata ya Ukwega), Kimala (Kata ya Idete) pamoja na Vijiji vya Ibumu na Ilamba (Kata ya Image), viro katika orodha ya Kata zitakazotangazwa katika Zabuni ya Awamu ya Kwanza (A) ya Mradi wa Mawasiliano kwa wote Vijijini. Mradi huo, unalenga kupeleka mawasiliano kwenye Kata 168, zenye vijiji 936, kwa wakazi wapatao 1,322,753. Mradi unakusudiwa kutangazwa mwezi huu wa Juni, 2013. Aidha, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali itaendelea na jitihada zote zinazowezekana kuhakikisha kwamba, maeneo yote yasiyo na mawasiliano nchini, yanapata mawasiliano kabla ya mwaka 2015 kama tulivyoahidi kwenye llani yetu.

**MHE. PROF. PETER M. MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri, ningelipenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 2012 mwezi Machi, Kampuni ya *Airtel*, ilikwenda Nyanza na kuwaomba Wananchi wachimbe barabara kuelekea Mlimani, kilomita tatu. Wananchi wamefanya kazi hiyo, barabara imechimbwa, lakini Kampuni hiyo haijarudi tena kuendelea na taratibu za kuweka minara. Je, Serikali itatusaidiaje ili Wananchi wa Nyanza waweze kupata mawasiliano hayo?

(ii) Katika Mpango wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote umeeleza kwamba kutakuwa na vijiji 936 vitakavyonufaika. Je, Wizara haioni umuhimu wa kuweka ratiba kamili (*time frame*) ili kila eneo wajue ni lini wategemee kupata mawasiliano hayo?

**NAIBUWAZIRIWA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, kama ifuatavyo:-

Kuhusu suala la Kampuni ya *Airtel* kwenda Nyanza na kuwahimiza Wananchi wachimbe barabaraka ajiiliya kupeleka mnara; napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge ya kwamba, nitasaidia kuwauliza nini kilitokea mpaka hawakurudi tena na nitampa Mheshimiwa Mbunge majibu nitakayopewa na Kampuni hiyo.

Kuhusu ratiba ya upelekaji wa mawasiliano kote nchini; hili ni jambo la msingi na sisi tungelipenda Wabunge wawe na uhakika, kwa sababu na wao wanawasiliana na Wananchi, ni vyema wakawaeleza ili ahadi zetu tunazozitoa zisionekane hewa.

Kama kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hawana kile kitabu tulichokigawa, basi watuone tutawapa tena; kinaeleza maeneo ambayo tumeyatangaza kwa sasa, lini zabuni zitatangazwa na lini ujenzi unatarajiwa kuanza. Kitabu kile hakichoshelezi, bado yako maeneo mengi ambayo hayako mle. Tutakapomaliza sasa awamu hizi mpaka ya pili

ambapo tumewe ka kwenye kile kitabu, kuna maeneo mengi zaidi ambayo tutayatoa. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ambao hawataona maeneo yao mle ndani, wasife moyo kwa sababu bado tunaendelea na hii kazi.

Kama nilivyosema, kazi ya kupeleka mawasiliano vijijini siyo ya *UCAF* peke yake na siyo ya Serikali peke yake, makampuni nayo yanao wajibu vilevile wa kufanya hivyo. Mpango huu wa *UCAF* ni kama *Carrot* kwa sababu unatoa fedha, unatoa ruzuku. Serikali kupitia Sera na Sheria, tunao uwezo wa kubadilisha aina ya *incentives*, kuhakikisha kwamba, makampuni haya yanapeleka kwa lazima mawasiliano. Tunaamini kwamba, hatujafika huko bado, lakini tutakapofika hatutasita kutoa masharti ikiwemo kuchukua masafa katika maeneo ambayo makampuni haya yamepewa masafa kwa nchi nzima. Itakapofika mahali kwamba, pamoja na hii *carrot*, pamoja na hii ruzuku, bado hawaendi, basi itabidi tuangalie utaratibu mwininge wa kuwalazimisha wapeleke mawasiliano kule ambako hakuna mawasiliano.

**MHE.DUNSTAND.MKAPA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kwanza, naishukuru Serikali na nina imani kwamba, ahadi ilioitoa ya kuweka minara kule Nanyumbu wataitimiza bila wasiwasi.

Swali langu ni kwamba, hivi hakuna teknolojia nydingine ya kupeleka haya mawasiliano mpaka kwa minara tu; nina wasiwasi tutakosa sehemu ya kulima kwa sababu ya minara mingi?

**NAIBUWAZIRIWA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalila Mheshimiwa Dunstan D. Mkapan, kama ifuatavyo:-

Ipo teknolojia nydingine ya kupeleka mawasiliano bila kuweka mnara; kwa mfano, *satelite*, zipo simu za *satelite*, ambazo hauhitaji mnara, lakini ni gharama kubwa sana, ambazo Watanzania hatuwezi kuzimudu hata wale wa kipato cha juu. *Satelite Phones* ni ghali mno.

Mheshimiwa Spika, minara inachukua eneo dogo sana, chini ya mita za mraba 20. *In fact*, ukiweka mnara unapaswa kulipwa, *either*, mwenye eneo au kijiji na fedha ambazo unalipwa kwa kuweka mnara ni nyingi kuliko kitu chochote ambacho ungeweza kulima kwenye lile. Kwa hiyo, kama ni suala la kipato na kukosa sehemu za kulima, mimi ningekuwa na eneo langu, kuliko kulima maharage, ningependa eneo hilo liwe na mnara ili niweze kupata kipato cha uhakia kwa mwaka. Ninashukuru.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa kuwa Makampuni ya Simu yanapeleka minara maeneo ambako yana-*interest*, yana faida kibashara. Hii ruzuku ya Serikali kwa nini isiende vijijini ambako hii mitandao ya simu haina *interest*; msipange fedha kwenye Mfuko huu maeneo ambayo wao wenyewe watakuwa na *interest* katika maeneo ya mijini wanajua watapata faida?

**NAIBUWAZIRIWA MAWASILIANO, SAYANSI NATEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Felix Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge, anaonesha jinsi ambavyo hana uelewa kabisa kuhusu dhana nzima ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote. Dhana ya Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ni kupeleka mawasiliano vijijini ambako hakuna mvuto wa biashara, hiyo ndiyo dhana ya msingi. (*Makof*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo sana la nyongeza.

Kwa kuwa tayari Mfuko huu wa UCAF umetenga shilingi milioni 350 kwa ajili ya mawasiliano mpakani mwa Tanzania na Msumbiji kule Muhukuru: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atanihakikishia kwamba maeneo yaliyobakia ya Ndongosi, Wino na kule Ifinga, yatakuwa katika Awamu ya Pili anayoisema ambayo atatuletea ndani ya Bunge hili taarifa zake?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, jibu, lakini ni swali jipya kabisa!

17 JUNI 2013

**NAIBUWAZIRIWAMAWASILIANO, SAYANSINATEKNOLOJIA:**  
Mheshimwia Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jenista  
Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Spika, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Mhagama kwa muda mrefu sana amekuwa anahangaika na baadhi ya maeneo yake, hasa yaliyoko mpakani mwa Tanzania na Msumbiji. Bahati nzuri, tumefanikiwa kutenga fedha kwa ajili ya Makampuni ya Simu kupeleka mawasiliano kwenye eneo moja hasa la Muhukuru, ambalo liko mpakani. Maeneo yaliyobaki, ninapenda kumhakikishia kwamba, tutafanya hivyo na tutampa taarifa ni lini tutapeleka mawasiliano.

Ningelipenda baadaye nimpe Kitabu hiki ambacho kinaoneshadhananzimaya Mfuko. Mheshimiwa Felix Mkosamali, ninaomba nikupe Kitabu ambacho kinatoa maeleo ya nini maana ya *UCAF* na Mheshimiwa Mhagama nitakusaidia kitabu hiki ili uweze kupata ratiba ya lini tutapeleka maeneo ambayo hayana mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hivyo vitabu wape Wabunge wote siyo hao tu uliowataja. Tunaendelea na swali linalofuata.

Na. 405

### **Bajeti ya Afya Kuongezwa Kufikia Asilimia 15**

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA** aliuliza:-

Azimio la Abuja (2001) linaagiaza Bajeti ya Afya kufikia asilimia 15 kufikia 2012 lakini Bajeti hiyo imeendelea kushuka kufikia asilimia 8.8 mwaka 2012/2013:-

Je, Serikali haioni kuwa bajeti finyu kama hiyo ndiyo chanzo cha upungufu wa dawa na vifaa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa Azimio la Abuja, ambalo linataka Bajeti ya Afya ifikie asilimia 15 ili iweze kuboresha Sekta ya Afya nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikiongeza Bajeti ya Wizara ya Afya na Sekta nyingine kadiri mapato yake yanavyoimarika. Ufinyu wa Bajeti haupo katika Wizara ya Afya peke yake, bali ni suala linalotokana na upungufu wa mapato ya Serikali. Aidha, upungufu wa vifaa na madawa ingawa unaweza kusababishwa na ukosefu wa rasilimali fedha, pia hutokana na matatizo kadhaa, ikiwa ni pamoja na mfumo wa usambazaji na ukosefu wa umakini katika ununuzi wa madawa. Hata hivyo, kwa sasa Bajeti ya Sekta ya Afya imefikia shilingi bilioni 1,288, ambayo ni sawa na asilimia kumi ya Bajeti yote. (Makof)

**MHE. ROSWEETER F. KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri sana. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa katika jibu lake la msingi Mheshimiwa Naibu Waziri, amejibu kwamba, kuna tatizo kubwa sana la mfumo wa ununuzi, usambazaji wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba kwenye zahanati zetu. Pamoja na kutambua huo mfumo wenye matatizo; je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha huo mfumo ili Wananchi waendelee kupata huduma bora za afya? (Makof)

(ii) Miaka mitatu iliyopita Serikali iliahidi kutenga asilimia moja ya *GDP* kwa ajili ya Vyuo Vikuu kufanya Tafiti mbalimbali, ikiwa ni pamoja Chuo Kikuu cha Muhimbili, lakini mpaka sasa hivi ahadi hiyo hajatimizwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza hiyo ahadi yake ili Chuo cha Muhimbili kiweze kufanya tafiti mbalimbali za magonjwa, madawa na chanjo kwa ajili ya Wananchi? (Makof)

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza  
ya Mheshimiwa Rosweeter Kasikila, kama ifuatavyo:-

Kwanza, mfumo wa usambazaji, tunachozungumza hapa ni kweli kwamba, kuna matatizo katika mfumo mzima wa usambazaji. Kama nilivyoeleza awali; Serikali tutaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya kuangalia suala zima la Sekta ya Afya. Vilevile tutashirikiana na Wizara ya Fedha, kuona *how best* tunaweza tuka-*improve* huo mfumo wa usambazaji, pengine matatizo mengine yalitokea kutokana na madeni ya *MSD* na kadhalika. Kwa hiyo, tutashirikiana kwa pamoja na Wizara ya Afya, kuangalia vipi hasa tunaweza ku-*strengthen* huu mfumo wa usambazaji.

Vilevile kwa sababu tunalolenga hapa ni kwamba, labda Serikali ndiyo ipeleke fedha kwa ajili ya hii Sekta ya Afya; naomba Waheshimiwa Wabunge, tuwashajihishe Wananchi wetu kuweza sasa kujiunga na Bima ya Afya, nayo pia itaweza kusaidia kuboresha upatikanaji wa afya kwa Wananchi wetu huko waliko.

Suala lingine ni kwamba, ahadi ya Serikali kwenye utafiti ni asilimia moja, lakini nayo si tu kwa Muhimbili, ni asilimia moja ya kufanya utafiti katika sekta mbalimbali; kwenye kilimo kuna utafiti, kwenye afya yenyewe kuna utafiti na hata kwenye fedha kwenyewe vilevile kuna utafiti. Kwa hiyo, hili nalo tutaendelea kulifanyia kazi, lakini *focus* kama ikiwa ni Wizara ya Afya tutaangalia *how best we can go* kuweza kusaidia hiki Chuo cha Afya Muhimbili kuweza kufanya utafiti wake. Hii inakwenda sambamba na kuongeza bajeti ya Sekta ya Afya kwa ajili ya kufikia lengo hili.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri, swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Tanzania tumefanikiwa kupambana na maambukizi ya UKIMWI kwa muda mrefu kwa kutumia *USAID* ambayo ni misaada inayochangiwa na nchi imbalimbali; na kwa kuwa sasa wale waliokuwa wanachangia Mfuko huu wameanza kutangaza kupunguza lile fungu lililokuwa linawekwa pale lakini pia wametangaza kukatisha kabisa misaada hii ifikapo mwaka 2014. Ninapenda kujua sasa pamoja na kuwa bajeti ni chache kwenye Wizara hii; je, Wizara imejipanga vipi kuhakikisha tutaendeleza mapambano ya UKIMWI kwa kutumia fedha za ndani ya nchi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. SAADA MKUYA SALUM):**  
Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalila Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na taarifa zao kwamba watakatisha misaada, hilo sina uhakika nalo; lakini napenda kusema kwamba, tunapopambana na maradhi kama haya, siyo Serikali tu peke yake, bali kuna *NGOs* nyingi sana ambazo fedha zake kweli sisi kama Serikali hatujaweza kuzi-*capture* kwa ajili ya kuona *how much* wao vilevile wanasaki katika mapambano hayo ya UKIMWI.

Kupambana na UKIMWI hakuendani peke yake na kutibu, lakini kinga nayo ni chanzo muhimu sana. Kwa hiyo, wakati *donors* labda wanasema kwamba, hawatasaidia sisi Waheshimiwa Wabunge tuwashajihishe Wananchi wetu katika kukiinga zaidi, kwa sababu kinga ndiyo muhimu hata kuliko tiba. Kwa hiyo, wakati tunaelekea huko, nadhani nguvu zaidi tuelekeze katika kuwashajihishe Wananchi kupambana kabisa na vyote vinavyochochea kuongezeka kwa maradhi ya UKIMWI pamoja na maradhi mengine.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara inayofuata ya Uchukuzi. Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, atauliza swali hilo.

17 JUNI 2013

Na. 406

## Vyombo vyatuhakika na anga

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR** aliuliza:-

Nchi nyingi duniani zinamiliki Mashirika ya Usafirishaji wa Majini na Angani kama vile Meli, Treni, Ndege na kadhalika na mfumo huo unanufaisha nchi husika kwa kutambulika na kujipatia kipato kikubwa kwa maendeleo ya Wananchi wake:-

Je, kwa nini Tanzania bado haina uhakika na vyombo vyatuhakika na anga ambavyo vinaaminika?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohammed Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Uchukuzi, inalo jukumu la kuhakikisha kuwa, kunakuwepo na huduma bora za usafirishaji na uchukuzi za uhakika na gharama nafuu ili kuchangia katika ukuaji wa uchumi na shughuli za kijamii nchini. Kama ilivyo kwa baadhi ya nchi Duniani, Serikali kupitia taasisi zake zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi, inamiliki vyombo vyatuhakika na anga ambavyo hutoa huduma za usafiri wa majini, reli na anga. Serikali ya Tanzania inamiliki kwa pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Kampuni ya Kimataifa inayotoa huduma ya usafiri wa majini iitwayo *China Tanzania Joint Shipping Company* au *SINOTASHIP*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa yanayotokana na kuwepo kwa makampuni hayo, Serikali bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali za uendeshaji wa makampuni hayo, ikiwa ni pamoja na mitaji midogo ya uendeshaji, menejimenti dhaifu na vyombo vyatuhakika na vitendeakazi chakavu. Hali hiyo inasababisha huduma za baadhi ya makampuni hayo ya Serikali kutokuwa za uhakika na kuaminika.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeimarisha usimamizi wa taasisi hizo kwa kuondoa Bodi na Menejimenti zilizo legelege na kufungua milango ya ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za uchukuzi nchini. Ili kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za makampuni hayo kwa viwango vyatubu wa hali ya juu, Serikali imekuwa ikitenga fedha katika bajeti yake kila mwaka. Katika kuboresha huduma za usafiri wa majini, katika kipindi cha muda mfupi, Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark, imeanza taratibu za kukarabati meli zinazotoa huduma katika Maziwa Makuu na pia kujenga meli tatu mpya, yaani kila moja katika Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Ujenzi wa meli hizo mpya unatazamiwa kukamilika mwaka 2018. Aidha, Serikali ya Ujerumani itasaidia katika ukarabati wa meli moja ya MV Liemba inayotoa huduma katika Ziwa Tanganyika. Vilevile Serikali inaendelea na taratibu za kuchukua madeni yote ya ATCL ili kuboresha mizania yake na kuiwezesha iboreshe uendeshaji na utoaji wa huduma zake.

**MHE. FAIDA MOHAMMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(i) Kwa kuwa vyombo vyatubu wa anga na baharini vingi ni vyatubu makampuni binafsi na baadhi yake ni vibovu, jambo ambalo husababisha maafa makubwa kwa Wananchi. Je, Serikali itasitisha lini safari za vyombo hivyo ambavyo ni vichakavu?

(ii) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati mwafaka wa kuweka Bima kwa wasafiri wanaosafiri kwa vyombo vyatubu wa anga na vyatubu baharini ili pale yanapotokea majanga waweze kulipwa Bima hizo? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Faida Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, vyombo vingi vinavyotumika kwa usafirishaji na uchukuzi hapa nchini, vinamilikiwa na watu binafsi na viro ambavyo ni chakavu na

vibovu. Sheria ya Usafirishaji wa Majini na Nchi Kavu kupertia Taasisi yetu ya *SUMATRA*, wanafanya usimamizi na ukaguzi wa vyombo hivi na vile vinavyoonekana kwamba havikidhi viwango, basi vyombo hivyo huzuiliwa kutoa huduma.

Swali la pili, wasafiri wa anga wamewekewa Bima, ndege inapokatiwa Bima ndani yake inakuwepo pia Bima kwa ajili ya wasafiri wanaotumia ndege. Hivyo hivyo, katika vyombo vya majini, Bima hizo zinakuwa zimehusisha wasafiri na mali zinazokuwemo katika vyombo hivyo.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Kwa kuwa hivi karibuni Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alifanya ziara nchini Oman; baada ya ziara ile kama ingekuwa ni *coincidence* au ni kwa dhamira, alijitokeza Mwarabu na kuja mpaka Tanzania na kusema kwamba *ata-inject about hundred million dollars* ili kuokoa na kulifufua Shirika letu la *Air Tanzania*, lakini hadi leo kimya kimekuwa kirefu, hatujapata taarifa zozote. Tunaomba tupate taarifa za Mwarabu huyo na uwekezaji wake umefikia wapi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Haya, ilikuwa usalama wa vyombo leo imekuwa uwekezaji. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli baada ya ziara ya Mheshimiwa Rais nchini Oman, alikuja mfanyakiareshara mmoja kutoka nchi hiyo na akaenda katika Ofisi za *ATCL*, kwa lengo la kufanya mazungumzo kuona namna gani angeweza kuweka mtaji wake ndani ya Shirika lile. Alikwenda pale na waandishi wa habari, zikapigwa picha nyingi, akazi peleka huko kwao na kutangaza kwamba amekubaliana na *ATCL* kuweka fedha kiasi

17 JUNI 2013

cha dola milioni 100 ili kulifufua Shirika hilo. Katika mazungumzo yaliyotokea pale, hapakuwepo na ahadi hiyo, hata wao *ATCL* walishangaa walipoona katika vyombo vyahabari vya huko Uarabuni akitaja mabilioni hayo ya fedha wakati mazungumzo yaliyofanyika nao hayakuwa yamezungumzia mamilioni mengi ya namna hiyo ya fedha. Amekwenda hajaonekana tena tangu aseme mtaji huo.

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Maji, muda umekwisha. Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, kwa niaba yake Mheshimiwa Mkosamali!

Na. 407

### **Wakazi wa Kigoma Ujiji Kufungiwa Dira za Maji**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. SABREENA H. SUNGURA)** aliuliza:-

Wakati akijibu hoja za Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Maji aliagiza kwamba wateja wote wa maji katika Manispaa ya Kigoma Ujiji wafungiwe dira ndani ya miezi mitatu ili kila Mwananchi aweze kulipia alichotumia na hadi sasa ni asilimia 50 tu ya watumiaji ndiyo wamefungiwa dira tena kwa gharama zao wenyewe:-

Je, Serikali sasa iko tayari kuchangia gharama iliyobaki ili kukamilisha zoezi hilo na kupunguza makali ya maisha kwa Wananchi hao?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI** aliujibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, la tarehe 11 Juni, 2013, kuhusiana na agizo la Mheshimiwa Waziri wa Maji juu ya ufungaji wa dira za maji kwa wateja wote wa Manispaa ya

Kigoma. Wakati akitoa agizo hilo, mwezi Julai, 2012, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kigoma ilikuwa na wateja 8,441, kati yao, wateja 3,603 walikuwa tayari wamefungiwa dira za maji, sawa na asilimia 43. Baada ya agizo hilo, Serikali kupitia Mamlaka imenunua na kufunga dira mpya 1,004, sambamba na kufufua dira 890; hivyo, kufikia asilimia 64 ya wateja waliofungiwa dira kwa sasa. Dira hizo zimenunuliwa kwa kutumia fedha za maduhuli ya Mamlaka ya Maji; hivyo, hakuna mteja aliyefungiwa dira kwa gharama zake.

Mheshimiwa Spika, tarehe 13 Juni, 2013, Mamlaka imesaini mkataba na mzabuni atakayenunua na kufunga dira 700 chini ya ufadhili wa Mradi wa Uhifadhi wa Ziwa Tanganyika (*Lake Tanganyika Integrated Programme*). Hadi kufikia mwezi Agosti, 2013, asilimia 74 ya wateja wa Mamlaka ya Kigoma watakuwa wamefungiwa dira za maji. Zoezi hili litakuwa endelevu ili kuhakikisha kuwa, Wananchi wanalipia maji kulingana na matumizi yao.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Maeneo mengi nchini ikiwemo Manispaa ya Kigoma, Mamlaka za Maji zinatoza watu bila mita, yaani wanakadiria tu halafu wanatoza watu. Sasa Serikali inasemaje; siyo kwa Kigoma peke yake, maeneo mengi ikiwemo Kibondo na maeneo mengine, wanatoza kwa kukadiria; mchezo huu wa kukadiria watu na kuwatoza fedha nyingi utaisha lini?

(ii) Mheshimiwa Waziri anasema kwamba watu hawajatumia gharama zao kufunga mita: Je, tukileta ushahidi wa watu ambao wametozwa fedha atatuambia nini baada ya kutoa majibu haya anayoyasema?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Kwanza, siyo kweli kwamba, Mamlaka za Maji zinatoza matumizi ya maji kwa Wananchi kwa kukadiria; zipo taratibu

zinazotumika kufikia kiwango chochote ambacho kinakuwa kimekubaliwanazoezizimalakufikiakiwangohicholinasimamiwa na *EWURA*. Kwa hiyo, wapo wale ambao wanatumia mita na wapo wale ambao hawatumii mita. Sasa ile bei panapokuwa hakuna mita lazima kuwe na makubaliano ambayo *EWURA* inakuja kufanya vikao na watumiaji maji na kukubaliana ile *flat rate* iwe kiasi gani, baada ya kukubaliana hiyo bei ndiyo inaweza ikatumika. Mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba, watu wote wanawekewa mita.

Pili, kwamba watumiaji wengi wana ...

Naomba nichukue swalii.

**SPIKA:** Anasema akitoa ushahidi kwamba watu wanalipa utafanyaje?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge anilettee huo ushahidi ili tuweze kusema ni namna gani na hatua gani zichukuliwe. Namhakikishia kwamba, hakuna mahali ambapo watu wanalipa fedha zao kwa ajili ya kuwekewa mita, lakini kama ushahidi upo atuletee tutaufanyia kazi.

**MHE. DKT. PETER D. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa matatizo ya Mji wa Igunga yanafanana sana na Kigoma Ujiji; na kwa kuwa chujio lililokuwa linajengwa kwenye Bwawa la Ulenya halikukamilika vizuri; je, Serikali itakamilisha lini chujio hili ili Wananchi wa Igunga waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kafumu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mikakati tuliyojiwekea Wizara ya Maji hasa katika matokeo ya haraka, *Big Results Now*, ni kwamba, tumelenga kupeleka miundombinu kwenye Miradi ambayo inaleta matokeo ya haraka na Miradi ya matokeo ya haraka ni pamoja na mabwawa ambayo yamejengwa

17 JUNI 2013

hayakuwekewa hiyo miundombinu.

Kwa hiyo, nina hakika Mradi anaousema Mheshimiwa Mbunge, utaingizwa kwenye fedha ambazo zimeongezeka bilioni 184.5 na hivyo utatekelezwa ili Wananchi waweze kupata maji.

Na. 408

### **Utekelezaji wa Sera ya Lugha ya Taifa**

**MHE. GOSBERT B. BLANDES (K.n.y. NYAMBARI C. M. NYANGWINE)** aliuliza:-

Sera ya Lugha ni uamuzi unaohusu uchaguzi wa lugha za kutumiwa katika nyanja mbalimbali zinazodhibitiwa na Vyombo vya Dola kama vile Bunge, Shule, Mahakama, Diplomasia ya Kimataifa na kadhalika:-

- (a) Je, hapa nchini Tanzania kuna Sera ya Lugha?
- (b) Kama ipo; je, Sera hiyo ya Lugha imeipatia hadhi gani Lugha ya Kiswahili?
- (c) Je, kuna mkakati gani mahususi wa kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa Lugha ya Kufundishia kwa viwango vyote vya elimu hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mbunge wa Tarime, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, Nchini Tanzania hakuna andiko mahususi au linalosimama pekee kama Sera ya Lugha, bali suala la lugha limezingatiwa kama Sura Maalum muhimu ndani ya Sera ya Utamaduni ya mwaka 1997.

(b) Mheshimiwa Spika, katika andiko hilo la Sura ya Utamaduni, Kiswahili kimetambuliwa kuwa siyo tu lugha ya mawasiliano mapana nchini, bali pia kuwa ni Lugha ya Taifa na mojawapo ya Lugha Rasmi za Taifa letu, yaani Kiswahili na Kingereza.

(c) Mheshimiwa Spika, mionganini mwa mikakati mahususi ya kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kufundishia ni jitihada zinazoendelea za Wataalamu wa Asasi za ukuzaji wa Kiswahili humu nchini, ambazo ni kuboresha Sarufi ya Kiswahili, kutunga Kamusi za Kiswahili za masomo na taaluma mbalimbali, kuandika vitabu vya kiada na ziada vya Kiswahili vya masomo ya sekondari na vyuo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri, lakini nataka kufahamu yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa mnamo mwaka 2004 *African Union* ilipitisha Kiswahili kiwe ni lugha ambayo itatumika katika mikutano na shughuli mbalimbali. Je, Serikali imejiandaa vipi kupeleka wakalimani wa kutosha kutoka Tanzania ili waweze kujipatia ajira?

(ii) Kwa kuwa Lugha ya Kiswahili imekuwa ni Lugha yetu ya Taifa hapa; ni lini Serikali itapitisha Kiswahili kutumika kufundishia kuanzia Shule za Msingi mpaka Vyuo Vikuu?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Blandes kama ifuatavyo:-

Nakubaliana naye kwamba, kulipitishwa azimio hilo na kwamba, Tanzania inaona hiyo ni fursa muhimu. Tayari moja ya kazi ambazo zinafanywa na Taasisi za Kukuza Kiswahili; BAKITA, BAKIZA na TATAKI, ni kuongeza wataalam zaidi ili waweze kupata ajira hiyo. Pia Tanzania kama Tanzania, pale Addis Ababa tayari tuna kituo chetu cha kufundishia Lugha ya Kiswahili, lengo likiwa ni kuona tunatumia fursa hiyo ya kuwa na

17 JUNI 2013

wakalimani katika Mikutano hiyo ya Kitaifa.

Nimeeleza kwamba, jitihada zinafanywa na taasisi hizi za kukuza Kiswahili, mojawapo ni kuongeza wataalam na kuandika vitabu vingi ambavyo vinaweza vikatumika kufundishia. Nasema wazo hilo tumelipokea na sisi ndani ya Serikali tutaendelea kulifanyia kazi. Hata wakati tunawasilisha bajeti ya Wizara yetu hapa, ilitolewa hiyo hoja kwamba, Kiswahili kifundishwe kuanzia Shule za Msingi, Sekondari na Vyuoni. Hilo tumelipokea na tutalifanyia kazi.

**SPIKA:** Tunaendelea na swali linalofuata, kutokana na muda Waheshimiwa. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, atauliza swali hilo na kwa niaba yake Mheshimiwa Moses Joseph Machali!

Na. 409

### **Mfumo wa Dijitali na Haki ya kupata Habari**

**MHE. MOSES J. MACHALI (K.n.y. MHE. CECILIA D. PARESSO)**  
aliuliza:-

Mfumo wa Dijitali umewanyima Wananchi wengi haki yao ya Kikatiba ya kutafuta na kupokea habari bila kujali mipaka ya nchi (lbara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania) na mfumo huu unahitaji ving'amuzi ambavyo bei yake ni ghali na Wananchi wengi hushindwa kuvinunua na hivyo kushindwa kupata habari:-

Je, Serikali inatoa tamko gani?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia D. Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, kila Mwananchi ana haki ya Kikatiba ya kutafuta na kupokea habari bila kujali

mipaka ya nchi. Kuna njia mbalimbali ambazo Mwananchi anaweza kutumia ili kupata habari kama vile magazeti, redio, televisheni na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, haki ya kupata habari ni lazima iambatane na wajibu wa Mwananchi kununua gazeti, redio au televisheni. Ili kuona matangazo ya dijiti, Mwananchi hana budi kununua televisheni yenye uwezo wa kushika mawimbi ya dijiti, ama kuendelea kutumia televisheni ya analoji na kununua visimbuzi ili aweze kupata matangazo kwa mfumo wa dijiti. Gharama za visimbuzi zinatofautiana mionganini mwa mawakala watatu waliopewa leseni. Aidha, ni asilimia 24 tu ya Watanzania wote ndiyo wanaopata matangazo ya televisheni. Hivyo basi, siyo kweli kwamba mfumo wa dijiti umewanyima Watanzania wengi haki yao ya Kikatiba ya kutafuta na kupokea habari.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasisitiza kuwa, zoezi la uhamaji kutoka mfumo wa analoji kwenda dijiti ni endelevu ili kukidhi matakwa ya Shirika la Mawasiliano Duniani (), ambalo linataka nchi zote duniani ziwe zimezima mitambo ya analoji ifikapo Julai, 2015.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri, maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Pamoja na kwamba, majibu yake ni mabaya na hayaridhishi, napenda nimwambie Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, mfumo wa dijiti umewanyima Wananchi walio wengi haki ya kuweza kupata habari. Mheshimiwa Naibu Waziri, anataka kutueleza sisi Wabunge pamoja na Wananchi wengine kwamba, maeneo mengine ambayo walikuwa wanatumia teknolojia ya analoji mitambo imezimwa halafu watu hawana uwezo wa kununua hivyo visimbuzi. Leo anataka kutuambia kwamba watu hao wanapata habari na wakati hawana hizo *decoders*. Ningependa Waziri atoe ufanuzi ni kwa nini anadiriki kusema uongo wakati watu wamekosa uwezo wa kununua visimbuzi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Machali, ukitumia maneno mazuri zaidi kuliko kusema uongo unaweza ukafikisha *message* tu. Hebu ondoa hayo maneno ya uongo.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, basi naondoa neno hilo na nitumie neno kwamba, amezungumza kinyume na uhalisia kwa sababu watu hawapati habari kutokana na kukosa uwezo wa kununua visimbuzi.

(ii) Serikali imekuwa na kigugumizi cha kuruhusu matumizi sambamba ya dijiti pamoja na analogi. Kama hakuna rushwa wakati mwingine kwa baadhi ya Watendaji wa Serikali pamoja na Viongozi Wakuu wa Wizara, kwa nini Serikali isiruhusu matumizi sambamba ya teknolojia zote mbili ili wakati huu mfumo wa dijiti haujtengemaa Wananchi wote waweze kupata habari kama ilivyokuwa siku za nyuma; kuna tatizo gani kuweza kuruhusu mifumo yote hii miwili kutumika? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme tu kwamba, majibu niliyotoa ni sahihi sana na hayajaenda kinyume na alivyotegemea yeye. Sasa nijibu maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Kwanza, Mwananchi anayo haki ya kupata habari kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, kwa kupitia katika magazeti, redio, mitandao ya kijamii na televisheni. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba, tunawanyima Wananchi haki. Haki ni lazima iendane na wajibu, kama unavyoweza kununua gazeti, redio na kama ambavyo unatakiwa ununue kisimbuzi ili uweze kupata habari.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka niseme Serikali haijawanyima watu haki ya kupata habari.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kwanza, siyo kweli kwamba, ndani ya Wizara *either* ya Habari au Mawasiliano, kuna suala la rushwa. Haya ni Maazimio na Tanzania haiwezi kuwa kisiwa katika Dunia ya sasa; ni Azimio kwamba, mpaka kufika mwaka 2015 tubadili twende katika mitambo ya dijiti. Kwa hiyo, Tanzania

haiwezi kuwa kisiwa tukawa tofauti, ndiyo maana nchi hizi zimekubaliana, za Afrika Mashariki tumekubaliana kwamba, mitambo ingezimwa mwaka 2012, *SADC* tungezima mwaka 2013 na Dunia nzima tungezima mwaka 2015. Lazima tujisifie kwamba, Tanzania imekuwa mionganoni mwa nchi za mfano. Zambia wamekuja hapa kujifunza sisi Tanzania tumewezaje; hivyo, ni lazima tujipongeze kwa haya ambayo tumeyapata kama mafanikio.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukiangalia muda ule tumevuka saa tunazostahili kuuliza maswali. Nina tangazo moja tu la kazi.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa 7.15 mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati kwenye Ukumbi wa Msekwa. Hii ni Kamati ya Nishati na Madini katika Ukumbi wa Msekwa.

Pia Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Mheshimiwa Iddi Azzan, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge, matokeo ya mechili zilizochezwa Siku ya Jumamosi, tarehe 15 Juni, 2013 kwenye Uwanja wa Jamhuri. Katika Mpira wa Miguu, Timu ya Bunge ilipata goli moja, *NMB* sifuri. Kwa hiyo, Bunge walishinda kwa goli moja. (*Makofii*)

Kulikuwa pia na Mpira wa Pete, Bunge walipata magoli 38 na *NMB* magoli 17. Nyota wa michezo hiyo ni Mheshimiwa Amos Makala na Mheshimiwa Ester Bulaya. Nawapongezeni sana kwa kucheza vizuri. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba tuendelee.

17 JUNI 2013

## KAULI ZA MAWAZIRI

### Taarifa Kuhusu Mlipuko Uliotokea Jijini Arusha

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa kauli ya awali ya Serikali Bungeni kuhusu mlipuko uliotokea katika Mkutano wa Hadhara wa Kampeni za Uchaguzi katika Kata ya Soweto, Jijini Arusha, tarehe 15 Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha Taarifa ya awali kuhusu tukio la mlipuko uliotokea kwenye Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi wa Chama cha CHADEMA katika Kata ya Soweto, Jijini Arusha, tarehe 15 Juni, 2013, saa 12 jioni.

Mheshimiwa Spika, Tarehe 15 Juni, 2013 ilikuwa siku ya kuhitimisha Kampeni za Uchaguzi wa Madiwani katika Kata 26 katika nchi yetu. Katika Jiji la Arusha kulikuwa na Mikutano mitatu iliyohusisha vyama vitatu vya siasa; CCM, CHADEMA na CUF. Mikutano hiyo ilihudhuriwa na mamia ya Wananchi.

Mheshimiwa Spika, ilikuwa ni katika Mkutano wa Chama cha CHADEMA, uliofanyika katika Kata ya Soweto, ambapo baada ya hotuba za Kampeni kumalizika, Viongozi wa Chama hicho walianzisha harambee ya kuchangia Chama chao. Wakati zoezi hili likiendelea, mtu asiyejulikana alirusha kitu katika kundi la watu, kilichosababisha mlipuko mkubwa na taharuki kubwa mionganoni mwa Wananchi waliosanyika.

Mheshimiwa Spika, Mkutano huu ulikuwa na ulinzi wa Jeshi la Polisi wakiwa na magari mawili na Askari walismama upande wa Kaskazini ya Uwanja na mrushaji wa mlipuko huo alikuwa upande wa Mashariki ya Uwanja huo na akarusha kuelekea Magharibi. Jaribio la Askari wa Polisi kutaka kumfuata aliyerusha mlipuko huo lilizuiliwa na makundi ya Wananchi amba walianza kuwashambulia Polisi kwa mawe na kuwazomea na hivyo Polisi kulazimika kuanza kujiokoa badala ya kumsaka mhalifu huyo.

Mheshimiwa Spika, mlipuko huo ulisababisha watu wawili kufariki Dunia, ambao ni Judith Wiliam, mwenye umri wa miaka 48 na mtoto Ramadhani Juma, mwenye umri wa miaka 15. Watu 70 walijeruhiwa, miongoni mwao watatu walijeruhiwa vibaya na wawili hali zao ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, mara baada ya tukio hilo, Kamanda wa Polisi Mkoa, Mkuu wa Polisi Wilaya na Timu ya Wapelelezi, walifika eneo la tukio kufanya upeletezi wa awali, ikiwa ni pamoja na kukagua eneo la tukio, kufanya mahojiano na baadhi ya mashuhuda, kudhibiti eneo la tukio pamoja na kutoa msaada wa majeruhi na kuwapeleka hospitalini. Katika uchunguzi wa awali umeonesha kuwa, mlipuko huo ulikuwa ni wa bomu la kurusha kwa mkono (*hand grenade*), ambalo lilitrushwa kutoka upande wa Mashariki kuelekea Magharibi kulikokuwa na gari aina ya Fuso lilitokuwa linatumika kuhutubia.

Mheshimiwa Spika, aina ya urushaji wa bomu hilo, hautofautiani na mbinu iliyotumika kwenye shambulio lingine la bomu lilitotokea tarehe 5 Mei, 2013 katika Kanisa Katoliki la Olasiti katika Jiji hilo hilo la Arusha.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi lina wajibu wa Kisheria na Kikatiba wa kulinda watu na mali zao. Wanapokuwepo kwenye mikutano ya hadhara ya kijamii au ya kisiasa, wanakuwa pale ili kuwalinda raia, wanaaga familia zao kuwa wanakwenda kazini kuwalinda raia na mali zao, hivyo ni muhimu raia kujua kuwa Polisi wapo kwa ajili yao. Kwa miaka mingi, raia wamekuwa wakijua wajibu wa Polisi, ndiyo maana wanapotafuta haki, wakiuawa ndugu wa wafiwa wanatoa taarifa Polisi, wakiibiwaa wanatoa taarifa Polisi, wakipigwa wanatoa taarifa Polisi na hata wakitukanwa wanatoa taarifa Polisi, kwa kuwa wanajua Polisi ni chombo chao cha awali katika kutafuta haki.

Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni, zimekuwepo jitihada za makusudi za baadhi ya vyama vya siasa, makundi ya kijamii na watu binafsi, kupandikiza chuki ya raia dhidi ya vijana wetu wa Jeshi la Polisi, kuwafanya raia wawachukie Askari, kuwafanya Raia wasiwaamini Askari, kuwafanya raia wasiwapo ushirikano Askari na hatimaye kuwa na Taifa ambalo halitawaliki.

Mheshimiwa Spika, Askari wetu hawa ni wale ambao wanajitolea usiku na mchana ili Watanzania wenzao wawe salama. Hawa ni Askari ambao wanauwawa kila siku na majambazi wakiwa wanatutetea, hawa ni Askari ambao ni watoto wa Taifa hili, nao ni Watanzania wanaofanya kazi za hatari kwa ajili yetu.

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kutoroka kwa mhalifu aliyelipua bomu siku ile Soweto, ni matokeo ya uchochezi unaofanywa kwa makusudi na baadhi ya Wanasiasa dhidi ya Serikali na Polisi na hivyo kuwafanya Wananchi wajenge chuki dhidi ya Polisi. Kutokana na Wananchi kujazwa sana chuki zinazosemwa kwenye mikutano ya hadhara na maeneo mbalimbali, ndiyo ikatokea siku hiyo badala la kuwapa ushirikiano Polisi waliokuwa pale kuwalinda, wao wenyewe Wananchi walianza kuwashambulia Polisi. Hatimaye badala ya kumsaka mhalifu, wakapoteza lengo kwa pamoja na wakaanza kupambana, huku Wananchi wakiwashambulia Askari na Askari nao wakabaki kujihami. Sote tunajiuliza; kwa nini Wananchi waliwashambulia na kuwazuia Askari wasitimizie wajibu wao, badala ya kuwasaidia ili wamkamate mhalifu? Je, ilitokea kwa bahati mbaya au ilipangwa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tarehe 6 Mei, 2013 Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alipotoa taarifa ya Serikali juu ya shambulio la bomu la Olasiti alisema, nanukuu: "*Siku za hivi karibuni zimekuwepo jitihada kubwa sana za watu wachache wasioitakia mema nchi yetu kutaka kupandikiza chuki za kidini mionganoni mwa Watanzania na kuleta mapigano na mauaji mionganoni mwa Watanzania. Sina shaka kuwa shambulio la Arusha ni sehemu ya mikakati hiyo miovu.*" Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, shambulio la Soweto limehama kutoka kanisani sasa wamehamia kwenye mikutano ya kisiasa. Nia ni ile ile ya kuwafanya Wananchi wachukiane, wapigane na Taifa letu liparanganyike. Baadhi ya Wanasiasa ama kwa bahati mbaya au kwa kujua na kushiriki mpango huo, wamekuwa wakitoa kauli mfululizo za kuendeleza chuki za kijamii wakidhani wanajimarisha kisiasa kumbe wanapanda mbegu ya uharibifu kwa Taifa letu, mbegu itakayozaa chuki, vita na majuto makubwa ikiachwa iendelee. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito na umuhimu wa kuharakisha uchunguzi huu, Jeshi la Polisi limeunda Timu ya Maafisa Upelelezi, itakayoongozwa na Mkuu wa Operesheni wa Jeshi la Polisi, Kamishna Paul Chagonja. Timu hii itashirikiana pia Vikosi vyote vya Ulinzi na Usalama likiwemo Jeshi la Ulinzi la Wananchi (JWTZ).

Mheshimiwa Spika, Serikali imepania kuwasaka na kuwatia mbaroni wahusika wa shambulio hilo la watu waoga na waovu. Kupitia Bunge hili, nataka niwaambie wahalifu hao kuwa, njama zao za kutugawa kwa misingi ya dini, makabila, rangi, rasilimali na itikadi za vyama zitashindwa. Tutapambana nao usiku na mchana, kwa silaha zote tulizonazo mpaka tutakapowashinda na kuwafikisha mbele ya mikono ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, naowaomba Watanzania kote nchini, kuungana na Serikali yao kuwasaka wahalifu hao.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1978, Nduli Idi Amini aliishambulia Kagera, Watanzania wote tuliungana; wengine walikwenda mstari wa mbele, wengine walichanga fedha, wengine walichanga mifugo, wengine walichanga damu, wengine waliomba dua, ilimradi kila Mtanzania alipambana mpaka tukashinda uvamizi ule.

Mheshimiwa Spika, adui wa sasa ni mbaya zaidi maana anataka kutupiganisha wenyewe kwa wenyewe, aivunje vunje nchi yetu kwa kutumia mikono yetu. Alipotangaza vita, Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere wakati ule, nanukuu alisema: “*Nia ya kumpiga tunayo, sababu za kumpiga tunazo na uwezo wa kumpiga tunao*”. Mwisho wa kunukuu.

Leo Watanzania wote, wa dini zote, wa makabila yote, wa vyama vyote vya siasa, turejee maneno ya Mwalimu kwa kauli na vitendo. Tuwakemee na kuwakabili maadui hawa, wawe wa ndani au wa nje na tuape kuilinda na kuitetea nchi yetu. Tuape kuendeleza Upendo, Umoja na Mshikamano wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwapa pole ndugu na jamaa wa marehemu, Mwenyezi Mungu azilaze mahala pema peponirohozao. Tunawaombea majeruhi, Mungu awapenafuu wapone haraka. Nawapa pole sana Wananchi wa Soweto na Arusha na kuwaomba wazikatae *propaganda* zote zenye sura ya uchochezi na uongo, zinazoenezwa kwa makusudi na baadhi ya watu na wanasiwa wenyewe nia mbaya. Kwa nini Arusha? Arusha iliyokuwa na amani, upendo na iliyotulia sasa panakuwa mahali pa hofu na mvurugano mkubwa; kulikoni?

Sote tushirikiane kuikataa hali hiyo isiendelee Arusha na mahali pengine popote nchini mwetu. Tanzania ni yetu sote, ikiharibika sote tumeharibikiwa! Wote tuseme basi inatosha na tushirikiane kupambana na maovu haya.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kutokana na mfululizo wa matukio haya mageni kabisa na makubwa katika nchi yetu, Serikali imetenga shilingi milioni 100 kama zawadi kwa mtu ye yeyote atakayeshirikiana na kutoa taarifa zitakazofanikisha kunaswa kwa mhalifu wa matukio ya aina hii na mtando wake mzima. (*Makofi*)

Narudia tena sehemu hii; kutokana na uzito na uchungu wa matukio haya ambayo ni mageni sana katika nchi yetu, Serikali imetenga shilingi milioni 100 kama zawadi, kwa mtu ye yeyote atakayetoa taarifa zitakazofanikisha kunaswa kwa

mhalifu wa matukio ya aina hii, ikiwa ni pamoja na mitandao yoyote inayohusika na matendo kama haya ya uhalifu hasa haya ya ulipuaji wa mabomu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na nawashukuru kwa kunisikiliza. Leo Mheshimiwa Makamu wa Rais, hivi sasa anaelekea Arusha kwa ajili ya kutoa rambirambi na kukutana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, lakini pia kujionea mwenyewe haya yaliyotokea kwa niaba ya Serikali.

Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, utaratibu unasema nikisimama ninyi mnakuwa mmekaa.

Waheshimiwa Wabunge, saa 7.00 mchana, nitaomba Kamati ya Uongozi pamoja na Wenyeviti wa Kamati mbalimbali, tukutane katika Ukumbi wa Spika.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Spika, natoa mwongozo kwa Kanuni ya 68(7).

**SPIKA:** Unatoa unaomba?

**MHE. MUSSA HAJI KOMBO:** Naomba.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri ametupa maelezo mazuri sana ya matukio yaliyotokea. Mheshimiwa Waziri, amekusudia kututoa wasiwasi nini Serikali inachofanya. Matukio haya sasa yamekuwa mengi; yametokea Unguja mara mbili, yametokea Arusha mara mbili, lakini baada ya maelezo haya, baada ya masomo ya magazeti yanayosomwa, Wananchi wanatiwa fitina kwamba hili linakwenda kwa mambo ya dini na hili linakwenda hivi. Matatizo haya Serikali haitoi tena *statement* kuwaeleza Wananchi tatizo lillilotokea Zanzibar ni nini, tatizo lillilotokea Arusha ni nini, bado tunabaki na chuki sisi kwa sisi.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, baada ya matukio haya atueleze ili Wananchi wapate kuwa na imani na Serikali yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, na mimi naomba mwongozo wako kuhusu mambo mazito kama haya kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu hatuwezi tukaacha mambo kama haya yanatokea halafu Serikali inajificha kwenye Kanuni ya Kauli ya Mawaziri, jambo lisijadiliwe, lakini mambo yanaendelea kutokea.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako kama sisi Wabunge tuko *serious* hapo kutetea nchi yetu. Baba wa Taifa ametuachia nchi hii ikiwa na amani na ninyi Viongozi wazee mlioko humu ndani, mko hapa kwa amani, msitake kutuachia nchi hii sisi tukiwa tunaongozwa kwenye matatizo ...

**SPIKA:** Omnia mwongozo siyo hotuba.

**MHE. FELIX S. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, sasa naomba mwongozo wako; kwa nini Waziri anayehusika na mambo ya Usalama wa Taifa na Waziri wa Mambo ya Ndani wasijiuzulu, kwa sababu mambo haya yanaendelea kila siku? Kauli hizi zimeshatolewa sana; kwa nini hawa Mawaziri wasijiuzulu, wasiache kazi, hawawezi kwa sababu hata kauli wakitoa kesho na kesho kutwa mambo haya yanaendelea. Yametokea Makanisani kila siku, wameunda Kamati, Kamati hazijamaliza kazi mambo yanatokea tena. Kwa nini watu hawa wasiachie madaraka ili waje watu wenye uwezo wajiuuzulu watu hawa?

**SPIKA:** Mwongozo tayari, tumekusikia.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7).

17 JUNI 2013

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo huu kwa sababu ...

**SPIKA:** Anza unataka nini halafu eleza. Mimi sijui hata ni kitu gani.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Naomba mwongozo kwa kanuni hiyo, kwa sababu jambo hili linahatarisha uchumi, linahatarisha biashara na linataharisha uhai wa watu.

Mheshimiwa Spika, kwa kauli ya Waziri ambayo ameitoa hapa, nilikuwa nafikiria kwamba, mambo kama haya yanapotokea tuyatenganishe na siasa kwa kiasi cha kutosha na tuyafanye yawe ya taaluma zaidi ili watu waweze kuwa na imani na haya ambayo yanazungumzwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kauli ya Waziri ya kusema kwamba, kuna kikosi cha uchunguzi ambacho kimeundwa kuchunguza wakati huo huo anasema kwamba, ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Kafulila unataka mwongozo wa kusemajie, mbona unahutubia; mwongozo hautakiwi kuhutubia.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wangu unatokana na jinsi kauli ya Waziri alivyoitoa. Kauli ya Waziri, inaashilia kwamba, anajua sababu za tukio lile, lakini wakati huo huo anasema kinaundwa kikosi cha kuchunguza. Hii ni *contradictionna* ndiyo maana nikasema naomba mwongozo wako ni kwa nini Waziri anatoa kauli ambayo inaonesha ana majibu, lakini wakati huo huo anasema anaunda kikosi cha kuchunguza.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 47, ambapo nahitaji pengine Bunge lako liahirishe shughuli zote tuweze kujadili suala hili. Kwa kuwa nimejaribu kupita kwenye mitandao ya kijamii, inaonekana kuna malumbano kati ya vyama viwili vinatupiana mpira; CCM pamoja na CHADEMA. Hii ni ishara ambayo ...

**SPIKA:** Mwongozo nifanye nini, msituhutubie?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako liruhusu tujadili, ikiwezekana vyama hivi viwili kama itabainika vinahusika, Msajili wa Vyama vya Siasa avifute, kwa sababu Tanzania ni zaidi ya vyama hivi viwili. Naomba tujadili. (*Kicheko/Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. (*Kicheko/Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ambayo mmesema yote inasema: "Spika anaweza kujibu wakati huo huo na anaweza kujibu wakati mwingine. Kwa hiyo, kwanza, ile habari ya nani aliyoisema kwamba tujadili; Waheshimiwa Wabunge, ndiyo maana nimesema Kamati yangu ya Uongozi ikae, ndiyo kwanza tumemsikia aliyoisema huyu Mheshimiwa Waziri wa Nchi. Sasa mtajadili mnakwenda kusema nini si mtakuwa mnajadili tu, iachieni Kamati yangu ya Uongozi ikakae halafu tutawaambia nini tutakachokuwa tumeongea. Tunaendelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba uniruhusu karatasi ya mwisho ilikuwa imechelewa, nifafanue kidogo juu ya zile fedha ambazo Serikali imetenga shilingi milioni 100 kufanikisha vita hii.

Serikali imetenga shilingi milioni 100 kama zawadi kwa ajili ya watu wote watakaowezesha kutoa taarifa za siri na zitakuwa taarifa za siri kabisa kwa Jeshi la Polisi, zitakazowezesha kupatikana kwa wahalifu hawa. Kila mmoja atakayetoa taarifa hiyo kwa Jeshi la Polisi, hata wawe wangapi, lakini kila mmoja atakayetoa taarifa hiyo ya uhakika kwa Jeshi la Polisi, anahakikishiwa usalama wake na kwamba usalama wake utalindwa. Kila mmoja atapewa shilingi milioni kumi mpaka zitakapokamilika hizo shilingi milioni 100 na hata kama taarifa zitaendelea kuwa zaidiya hapo, Serikali ina uwezowa kuendelea kutoa hizo zawadi, lakini kila taarifa moja ya siri mtoaji atapewa shilingi milioni kumi.

17 JUNI 2013

**SPIKA:** Ahsante. Katibu, hatua inayofuata!

## HOJA ZA SERIKALI

**Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti! Huyu atazungumzia hoja zote ya Fedha na ya Mipango, kwa hiyo, atatumia saa nzima.

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuchukua fursa ili kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2013/2014 pamoja na Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2012/2013 na Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti umeliwezesha Bunge kutekeleza ipasavyo wajibu wake wa Kikatiba wa kuishauri na kuisimamia Serikali pamoja na kulijengea Bunge uwezo wa kuchambua Bajeti ya Serikali kwa kujikita zaidi katika kuangalia mwenendo wa ukusanyaji wa mapato na kusimamia matumizi kwa kulinganisha na hali halisi ya ukuaji wa uchumi wa nchi. Aidha, naamini Kamati hii itawasaidia Waheshimiwa Wabunge, kujielekeza zaidi katika kuishauri na kusimamia Serikali katika kuzingatia upatikanaji wa vyanzo vipyta vya mapato na hivyo kuondokana na utaratibu uliozoleka wa kusimamia matumizi ya Serikali bila kujua matumizi hayo kama yanatokana na vyanzo vipi vya mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo, kuwepo kwa Kamati hii kunalenga kusaidia kupanua uwazi na uwajibikaji na kuimarisha uwezo wa kitaalam wa Waheshimiwa Wabunge

katika kujadiliana kuhusu namna bora ya kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Dhana hii ya ushirikishwaji wa Bunge katika uandaaji, usimamizi na kufuatilia utekelezaji wa bajeti ndiyo utaratibu mzuri (*best practice*) unaotumiwa katika nchi nyingi duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati hii ni mpya, napenda nitumie fursa hii kuainisha majukumu yake kwa mujibu wa Kanuni ya 118, Nyongeza ya Nane, Kanuni ya 9 (a) – (i) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013 ili Wananchi waweze kuyafahamu:-

- (i) Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa kila mwaka;
- (ii) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya kila mwaka yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;
- (iii) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
- (iv) Kuchambua na kushauri kuhusu Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni yenye madhumuni ya kuongeza au kupunguza Mapato na Bajeti ya Serikali;
- (v) Kufanya utafiti na uchambuzi kuhusu Sera za Kodi, Sera za Fedha na Sera za Kiuhasibu zinazopendekezwa na Serikali;
- (vi) Kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu vyanzo vya Mapato ya Serikali na mapendekezo ya hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;
- (vii) Kutoa ushauri wa jumla kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge;
- (viii) Kuchambua na kutoa maoni na ushauri kuhusu Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaopendekezwa na Serikali; na

- (ix) Kuchambua hoja zinazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa ajili ya kuishauri Serikali.

**SPIKA:** Jamani, minong'ono imezidi!

**MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Spika, ni matumaini yangu kuwa, Bunge lako Tukufu limefarijika kwa kuanzishwa kwa Kamati hii, kwani imeondoa kilio na manung'uniko ya siku nydingi kwa Bunge hili kuonekena kama mgonga muhuri (*rubber stamp*) hasa pale lilipokuwa likikutana kwa ajili ya kujadili na kupitisha Bajeti ya Serikali. Ni dhahiri kuwa, utaratibu huu mpya wa kupitisha Bajeti ya Serikali kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha, unatoa nafasi kwa Bunge kujadili kwa kina bajeti za kila Wizara na kuweza kufanya mabadiliko kabla ya kufanya uamuzi wa mwisho kwenye Bajeti Kuu na pia bajeti inamaliza kujadiliwa kabla ya kuanza kwa mwaka mpya wa fedha.

Mheshimiwa Spika, manufaa ya utaratibu huu tayari yameanza kuonekana. Mashauriano ya awali kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali yameonesha mafanikio makubwa kwa Serikali kukubaliana na Kamati ya Bajeti kuongeza fedha katika baadhi ya mafungu ambayo yalikuwa na hoja za msingi kama ilivyoelezwa kwenye taarifa yangu ya mrejesho, niliyoitoa Siku ya Alhamisi, tarehe 13 Juni, 2013.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu tayari limeshapokea taarifa kuhusu mwenendo wa uchumi kwa mwaka 2012 na Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2013/2014, ambapo madhumuni makubwa ni kuongeza kasi ya maendeleo ili ifikapo mwaka 2015, nchi iwe imejikwamua kutoka kundi la nchi masikini duniani na kuwa nchi yenye kipato cha kati (*Middle Income Country*) kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Hali ya Uchumi

iliyowasilishwa na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Wasira. Kwa kuzingatia hili, Tanzania haina budi kuhakikisha inajenga uchumi wenyewe misingi imara na uwezo wa ushindani ili jamii iweze kukabiliana na changamoto za maendeleo na kuweza kwenda sambamba na mabadiliko ya utoaji huduma, masoko, biashara na teknolojia katika kanda na ulimwengu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Pato la Taifa ni kigezo muhimu katika kupima uwezo wa nchi kukua kiuchumi. Katika mwaka 2012, Pato halisi la Taifa limeendelea kuimarika na kukua kwa kiwango cha asilimia 6.9 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2011. Kiwango hiki cha ukuaji ni asilimia nukta moja zaidi ya malengo ya mwaka 2012 ambapo uchumi ulikadiriwa kukua kwa asilimia 6.8. Kuimarika kwa Pato hili la Taifa kunachangiwa kwa kiasi kikubwa na kuboreshwa kwa miundombinu ya usafirishaji na mawasiliano ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa uzalishaji viwandani.

Mheshimiwa Spika, sehemu kubwa ya mchango katika Patola Taifa ni kutoka katika Sekta ya Kilimo ambayo imechangia kiasi cha asilimia 24.7, ikilinganishwa na Sekta ya Mawasiliano ambayo ilichangia asilimia 2.3 tu. Hata hivyo, ukuaji wa Sekta ya Kilimo bado upo chini sana. Kwa kuzingatia kwamba sehemu kubwa ya Watanzania wa hali ya chini wanajishughulisha na killimo, sekta hii ni muhimu sana kama tuna nia hasa ya kuboresha maisha ya watu wetu. Hivyo, ni vyema Serikali ikaongeza juhudi katika kuwezesha sekta hii kwa kuitengea walau asilimia kumi ya bajeti yake ili ukuaji wa uchumi unaozungumzwa ulete maana hasa kwa Wananchi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei wa Taifa kwa kipimo cha mwaka unapima kiwango cha badiliko la kasi ya bei za bidhaa na huduma zote zinazotumiwa na kaya binafsi. Katika mwaka 2012, kasi ya upandaji bei za bidhaa na huduma ilifikia wastani wa asilimia 16.0 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 12.7 mwaka 2011. Upandaji huu wa bei umetokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli katika Soko la Dunia na kupanda kwa bei za chakula kulikosababishwa na mahitaji makubwa ya chakula katika baadhi ya nchi jirani. Kamati inatambua juhudi

mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali katika kudhibiti mfumuko wa bei hadi kufikia hali iliyopo sasa, ambapo mfumuko wa bei umepungua kutoka asilimia 18.2 mwezi Mei, 2012 hadi asilimia 8.3 mwezi Mei, 2013. Hatua hii ni kubwa sana kwa kipindi cha mwaka mmoja. Ni vyema Serikali ikaendeleza juhudini za kudhibiti masuala yote yanayosababisha kuongezeka kwa mfumuko wa bei ili kiasi hiki kiweze kuendelea kubaki katika kiwango kilichofikiwa sasa ama chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti bado inasisitiza mtizamo tofauti katika kubadili changamoto kubwa ya kukuza uchumi wetu kwa upande wa Serikali. Pamoja na kuwa uchumi jumla unategemewa kukua na kufikia kiwango cha asilimia saba na zaidi, ukuaji huo haujawanufaisha Wananchi wengi hasa wanaoishi vijijini. Ukuaji wa Uchumi jumla unapaswa kuleta mabadiliko vijijini ili kupunguza umaskini wa kipato unaowaathiri Wananchi wengi. Hatua hii inaweza kufanikiwa kwa kutumia fursa zilizopo kikamilifu kwa kuendeleza sekta zinazogusa Wananchi wengi kama vile shughuli za kilimo, uvuvi, mifugo na uzalishaji viwandani hususan viwanda vinavyotumia malighafi zinazotokana na sekta hizo ili kuongeza thamani (*Value Addition*) ya mazao hayo. Jitihada hizi za kusaidia Wananchi wa kipato cha chini ni budi ziende pamoja na jitihada za kudhibiti mfumuko wa bei ili kutowapunguzia Wananchi uwezo wa kumudu gharama za maisha (*Purchasing Power*).

Mheshimimwa Spika, Kamati imetafakari kwa kina utendaji wa taasisi za kifedha nchini hususan mabenki yetu ya biashara katika kuchangia kukua kwa uchumi. Kulingana na malengo ya Sera ya Fedha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa asilimia 15.3 Machi, 2013 ikilinganishwa na lengo la asilimia 18.0. Ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi ulifikia asilimia 21.1 katika kipindi kilichoishia Machi, 2013 ikilinganishwa na lengo la asilimia 18.2, hii ni sawa na asilimia 20.9 ya Pato la Taifa. Sehemu kubwa ya mikopo kwa sekta binafsi ilielekezwa katika shughuli za biashara ambazo zilipata wastani wa asilimia 21.8 ya mikopo yote, zikifuatiwa na shughuli binafsi (asilimia 19.7), viwanda (asilimia 11.8) na kilimo (asilimia 11.2).

Mheshimiwa Spika, kutokana na takwimu hizi, inaonesha kuwa, mikopo kwa Sekta Binafsi imeongezeka. Hata hivyo, swali la kujiuliza hapa ni mikopo hii imeelekezwa katika maeneo yapi na matokeo yake ni yapi ikilinganishwa na ukuaji wa uchumi wa nchi na kasi ya ongezeko la Pato la Taifa. Benki zetu nyingi zipo katika mfumo wa kibiashara na hivyo inakuwa ni vigumu kukopesha wakulima mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Hili ni eneo linalohitaji kufanyiwa kazi na Serikali kwa haraka. Jawabu sahihi kwa unafuu wa mikopo kwa wakulima ni kuwa na benki ya kilimo yenye mtaji wa kutosha, ambayo itatoa mikopo ya muda mrefu na yenye riba nafuu. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuharakisha uanzishwaji wa Benki ya Kilimo itakayowekewa mtaji wa kutosha. Aidha, Kamati inaendelea kuimbusha Serikali kutekeleza ahadi yake ya kutenga shilingi bilioni 100 kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitano ili kuiwezesha Benki ya Rasilimali (*TIB*) kuongeza mtaji wake iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Sera za Fedha, Toleo la Juni, 2013, katika mwaka 2012, riba za amana na zile za mikopo ziliimarika ukilinganisha na zilivyokuwa mwaka 2011. Viwango vya riba kwa mikopo ya mwaka mmoja viliongezeka kutoka wastani wa asilimia 13.98 mwezi Machi, 2012 hadi asilimia 14.22 mwezi Machi, 2013, wakati riba kwa amana za mwaka mmoja iliongezeka kutoka wastani wa asilimia 11.24 hadi asilimia 11.40. Hivyo, tofauti kati ya riba za amana za mwaka mmoja na riba za mikopo ya mwaka mmoja ilikuwa asilimia 2.82 mwezi Machi, 2013, ikilinganishwa na asilimia 2.74 mwezi Machi, 2012. Pamoja na mabadiliko hayo, viwango hivi vinavyotozwa kwenye mikopo vimeendelea kuwa vya juu, licha ya kuongezeka kwa ushindani kwenye Sekta ya Kibenki. Serikali inahitajika kuongeza kasi ya kufanya maboresho katika Sekta ya Fedha ili kutoa fursa kwa Wananchi kupata mikopo kwa riba nafuu. Kamati inahimiza maboresho ya sheria yafanyike katika Sekta ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Aprili, 2012, thamani ya Shilingi ya Tanzania imeimarika kidogo na kuwa shilingi 1,569.32 kwa Dola kutoka shilingi 1,573.55 kwa Dola mwezi Machi, 2012. Hali hii ilikuwa tofauti na ilivyokuwa kipindi cha mwezi Desemba, 2010 hadi Desemba, 2011 ambapo thamani ya Shilingi ya Tanzania kwa Dola ilishuka kwa asilimia 10.3 kutoka shilingi 1,432.3 kwa Dola hadi shilingi 1,579.5 kwa Dola. Hii ilitokana na kuongezeka kwa uagizaji wa bidhaa hasa mafuta kwa ajili ya mitambo ya kufua umeme wa dharura, tofauti ya mfumuko wa bei kwa nchi tunazofanya nazo biashara.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili Kamati inapendekeza Benki Kuu ifanye tathmini ya athari za matumizi ya sarafu mbili katika uchumi wa nchi. Aidha, iweke mikakati madhubuti ya kuimarisha thamani ya shilingi kwa kuwa ni muhimu katika ufanyaji wa biashara.

Mheshimiwa Spika, kufikia mwezi Machi, 2013, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 10.7 hadi kufikia Dola za Kimarekani milioni 8,406.0, ikilinganishwa na thamani ya mauzo nje kwa kipindi kama hicho mwaka 2012 ya Dola za Kimarekani milioni 7,563.9. Mapato kutokana na mauzo ya bidhaa nje yaliongezeka kwa asilimia 8.7 kufikia Dola za Kimarekani milioni 5,682.9 wakati mapato kutokana na huduma nje yalikuwa Dola za Kimarekani milioni 2,723.1, sawa na ongezeko la asilimia 15.2.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa thamani ya uagizaji wa bidhaa na huduma iliongezeka kwa asilimia 1.8 na hivyo kufikia Dola za Kimarekani milioni 12,909.7 kutoka Dola za Kimarekani milioni 12,686.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Thamani ya uagizaji wa bidhaa iliongezeka kwa asilimia 1.1 kufikia Dola za Kimarekani milioni 10,514.9 katika kipindi hicho. Aidha, thamani ya malipo ya huduma nje ilifikia Dola za Kimarekani milioni 2,394.9 katika mwaka unaoishia Machi, 2013 ikilinganishwa na Dola milioni 2,284.2, hii ni sawa na ongezeko la asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2012. Kutokana na mwenendo huo, nakisi katika urari wa biashara ilipungua kwa asilimia 10.5 na kufikia Dola za Kimarekani milioni 4,011.1 kutoka Dola milioni 4,479.4 katika kipindi kama hicho mwaka

2012. Kamati ina maoni kuwa jitihada zaidi ziongezwe katika uzalishaji wa bidhaa ndani ili kuongeza mauzo nje ya nchi na hivyo kupunguza uingizaji wa bidhaa nchini.

Mheshimiwa Spika, watu ni rasilimali muhimu sana katika maendeleo ya nchi. Rasilimali hii huleta tija endapo tu sehemu kubwa ya watu hao itajishughulisha katika shughuli za kiuchumi, vinginevyo ni mzigo kwa Taifa. Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika kuanzia tarehe 26 Agosti, 2012, idadi ya watu Tanzania imefikia milioni 44.9 na kati ya hao, watu milioni 43.6 wanaishi Tanzania Bara na milioni 1.3 wanaishi Zanzibar. Matokeo hayo pia yanaonesha kwamba, Tanzania ina wanawake wengi zaidi (51%) kuliko wanaume (49%) na kwamba idadi kubwa ya watu hao ipo Mikoa ya Kaskazini mwa Tanzania ikilinganishwa na ile ya Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa idadi ya watu wanaoishi vijiji ni takribani asilimai 70 na shughuli kuu ya kiuchumi ya vijiji ni kilimo (kilimo, ufugaji na uvuvi); na kwa kuwa takwimu zinaonesha kuwa kasi ya ukuaji wa kilimo ni ndogo sana; ni muhimu kwa Serikali kuendelea kuimarisha Sekta ya Kilimo ili kuweza kutumia fursa ya idadi ya watu iliyօ nayo katika kujiimarisha kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) unaotoa mwongozo wa namna vipaumbele vya Taifa vitakavyotekelvezwa ili kufungua fursa za ukuaji uchumi. Mwaka 2012/2013 ni mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango huo katika mfululizo wa miaka mitano iliyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2012/13 ulilenga kutoa kipaumbele kwa Sekta Binafsi (PPP), kushiriki katika utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo. Aidha, msukumo wa utekelezaji uliwekwa kwenye vipaumbele

vifuatavyo; miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu na huduma za utalii na fedha. Katika kupitia utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2012/2013, Kamati imebaini mafanikio kadhaa katika utekelezaji wa Mpango huo. Hata hivyo, zipo changamoto katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati imeona kuwa, bado Serikali imejikita katika kuchukua mambo mengi kuwa vipaumbele na hivyo kushindwa kutekeleza au kuainisha utekelezaji wake ipasavyo. Kamati inashauri kuwa Serikali ichague maeneo machache ya kipaumbele itakayoweza kuyagharamia kuliko kuchukua maeneo mengi na kushindwa kuyatekeleza kikamilifu. Kwa mfano, Kamati inapendekeza kuwepo kwa vipaumbele walau vitatu tu kwa mwaka kama vile kilimo, miundombinu na nishati, tukiimarisha tunaenda katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, msingi wa kuainisha vipaumbele vya Taifa ulilenga katika kufahamu kiasi cha fedha zitakazotumika pamoja na muda wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hali ilivyo sasa ni kwamba, pamoja na Bunge kuidhinisha fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, bado miradi mingi inaanialiwa bila ya kuwa na fedha ya uhakika katika kuigharamia na hivyo kusababisha gharama kubwa (*Cost Overruns*).

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua iliyochukuliwa na Serikali katika kuanzisha mfumo wa uratibu, ufuatiliaji na tathmini ya miradi kwa kuunda kitengo maalum cha kufanya shughuli hiyo chini ya Ofisi ya Rais (*Presidential Delivery Bureau - PDB*). Utaratibu huu ni mzuri kama ukitekelezwa ipasavyo. Aidha, Kamati inashauri kwamba, ili utekelezaji wa mfumo huu mpya ufanikiwe ni lazima watu wabadili mitazamo ya kifakra kwa kuwa tayari kuwajibika na kuwajibishwa pale wanapokosea. Nidhamu ya kuheshimu sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa isimamiwe.


Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya kodi kila mwaka. Inakadiriwa kuwa kati ya mwaka 1999/2000 na mwaka 2012/2013, kiasi cha makusanyo ya kodi kimeongezeka kutoka 15.7% ya *GDP* hadi 16.6% ya *GDP*, ambalo ni ongezeko la asilimia 0.9 katika kipindi cha miaka 12. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 0.075 kwa mwaka. Ongezeko hili linadhahirisha kwamba, bado kuna changamoto kubwa katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kwamba, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2013, makusanyo ya kodi yalikuwa yamefikia kiasi cha shilingi triliuni sita, bilioni mia tatu sabini na moja nukta tatu, sawa na asilimia 96 ya makadirio ya kipindi hicho na asilimia 79 ya lengo la mwaka la shilingi trillioni nane bilioni sabini nukta moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo jitihada za Serikali katika kuongeza makusanyo ya kodi, bado kiwango hiki cha makusanyo siyo cha kujivunia sana. Ikinganishwa na nchi nyingine za jirani zinavyofanya katika eneo hilo, Tanzania ni kati ya nchi ambazo zina utajiri mkubwa wa rasilimali zikijumuisha watu na maliasili. Bado rasilimali hizo hazijaweza kutumika kikamilifu katika kuongeza wigo wa kodi. Ni wakati sasa kwa Serikali kufikiria mbali zaidi katika kukusanya kodi kwa kuibua vyanzo vipyta ya kodi kwa kutumia rasilimali tulizonazo katika kuongeza mapato ya ndani.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2012/2013, Serikali ilitegemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 644.582 kama maduhuli. Mpaka kufikia mwezi Aprili, 2013, makusanyo ya maduhuli yalikuwa yamefikia kiasi cha shilingi bilioni 357.8, sawa na asilimia 55.5 ya lengo la mwaka. Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na baadhi ya Wizara zenye maduhuli mengi kutokusanya kikamilifu. Baadhi ya Wizara hizo ni Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Mashirika yanayosimamiwa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Mchoro 1; Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara na Idara ambazo zipo kwenye mfumo wa kubakiza (*Retention Scheme*) kwa kipindi cha mwezi Julai, 2012 hadi Februari, 2013.



### Chanzo: Wizara ya Fedha, 2013

Mheshimiwa Spika, Tanzania inayo hazina kubwa ya maduhuli kwa sababu ya utajiri mkubwa uliopo wa maliasili. Inakadiriwa kwamba, hazina hii inaweza kufikia kati ya asilimia tatu hadi asilimia tano ya Pato la Taifa (*GDP*). Hata hivyo, mpaka sasa kiwango cha makusanyo ya maduhuli ni asilimia 1.7 tu ya *GDP*. Mwenendo wa makusanyo ya mapato haya unaonesha kwamba, lipo tatizo kubwa katika uwekaji wa malengo ya makusanyo hasa udhaifu katika kusimamia ukusanyaji wake. Udfaifu huu pia upo katika makusanyo ya maduhuli katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba takwimu za makusanyo zinaonesha baadhi ya Wizara na Idara za Serikali zinafanya vizuri katika kukusanya maduhuli, Kamati inaona ipo changamoto kubwa katika kuhakikisha mapato zaidi yanapatikana kutoka eneo hili. Ipo haja ya kuangalia upya

malengo ya makusanyo yanayowekwa pamoja na jitihada inayowekwa katika kuhakikisha malengo hayo yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makusanyo ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa, hadi kufikia mwezi Aprili, 2013, mapato yaliyokusanywa yanafikia shilingi bilioni 177.4, sawa na asilimia 49 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi bilioni 362.2. Kamati imebaini kwamba, ipo changamoto kwa Halmashauri zetu kutumia utaratibu wa kuweka wakala (wakandarasi) katika kukusanya mapato, hali inayosababisha upotevu wa mapato mengi. Hivyo, Kamati ina maoni kuwa Serikali ifikirie kutumia utaratibu wa watendaji kata kuwa ndiyo wakusanyaji kodi na iwave motisha pale wanapovuka malengo ya makusanyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, Kamati inasubiri matokeo ya utafiti wa eneo hili la maduhuli unaofanywa na Wizara ya Fedha kwa madhumuni ya kuboresha makusanyo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, nchi yetu ni miongoni mwa nchi zinazoendelea Duniani. Mbali na mapato ya ndani, Bajeti ya Serikali hutegemea misaada na mikopo kutoka kwa washirika mbalimbali wa maendeleo. Utetegemezi wetu katika Bajeti ya Serikali unaoneshwa katika Jedwali Na 1 katika Taarifa hii.

**Jedwali 1: Misaada na Mikopo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo**

	2010/2011		2011/2012		2012/2013		2013/2014
	Makisio ya Bajeti	F e d h a iliyotolewa	Makisio ya Bajeti	F e d h a iliyotolewa	Makisio ya Bajeti	F e d h a iliyotolewa	Makisio ya Bajeti
<b>GBS</b>	821,645	928,330	869,414	916,381	842,487	645,419	1,163,131
<b>Basket Fund</b>	477,788	522,560	688,000	471,916	415,136	434,300	500,422
<b>Project Funds</b>	1,975,120	1,557,829	2,366,137	1,424,994	1,899,095	1,166,341	2,191,647
<b>ODA</b>	3,274,553	3,008,720	3,923,551	2,813,290	3,156,718	2,246,059	3,855,199

Chanzo: Wizara ya Fedha, 2013

Mheshimiwa Spika, kama ilivyoainishwa katika jedwali hapo juu, wafadhili wamejitahidi kutekeleza ahadi zao na hata kuvuka malengo. Hata hivyo, kwa upande wa fedha za miradi, mwenendo wa utoaji wa fedha hizo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka kutohana na Serikali yetu kutotimiza mchango wake katika miradi hiyo.


Mheshimiwa Spika, Kamati inaungana na Serikali, kuwashukuru Washirika wetu wa Maendeleo katika kuchangia sehemu ya bajeti yetu. Hata hivyo, ili kuwafanya washiriki wetu waweze kukamilisha ahadi zao hasa katika Miradi ya Maendeleo, Serikali itenye mapema iwezekanavyo kiwango kinachotakiwa kama sehemu ya mchango wetu katika miradi hiyo. Kamati inashauri juhudzi ziongezwe kupunguza utegemezi wa kibajeti. Aidha, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali ijithahidi kukusanya zaidi mapato yake ya ndani ili kuweza kugharamia matumizi yake ya kawaida na ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatambua jitihada za Serikali katika kutafuta fedha maeneo mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza miradi ya maendeleo pamoja na kulipia madeni. Pamoja na ukweli kwamba, mikopo ya masharti ya kibiashara ina riba kubwa ikilinganishwa na ile isiyo ya kibiashara, mikopo hii ndiyo iliyo na uhakika na uharaka katika upatikanaji wake. Katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Aprili, 2013 Serikali ilikopa shilingi trillioni 1,364.7 kutoka soko la ndani la mitaji pamoja shilingi bilioni 809.1 kwa ajili ya kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inasisitiza kwamba, misaada na mikopo yote (yaani mikopo nafuu na mikopo yenye masharti ya kibiashara), ielekezwe katika Miradi ya Maendeleo ili iweze kuleta tija badala ya fedha hizo kutumika kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, Jedwali lifuatalo linaeleza kwa ujumla mchango wa vyanzo mbalimbali vyatapato kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013.

Mchoro 2: Vyanzo vya Mapato 2012/2013



Mheshimiwa Spika, matumizi ya Serikali kwa ujumla bado ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti. Kamati imebaini kuwa, matumizi ya Serikali ni makubwa kuliko mapato yake. Hali hii imesababisha Serikali kuendelea kutumia utaratibu wake wa kukopa nje au ndani ili kufidia pengo la upungufu wa fedha. Kamati imebaini kuwa, kuongezeka kwa matumizi ambako hakuendisambamba na kuongeza juhudiza ukusanyaji wa mapato, kutaendelea kuwa mzigo kwa nchi kutohana na kwamba, nchi itakuwa ikiendelea kukopa na hivyo kuendelea kuongeza kiasi cha matumizi. Takwimu za miaka miwili hapa chini zinaelezea hali hiyo:

Jedwali 2: Mapato na Matumizi ya Serikali

MWAKA	MAPATO YA NDANI	MATUMIZI	TOFAUTI
2011/2012	7.3 Trillioni	8.6 Trillioni	1.3 Trillioni
2012/2013	9.1 Trillioni	10.6 Trillioni	1.5 Trillioni

Mheshimiwa Spika, sambamba na matumizi yanayooneshwa na Serikali kuitia vitabu vyake via bajeti, Kamati imebaini kuwa, zipo Wizara ambazo zimekuwa zikitumia fedha zaidi ya zile zilizoidhinishwa na Bunge; mfano, katika mwaka 2011/2012 Wizara zifuatazo ziliidhinishiwa fedha katika mtiririko unaooneshwa katika Jedwali Na 3. Lakini katika hali ya kushangaza, fedha iliyotumika ilizidi ile iliyoidhinishwa na Bunge.

Jedwali 3: Ulinganisho wa Fedha zilizoidhinishwa na zile zilizotumika kwa baadhi ya Mafungu

<b>WIZARA</b>	<b>F E D H A ILIOIDHINISHWA - 2011/2012</b>	<b>F E D H A ILIYOTUMIKA - 2011/2012</b>	<b>ONGEZeko</b>
Ugharamiaji wa Deni la Taifa na Deni lenyewe	trillioni 1.901	trillioni 2.525	Billioni 624
Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa	bilioni 80.602	b i l l i o n i 112.080	B i l l i o n i 31.478
Wizara ya Afya	bilioni 219.367	b i l l i o n i 246.719	B i l l i o n i 27.352
Wizara ya Nishati na Madini	bilioni 76.9953	b i l l i o n i 148.429	B i l l i o n i 71.4337

Chanzo: Wizara ya Fedha

Mheshimiwa Spika, huu ni mfano tu kwa baadhi ya Wizara. Msingi wa kuainisha matumizi hayo umelenga katika kutafuta ufumbuzi juu wa Maafisa Masuuli kutumia zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa moja ya majukumu ya Kamati ya Bajeti ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali, Kamati inaitaka Serikali kabla ya kuhaulisha (*reallocation*) fedha kutoka fungu moja kwenda lingine, angalau iwasiliane na Kamati ya Bajeti katika msingi ule wa mashauriano baina ya Bunge na Serikali ili kuhakikisha nidhamu ya bajeti inafuatwa.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, jumla ya shilingi triliioni 1.901 zilitengwa kwa ajili ya kugharamia Deni la Taifa. Hata hivyo, kiasi cha shilingi triliioni 2.525 zilitumika katika mwaka huo kugharamia Deni la Taifa. Ugharamiaji wa deni hilo katika mwaka huo ni sawa na ongezeko la shilingi bilioni 624, ambalo halikuwa kwenye bajeti. Serikali iharakishe mpango wake wa kuanzisha Idara ya Usimamizi wa Deni la Taifa. Hatua hii itazuia kuhamishwa kwa fedha kutoka kwenye mafungu mengine ili kulipia Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti haioni tatizo kwa Tanzania kuendelea kukopa kwani bado deni lake ni himilivu. Kamatiyanguinaaminikuwa, uwezowakukopazaidiupona hasa kama mkopo huo utaelekezwa katika maeneo yenye matokeo ya haraka. Aidha, ni vyema mikopo hii ikalenga kuanzisha ama kukamilisha miradi ya kimkakati ili iweze kuwa na tija kama vile reli ya kati, bandari zetu na maeneo mengine muhimu. Ni vyema mikopo hii ikatoka katika vyanzo vinavyoaminika na kwamba ifike kwa wakati kwa ajili ya matumizi.

Mheshimiwa Spika, mnyongemnyongeni, hakiyake mpeni. Kamati ya Bajeti imeridhishwa kuona sasa Serikali imeanza kupunguza bajeti yake katika baadhi ya maeneo ambayo yamekuwa kero kubwa mwaka hadi mwaka. Mwelekeo wa matumizi kwa mwaka 2013/2014 unaonesha kwamba, Serikali imeanza kupunguza bajeti yake ya viburudisho (*Hospitality*) kwa takribani asilimia 52, wakati ile ya gharama zingine za uendeshaji (*other operating expenses*) imepungua kidogo kwa takribani asilimia mbili.

Jedwali 4: Ulinganisho wa Bajeti ya Kasma kadhaa kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 na 2013/2014

KASMA	MALELEZO	2012/2013 JUMLA	2013/2014 JUMLA	ASILIMIA YA ONGEZeko/ PUNGUZO
220300	Mafuta na Vilainisho	74,191,213,802	88,696,009,177	19.5
221000	Kusafiri ndani ya Nchi	104,938,705,157	123,858,000,000	18
221100	Kusafiri nje ya nchi	39,309,892,369	51,398,272,804	30.7
221400	Hospitality	53,947,901,359	25,831,899,570	(52)
229900	Gharama nyingine za uendeshaji <i>(Other Operating expenses)</i>	450,001,310,119	441,279,000,000	(1.9)
230400	Matengenezo ya Magari <i>(Routine Mantanance and Repair of Vehicles)</i>	20,019,858,987	15,625,000,000	(21.9)
410200	Ununuzi wa Magari <i>(Acquisition ov Vehicles)</i>	21,079,586,700	12,360,079,00	(41.4)
JUMLA		763,488,468,493	899,677,000,000	

Chanzo: Wizara ya Fedha - Volume II

Mheshimiwa Spika, bajeti ya ununuzi wa magari pia inaelekea kupungua kwa takribani asilimia 41 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2012/2013. Aidha, fedha zilizotengwa kwa ajili ya kufanya matengenezo (*repair*) ya magari haya pia imepungua ikilinganishwa na mwaka 2012/2013 kwa takribani asilimia 22. Hata hivyo, bado lipo tatizo kubwa katika matumizi ya mafuta na vilainishi Serikalini. Tathmini inaonesha kwamba, Serikali inategemea kutumia fedha nyingi zaidi kwa ajili ya mafuta katika mwaka ujao ikilinganishwa na mwaka huu wa fedha. Ongezeko hilo litafikia asilimia 19.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo yanaonesha kuongezeka ni pamoja na safari za ndani na nje ya nchi, ambapo kwa upande wa safari za nje, mwelekeo unaonesha kwamba, kuna ongezeko la takribani asilimia 12 wakati kwa safari za ndani ongezeko ni takribani asilimia 18.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla mwelekeo wa matumizi ya Serikali bado hauridhishi. Kamati imepokea kwa matumaini maneno ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itadhibiti matumizi yake kwa kiasi kikubwa.

Kwa kuwa moja ya jukumu la Kamati ya Bajeti ni kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa niaba ya Bunge, naomba kulihakikishia Bunge lako kwamba, Kamati itafuatilia kwa karibu ahadi hii ya Serikali kuhakikisha kwamba inatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la malimbikizo ya madeni katika Wizara na Idara za Serikali. Katika hali ya kawaida, inatazamiwa kwamba, Wizara na Idara za Serikali zitatumia fedha kulingana na bajeti iliyopangwa. Hata hivyo, hali hii imekuwa haitekelezeki kwa sababu mbalimbali zikiwemo ucheleweshwaji wa fedha za bajeti. Endapo Wizara na Idara zitaendelea kutumia huduma, ama kulazimika kufanya hivyo, hutengeneza deni ambalo kama fedha za mwaka husika zisipotolewa, deni hilo huathiri bajeti ya mwaka unaofuata.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine ni kwamba, bajeti zetu mwaka hadi mwaka zimekuwa zikitumika kwa kiasi kikubwa kulipa madeni badala ya kutekeleza mipango iliyopangwa katika mwaka husika. Matokeo yake ni kutokamilika kwa wakati kwa miradi mingi, lakini pia kuiongezea Serikali gharama pale ambapo miradi iliyopangwa kutekelezwa huchelewa kukamilika au kutokamilika kabisa.

Mheshimiwa Spika, ipo haja kwa Serikali kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha kwamba, madeni haya yanadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, moja ya malengo makubwa na ya muhimu ya kuwepo kwa Sheria ya Ununuzi wa Umma ni kuweka uwazi katika suala zima la manunuzi. Lengo hili ni jema na la msingi. Hata hivyo, katika utekelezaji wa Sheria hii, Kamati yangu imebaini ukweli ambao upo dhahiri kabisa kwamba, utaratibu mzima wa manunuzi huchangia sana katika kuongeza gharama kwa Serikali. Bei zinazotumika kuuza huduma na vitu mbalimbali kwa Serikali hufikia karibu maradufu ya bei ya soko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, takribani asilimia 70 ya bajeti yote tunayopitisha hapa Bungeni inatumika katika manunuzi. Katika utaratibu nilioutaja awali, kiasi kikubwa cha fedha hiyo hutumika bila tija kwa sababu hununulia vitu kwa bei ya juu sana. Hivyo, manunuzi ni sehemu ambapo Serikali inapoteza fedha nyingi sana za Wananchi; ni muhimu hatua za haraka zikachukuliwa katikakurekebisha halihii. Kamati iinaungamkono azmaya Serikali ya kutengeneza jedwali la bei elekezi kwa baadhi ya bidhaa zinazotumika kwa wingi Serikalin. Kamati inasisitiza kwamba, utengenezaji wa Jedwali hilo ufanyike haraka iwezekanavyo ili uanze kutumika katika bajeti ya mwaka 2013/2014. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Serikali imechukua hatua mbalimbali kwa madhumuni ya kujiongezea mapato ya kodi. Hatua hizo ni pamoja na kupunguza misamaha ya kodi katika baadhi ya maeneo, kuongeza viwango vya kodi kwa maeneo kadhaa, lakini pia kuanzisha kodi na tozo mbalimbali. Hatua hizi zinalenga kuipatia Serikali kiasi cha shilingi trilioni 10.412 kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, sawa na ongezeko la asilimia 29 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa makusanyo ya kodi kwa mwaka 2012/2013 unaashiria kwamba, *TRA* hawataweza kufikia malengo waliyojiwekea ya kukusanya asilimia 27 zaidi ya makusanyo ya mwaka uliotangulia. Inakadirwa kwamba, upungufu wa makusanyo hayo utafikia asilimia nne. Katika hali hii, Kamati ina wasiwasi kama malengo ya mwaka 2013/2014 yatafikiwa kutokana na changamoto mbalimbali za ukusanyaji wa mapato ya kodi. Changamoto hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutowiana kwa mwenendo wa ongezeko la malengo ya makusanyo ya kodi na ukuaji wa Pato la Taifa. Mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 ukuaji wa Pato la Taifa ni asilimia 6.9, ambao umeonekana kuwa ni mdogo ukilinganishwa na kiwango cha malengo ya makusanyo ya kodi yanayotegemewa.

(ii) Malengo haya yatasababisha ongezeko la gharama za ukusanyaji wa kodi usio na uwiano na makusanyo halisi.

(iii) Kuwepo kwa changamoto na matatizo ndani ya *TRA* mfano kukadiria chini ya viwango (*Under Declaration*), kukadiria chini ya thamani (*Under Valuation*), kupandishwa viwango vya thamani (*uplifting*) rushwanakadhalika, kunasababisha kiwango cha makusanyo kuwa hafifu. Kamati ina maoni kwamba, ni vyema *TRA* ikaboreshwala ili iweze kukusanya mapato ya kodi ya ndani kwa kiwango cha kuridhisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mapato yasiyo ya kodi: Kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, makadirio ya makusanyo ya maduhuli ni kidogo (asilimia kumi ya mapato yote ya ndani), ikilinganishwa na makadirio ya mwaka 2012/2013, pamoja na vyanzo vilivypo. Aidha, Bajeti ya mwaka 2013/2014 inaonesha kiwango kipyta kitokanacho na asilimia kumi ya mapato ghafi ya Taasisi za Serikali. Hivyo, kuwepo kwa kiwango hicho kipyta kungetegemewa kuongeza kiwango cha maduhuli katika bajeti ya 2013/2014, lakini hali imekuwa tofauti. Ingawa kuna vyanzo vingine vya mapato yasiyo ya kodi ambayo ni pamoja na shughuli za utalii, misitu, uvuvi, ardhi, viza, Kamati ina maoni kuwa, vyanzo hivi vikisimamiwa kikamilifu vinaweza kuongeza kiasi cha ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali inategemea kupata misaada na mikopo ya kibajeti yenye masharti nafuu kiasi cha shilingi trilioni 3,855.2. Kati ya fedha hizo, misaada na mikopo ya kibajeti ni shilingi trilioni 1,163.1 na misaada na mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ni shilingi (*Makof*) 2,191.6 na Mifuko ya Kisikta ni shilingi bilioni 500. Kiwango hiki cha mikopo na misaada kimepungua kufikia

asilimia 21 kutoka asilimia 30 ya mwaka 2012/2013. Hii ni hatua nzuri kwa nchi, iwapo changamoto zinazoikabili *TRA* katika ukusanyaji wa mapato zitapatiwa ufumbuzi na majawabu sahihi na iwapo vyanzo vya ndani vitawezeku kukusanya mapato ipasavyo. Aidha, Serikali iendelee kupunguza matumizi mengineyo (*OC*) yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Mikopo ya Ndani na Nje: Katika Mwaka wa Fedha wa 2013/2014, Serikali inatarajia kukopa shilingi (*Makofi*) 1,699.8. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 552, sawa na asilimia moja ya Pato la Taifa ni kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo. Aidha, kiasi kinachobaki cha shilingi bilioni 1,147.6 ni kwa ajili ya kulipia hatifungani na dhamana za Serikali za muda mfupi. Kiasi hicho cha fedha kinachokopwa kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo ni kidogo kutokana na ukomo uliowekwa wa kutokopa zaidi ya asilimia moja ya Pato la Taifa. Kamati inashauri kwamba, Serikali ijadiliane na Taasisi za Kifedha za Kimataifa ili ziweze kuongeza kiwango cha kukopa zaidi ya hiyo asilimia moja. Aidha, Serikali iharakishe zoezi la nchi kufanyiwa tathmini (*Sovereign Rating*), ambalo litawezesha nchi kukopa katika Masoko ya Kimataifa hivyo kuharakisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kupitia mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Serikali imepanga kutumia shilingi trilioni kumi na mbili, bilioni mia tano sabini na nne nukta tisa tano, ambayo ni sawa na asilimi 69 ya Bajeti, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni tano bilioni mia sita na sabini na nne nukta sifuri tatu, sawa na asilimia 31 ya Bajeti kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo. Katika sura hii, Kamati ina maoni kwamba, bado matumizi ya kawaida ni makubwa kuliko yale ya miradi ya maendeleo. Narudia; katika sura hii, Kamati ina maoni kwamba, bado matumizi ya kawaida ni makubwa kuliko yale ya miradi ya maendeleo. Hivyo, Kamati inashauri kwamba, Serikali iongeze ukusanyaji wa mapato ili tuweze kugharimia Miradi ya Maendeleo katika kiwango cha asilimia 35 ya Bajeti ya Serikali kama Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo unavyoelekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati kuhusu baadhi ya Hatua za Kodi zinazopendekezwa na Serikali; mapendekezo ya mabadiliko ya kodi na tozo mbalimbali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha, yatakuwa ni sehemu ya pili ya mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Serikali ambayo yatafanyika wakati wa kujadili Muswada wa Fedha (*Finance Bill*) ya mwaka ujao wa fedha. Hivyo, Kamati itatoa maoni kuhusu eneo hili wakati wa kuwasilisha taarifa yake kuhusu Muswada huu. Aidha, Kamati inatoa maoni katika baadhi ya maeneo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inapendekeza kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato kutoka asilimia 14 hadi asilimia 13, hii ni sawa na punguzo la asilimia moja. Kamati ina maoni kuwa, kiwango hiki ni sawa na ongezeko la shilingi 1,900 kwa mwezi, ambazo ni sawa na shilingi 22,800 kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ni kweli lazima ushukuru hata kwa kidogo, lakini ongezeko hili ni dogo ikilinganishwa na hali halisi ya uwezo wa mfanyakazi kununua bidhaa na huduma mbalimbali na kuendesha maisha yake. Ni maoni ya Kamati kwamba, punguzo lingeongezeka mpaka angalau asilimia tatu ili kuongeza uwezo wa kumudu gharama za manunuzi (*purchasing power*) kwa wafanyakazi. Hatua hii itachochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220 na Sheria ya Petroli, Sura 392: Serikali inapendekeza kurekebisha viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli kama ifuatavyo:-

(i) Mafuta ya Dizeli kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 215 kwa lita hadi shilingi 217 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi mbili.

(ii) Mafuta ya Petroli kutoka kiwango cha sasa cha shilingi 339 kwa lita hadi shilingi 400 kwa lita ikiwa ni ongezeko la shilingi 61.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili Kamati inashauri kuwa, ongezeko lifutwe. Hivyo, Kamati itashauriana na Serikali kuhusu vyanzo vingine vya mapato ili kufidia pengo hilo. (*Makof*)

(iii) Sheria ya Ushuru wa Mafuta, Sura 220 inapendekeza kuongeza kiwango cha ushuru wa mafuta (*Fuel Levy*) kutoka shilingi 200 kwa lita hadi shilingi 263 kwa lita, sawa na ongezeko la shilingi 63 kwa lita.

(iv) Pia, Sheria ya Petroli, Sura 392 inapendekeza kuanzisha tozo ya mafuta ya petroli (*Petroleum Levy*) ya shilingi 50 kwa lita ambayo itakusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*). Mapato hayo yatatumika kugharamia mahitaji ya umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, katika maeneo haya mawili na kwa kuzingatia kwamba mara ya mwisho Bunge lako Tukufu liliidhinisha viwango vya shilingi 200 kwa lita mwaka 2007 kwa ajili ya matengenezo ya barabara, na kwa kuzingatia umuhimu wa kuendelea na matengenezo ya barabara zetu nchini na pia kusambaza umeme vijijini, Kamati inakubaliana na ongezeko la shilingi 63 kwa ajili ya Mfuko wa Barabara na ongezeko la shilingi 50 kwa ajili ya kusambaza umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 – Ushuru kwenye simu; Serikali inapendekeza kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 14.5 kwenye huduma zote (*all mobile phone services*) za simu za kiganjani au mkononi badala ya muda wa maongezi peke yake kama ilivyo sasa. Katika ushuru huu, asilimia 2.5 zinapendekezwa kugharamia elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wigo wa kukokotoa ushuru umepanuka kwa kujumuisha huduma zote za simu za mikononi (*data, internet, sms* na kadhalika na simu za mezani), mapato yataongezeka kwa hatua hii. Hivyo, ili kuhamasisha utumiaji wa simu na kupunguza gharama kwa mtumiaji ni vyema asilimia 2.5 isiongezwe ili kiwango kinachotumika sasa cha asilimia 12

kibaki vilevile. Aidha, ushuru wa asilimia 2.5 unaopendekezwa kwa ajili ya kugharamia elimu, utafutwe kutoka kwenye maeneo mengine kama ilivyopendekezwa kwenye Ripoti ya Mheshimiwa Chenge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa teknolojia ya simu inahama kutoka *3G* (*Third Generation*) kwenda *4G* (*Forth Generation*) ambapo nchi nyingi duniani huuza leseni zake kwa mnada kiasi cha kwamba, kiwango cha chini cha leseni moja huuzwa kwa dola milioni 50 wakati hapa nchini ni dola milioni tatu tu. Kamati inashauri kuwa, Serikali ifikirie kutumia utaratibu wa mnada ambao hutoa ushindani wa kibiashara na kuongeza mapato ya nchi. Aidha, Kamati inaanini kuwa eneo hili ni muhimu (*potential*) na litazidi kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua umuhimu wa upatikanaji wa umeme nchini, huduma inayotolewa na Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). Kwa muda mrefu sasa Shirika hili limekuwa likitumia fedha nyingi kwenye ununuzi wa mafuta kwa ajili ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme. Kamati imebaini kuwa, Serikali imekuwa ikitenga fedha kidogo kwa ajili ya kuendesha Shirika hili, hali inayosababisha kufanyika kwa uhamisho wa fedha kutoka kwenye maeneo mengine kwa ajili ya kupeleka *TANESCO*. Mfano, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Serikali ikitenga jumla ya shilingi bilioni 47.96 fedha za ndani na shilingi billioni 2.43 fedha za nje kwa ajili ya kununulia mafuta mazito. Fedha hizo ni kidogo ikilinganishwa na mahitaji ya shilingi trillioni 2.2 iwapo mitambo yote itawashwa na kutumika kwa uwezo wake wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati yangu kutoa taarifa ya mrejesho Bungeni kuhusu matumizi halisi ya *TANESCO*, ililazimu Kamati kukutana tena na Wizara ya Nishati na Madini. Wizara ya Fedha pamoja na Uongozi wa *TANESCO* ili kupata taarifa kuhusiana na gharama halisi za uzalishaji wa umeme kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 kwa kuwa mwaka huo Shirika limetengewa shilingi bilioni 273 tu. Katika kikao hicho ilibainishwa kwamba, kwa mwaka 2013/2014, *TANESCO* itaendesha mitambo yake kwa asilimia 78 na kwa mpango huo *TANESCO* itatumia shilingi trillioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa fedha hiyo ipatikane bila kuathiri Bajeti ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, narudia; Kamati inashauri kuwa fedha hiyo, yaani shilingi trillioni 1.2 ipatikane bila kuathiri Bajeti ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kueleza hapo awali kuwa, Bajeti ya Serikali ni Sheria; hivyo, utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kama ilivyopitishwa na Bunge ni moja ya njia ya kusimamia sheria. Bunge letu hupitisha bajeti ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo. Kwa upande wa matumizi ya maendeleo, fedha hizi huelekezwa kwenye kutekeleza miradi ya maendeleo. Utekelezaji wa miradi hii unategemea jinsi ambavyo Serikali imejipanga katika kusimamia vipaumbele iliyojiwekea kwa kuzingatia bajeti iliyotengwa katika miradi husika. Pamoja na kuwepo kwa changamoto za kibajeti; mfano, kutotolewa kwa fedha hizo kwa wakati au fedha husika kutokutolewa kabisa. Pia licha ya kuwepo na usimamiaji dhaifu wa miradi, bado kama nchi tumekuwa na tatizo la kusimamia uwajibishaji kwa wale wanaoshindwa kusimamia miradi ipasavyo. Hivyo, Kamati inaona kuwa ni vyema Serikali ikaenda mbele zaidi katika kuhakikisha kuwa, vipaumbele vya kiuchumi vinatekelezwa sambamba na kuzingatia masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kuainisha na kueleza hapo awali, Serikali inalo jukumu la kusimamia utekelezaji wa bajeti yake kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Katika kutekeleza jukumu hilo ni muhimu kwa Serikali kuonesha nidhamu ya hali ya juu kwenye matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi yasiyokuwa ya lazima ambayo Bunge lako Tukufu limekuwa likilalamikia siku hadi siku, Kamati inaona kwamba, Serikali iimarishe kaguzi zake za ndani katika kila Wizara, Idara na Taasisi ili kujiridhisha na mahitaji halisi katika maeneo hayo. Hatua hii itasaidia kupunguza au kuondoa kabisa tatizo kwa Wizara na Idara kuwa zinategemea fedha kila mwaka kwa ajili ya kufanya manunuzi, ukodishaji, ukarabati wa aina moja kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, suala la Serikali kubana matumizi katika bajeti yake halihitaji kuundwa kwa Tume kwa kuwa Bunge lako Tukufu limekuwa likishaurijuu ya jambo hili kwa muda mrefusana. Pamoja na Serikali kuonesha nia yake ya kutaka kutekeleza azma hii, Kamati haijaridhishwa na juhudzi zinazochukuliwa na Serikali juu ya jambo hili. Hivyo, Kamati inajiliza ni lini Serikali itatamka rasmi kuwa itaachana na matumizi ya magari ya kifahari ambayo yanaligharimu Taifa hili kiasi kikubwa cha fedha?

Mheshimiwa Spika, katika hili Kamati inaitaka Serikali ije na mpango mahususi utakaoainisha njia mbadala ambayo itatumwa na Serikali katika kutekeleza ushauri huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Serikali kwenye Wizara mbalimbali, Kamati imebaini kuwepo kwa malalamiko mengi kuitia Wizara hizo kuwa ukomo (*ceiling*) wa bajeti unaowekwa katika Wizara umekuwa hauendani na mahitaji halisi ya Wizara hizo hasa ikizingatiwa kuwa, baadhi ya Wizara wamekuwa katika ukomo unaowekwa katika muda wa miaka mitatu hadi minne wakati mahitaji halisi ya Wizara yamekuwa yakipanda. Kamati inajiliza je, ni vigezo gani vinatumika nje ya vile vinavyoelekezwa na Hazina kuzipa Wizara ukomo (*ceiling*) inayoendana na mahitaji yao halisi? Kamati inatambua upungufu wa rasilimali fedha uliopo lakini ina maoni kuwa, suala la kuweka ukomo wa bajeti liangaliwe kwa makini ili kuziwezesha Wizara kupata fedha kulingana na mahitaji yao halisi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuongeza wigo wa ulipaji kodi, Kamati ya Bajeti inaamini yapo maeneo mengine ambayo Serikali ikifanya maamuzi ya makusudi, yanaweza kuiingizia Serikali kiasi kikubwa cha mapato kama kodi na ushuru mbalimbali. Kamati ya Bajeti inaunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Mheshimiwa Chenge, uliyoiunda kuandaa mapendekezo ya maeneo ambayo bado Serikali haijayatumia kikamilifu katika makusanyo ya kodi. Hivyo, Kamati

ya Bajeti inashauri mapendekezo hayo yafanyiwe kazi mara moja. Maeneo hayo ni eneo la uvuvi katika Bahari Kuu, simu za mikononi pamoja na maboresho katika makusanyo ya kodi mbalimbali hususan kodi ya majengo, ardhi na pango.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa kila Shirika ama Taasisi za Umma zinazowajibika kisheria kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa Sheria kufanya hivyo. Serikali ifuatilie kwa karibu uchangiaji huu na hatua stahiki zichukuliwe kwa wale wanaokaidi kutekeleza takwa hili la kisheria.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa Serikali za Mitaa zina mapato mengi ambayo yakikusanywa ipasavyo yatasaidia katika kupunguza utegemezi wa bajeti. Kwa kutambua hilo, Kamati ina maoni kuwa maeneo muhimu kama vile kwenye majengo, Serikali inapoteza kiasi kikubwa cha fedha kutokana na majengo mengi kutolipiwa ushuru vile inavyostahili. Kamati inashauri kuwa, Serikali iharakishe mchakato wa uandikishaji wa anuani za makazi ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato kupitia kodi za majengo. Aidha, katika kutekeleza azma hii, Kamati ina maoni kuwa Serikali inaweza kuanza kutambua wamiliki wa majengo kupitia *TANESCO*. Chini ya utaratibu huu, walipaji wa umeme wanaweza kuwa wanalipa kodi ya majengo moja kwa moja, hali ambayo inaonesha kurahisisha upatikanaji wa kodi wakati tukisubiri utaratibu wa uandikishaji wa anwani za makazi kukamilika kwani linaonesha kutumia muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika, wadau wa maendeleo wamekuwa msaada mkubwa katika kuchangia Bajeti Kuu ya Serikali. Serikali kupitia wadau hao, imekuwa ikipokea misaada na mikopo yenyé masharti nafuu kwa njia ya Mfuko wa Pamoja (*GBS*), lakini pia kwa njia ya kusaidia Miradi (*Project Support*). Uchangiaji huu kwenye Bajeti ya Serikali umekuwa wa kuridhisha pamoja na kwamba, Serikali bado inahitaji kufanya kazi baadhi ya maeneo kama vile fedha zinazopelekwa moja kwa moja kwenye baadhi ya Miradi bila kupita Hazina, zinashindwa kutoa picha ya halisi ya kiasi cha fedha kinachokuwa kimepokelewa kutoka kwa wafadhili katika mwaka husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa wadau hao na kazi nzuri wanayofanya, Kamati inashauri kwamba, Serikali isiishie hapo; zipo fursa nyingine za ushirika wa maendeleo ambazo bado hazijatumika kikamilifu. Ni wakati sasa kwa Serikali kuondokana na tegemezi washirika wale wale tu na badala yake iangalie fursa zilizopo za kushirikiana kimaendelea na washirika wengine wasiofungamana na upande wowote; mfano, washirika katika nchi za Asia.

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inasisitiza kuwa, dhana ya kuwa Serikali itafanya kila kitu katika ukuaji wa uchumi siyo sahihi. Ni vyema kila Mtanzania akajitambua na kujua ana jukumu gani katika kusaidia Serikali na kutimiza wajibu wake ipasavyo. Uchumi wa nchi, huanzia kwa mtu mmoja mmoja; hivyo, mitizamo ya kitabia lazima ibadilike ili tuweze kusaidia kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Miradi ya Ubia (*PPP*); bado utekelezaji wa Sera na Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi haujawa wa kuridhisha kama ilivyodhaniwa ili iweze kutusaidia kupiga hatua kubwa kwenye maendeleo hasa kwa upande wa miundombinu na ujenzi. Miradi mingi bado ipo kwenye awamu, kufanyiwa uchambuzi zaidi ili kutekelezwa kwa utaratibu wa ubia. Hata hivyo, mapendekezo ya miradi iliyopokelewa na Serikali bado hayajakidhivigezo vinavyohitajika kutekelezwa kwa kuzingatia utaratibu na muundo wa *PPP*. Takwimu zinaonesha kuwa, jumla ya miradi 125 iliyowasilishwa kwa kuzingatia utaratibu wa *PPP*, imeshindwa kukidhi vigezo. Aidha, miradi minne ndiyo imekidhi vigezo na sasa inafanyiwa uchambuzi. Ili kuongeza kasi ya maendeleo na kukuza uchumi, mapendekezo ya miradi ifuatayo, ifanyiwe kazi haraka na ipewe muda wa kikomo ili ikamilike; miradi hiyo ni pamoja na:-

(a) Miradi ya ujenzi kama vile Mradi wa Barabara ya Dar es Salaam - *Chalinze Expressway*, yenye urefu wa km. 100, Mradi wa Barabara ya Arusha – Moshi - Himo yenye urefu wa Km. 105 na Mradi wa Usafiri wa Bahari kutoka Dar es Salaam hadi Bagamoyo.

(b) Kwa upande wa Sekta ya Uchukuzi Mradi wa Ujenzi wa Gati Na. 13 na 14 katika Bandari ya Dar es Salaam; Ujenzi na Upanuzi wa Bandari za Mwanza, Mbegani, Mwambani na Mtwara; Ujenzi wa reli kutoka Mtwara hadi Mchuchuma; Uboreshaji wa Reli kutoka Dar es Salaam mpaka Isaka; Uboreshaji wa Reli ya Tanga mpaka Arusha; Ujenzi wa Reli kutoka Arusha hadi Musoma; Kiunganishi cha Reli kwenda Bandari ya Mwambani - Tanga; Kiunganishi cha Reli kutoka Mbegani hadi Tanga; Ukarabati wa viwanja vya ndege vya Mwanza, Kilimanjaro, Mtwara na Arusha; Upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere na Ujenzi wa Bandari ya Nchi Kavu (*Kisarawe Cargo Freight Station*).

(c) Miradi ya ujenzi wa Majengo kwa ajili ya Ofisi, Biashara na Mabweni kwa Taasisi zilizo chini ya Wizara mbalimbali kwa mujibu wa Sheria ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi Na. 18 ya mwaka 2010 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya ubia kama hii inatarajiwa kupunguza mzigo kwa Bajeti ya Serikali na hivyo kuelekeza rasilimali ndogo kwenye maeneo machache ya kipaumbele tuliyojiwekea kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ina maoni kwamba, wakati umefika kwa Serikali kuweka utaratibu wa kutumia Mfumo wa *Accrual* kwenye malipo yake, ambao umebainika kuwa ni wa uwazi na ni rahisi kufuatilia malipo yanavyofanyika. Mfumo huu unatumika katika nchi za Australia na New Zealand na umeonesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa bajeti umeonesha kwamba, bajeti imejaribu kugusa watu wa chini, lakini katika mfumo ambao kwa namna fulani unaonekana kuwa na changamoto. Ni dhahiri kuwa, mapendeleko ya mifumo ya kodi na tozo mbalimbali zilizoainishwa zinaonesha nia ya Serikali

katika kutaka kuongeza mapato, lakini baadhiya mapendekezo hayo yana ugumu ndani yake. Hivyo, ni vyema Wananchi wakaelewa kwamba, nia ya Serikali ni kuboresha huduma kwa umma na huduma hizi zina gharama. Ni matarajio ya Kamati ya Bajeti kwamba, gharama zinazolipwa na Wananchi kwa njia ya kodi, zinatoa matokeo chanya kwa Wananchi kulingana na gharama hizo ambazo ndizo matarajio yao.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hiikukushukuru kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. William M. Mgimwa, Naibu Mawaziri wake; Mheshimiwa Saada Mkuya na Mheshimiwa Janeth Mbene, kwa ushirikiano wao waliontao kwa Kamati. Namshukuru pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), Mheshimiwa Stephen Wasira, kwa kushirikiana vyema na Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Tume ya Mipango, ambao walishirikiana na Kamati katika hatua zote za kujadili na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati hii, kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu uchambuzi wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka uliopita, mwaka huu na mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hiikwa umakini wa okatika kujadilina kutoa mapendekezo mbalimbali yaliyohusu uchambuzi wa Bajeti ya Serikali. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Andrew J. Chenge – Mwenyekiti, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Dkt. Cyril A. Chami, Mheshimiwa Mansoor S. Hiran, Mheshimiwa Josephat S. Kandege, Mheshimiwa Christina M. Lissu, Mheshimiwa Dkt.

Festus B. Limbu, Mheshimiwa James F. Mbatia, Mheshimiwa Assumpter N. Mshama, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mheshimiwa Saleh A. Pamba, Mheshimiwa Mwigulu L. N. Madelu, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Ritha L. Mlaki, Mheshimiwa John M. Cheyo na Mheshimiwa Peter J. Serukamba.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru pia Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah na Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati inayoongozwa na Ndugu Elisa D. Mbise na Makatibu wa Kamati; Ndugu Lina Kitosi, Ndugu Michael Chikokoto na Ndugu Michael Kadebe, kwa kuihudumia vyema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na nitamke kuwa, naunga mkono hoja hii. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunashukuru. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, sasa ilikuwa itolewe Maoni ya Kambi ya Upinzani, sijapewa rasmi taarifa kwamba itakuwaje. Kwa hiyo, tunaendelea kuchangia, kwa sababu bahati nzuri Kamati ya Bajeti ina watu wote ndani yake. Sijapewa rasmi kwa nini watu hawapo! Kwa hiyo, namwita Mheshimiwa John Cheyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Salim Hassan Turky na wengine nitawataja baadaye.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nazungumza baada ya kupata kauli nzito sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Lukuvi. Ombi langu ni kwamba, nchi yetu Mungu aibariki, turudi nchi ya amani na tufanye uchaguzi bila kupigana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lazima kwanza nijitambulishé kwamba, mimi pia ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti. Sasa Mwenyekiti wangu akishasema naunga mkono hoja na mimi natoka Kambi ya Upinzani, watu wote wanaonisikiliza watashangaa wakinisikia kwamba na mimi naunga mkono hoja ya Bajeti. Kwa sababu ni vigumu, wewe umechambua ile bajeti, umekuwa katika Kamati, umetoa maoni, halafu usimame hapa useme kwa sababu natoka Kambi ya Upinzani naipinga bajeti hii. Mimi naona nilitaka nilieleze hilo ili wanaonisikiliza waweze kunielewa vizuri zaidi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Fafanua Mheshimiwa Cheyo, siyolazima mtu apinge kwa sababu anatoka upande wa Upinzani. Atazungumza ubora wa bajeti au upungufu wa bajeti. Sasa hilo ndio tunasikia Wananchi wanaopenda kusikia. Wewe unatoka Kambi gani siyo muhimu sana, ubora wa bajeti ama upungufu wa bajeti, hiyo ndio useme kwa nguvu zako zote bila hata kujali unatoka wapi. Hata wa Chama cha Mapinduzi hivyo hivyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Huu umekuwa msimamo wangu kwa miaka mingi Mheshimiwa Spika. Ahsante sana kwa kuimarisha tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la kwanza, ni kwa mara ya kwanza tumeanza utaratibu huu wa kuzungumza kwanza *sectors* za nchi yetu halafu tunahitimisha na mrejesho kama Mwenyekiti wetu, Mheshimiwa Chenge, ambaye nampa hongera sana kwa *speech* yake, alivyofanya. Tunarejesha na kweli Serikali imeonesha kwamba, inaweza ikasikia na kama tulivyoonesha wiki iliyopita, tukapata billioni zaidi ya 500 na ushee.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa kuondokana na utaratibu wa zamani ukaingia kwa utaratibu mpya ambao unashirikisha watu wengi zaidi ambao unaishirikisha Bunge lako. Kwa hiyo, tunapoondoka hapa hii ni bajeti ya Bunge la Tanzania na siyo bajeti ya Serikali peke yake. Kwa hiyo, utekelezaji wake ni lazima uangaliwe na Bunge, kwa sababu hii Bajeti ya Bunge.

Sasa tatizo, kitu kipyä hakiwezi kwenda kwa haraka haraka unajua, lakini pia Serikali ina utamaduni wake ambao Wazungu wanasema *Conservatism*, yaani kung'ang'ania kitu hata ambacho siyo lazima uking'ang'anie. Nimeona kama mojawapo ya Kamati hii ya Bajeti, Serikali bado imeng'ang'ania upande wa mapato. Bunge linataka kushiriki katika kuainisha mambo mbalimbali ya matumizi, lakini pia upande wa mapato. Kwa sababu hatuwezi kuwa watu ambao kila wakati unasema nipe hiki nipe kile bila kujibu upande mwingine unanipa hiki kitu kutoka wapi?

Kwa hiyo, kama vile ulivyoona umuhimu wa kutusikiliza kwa upande wa matumizi kwa awamu hiyo ya kwanza ya majadiliano ya Bajeti, bado Serikali haijaona umuhimu wa kulisikiliza Bunge kwa upande wa mapato. Hii kama Mwenyekiti wangu alivyosema, ultengeneza kwa majoribio, mimi kweli ilikuwa kwa majoribio na nikitu ambacho ulithubutu na ulithubutu vizuri. Kamati Maalum ya Spika, ambayo sasa tunaiita ni Kamati ya Chenge na mimi nikawa ni mmojawapo wa Wanakati wale. Ili kuionesha Serikali kwamba, sehemu ya utafutaji wa mapato haipaswi tu kuhodhiwa na Serikali hata Bunge linaweza likaja na mawazo mbalimbali. Tumetoa maoni kwa upande huo, lakini kila tukiuliza Serikali tuambieni basi ni vitu gani ambavyo mmekubaliana na sisi; Serikali imefunga mdomo. Tuelezeni ni kitu gani ambacho hamkipendi katika mambo ambayo yametoka kwenye Kamati ya Chenge; Serikali haitaki kufunua.

Kwa hiyo, Serikali imekuja kulishtukiza Bunge na vyanzo mbalimbali na misamaha mbalimbali ya kodi na hatua mbalimbali bila kuliandaa Bunge katika kushiriki kikamilifu. Mimi natoa rai, kama tumeamua kuwa tuwe na Bajeti Shirikishi, basi Serikali kwa upande huo pia ifunguke. Itueleze vyanzo vyake inavyofikiria ili Waheshimiwa Wabunge nao waseme unakoenda huku unaachana nako afadhali upitie njia hii. Hii ndiyo dhana ya Bajeti Shirikishi. Kama tungeshirikishwa kwa muda mrefu, Serikali Waheshimiwa Wabunge, kuna mambo mengi ambayo yameletwa hapa na Serikali ambayo tungeweza kuyatolea maoni.

Mojawapo ambalo limezungumzwa kwa urefu ni mambo ya matumizi, lakini mimi nataka kujielekeza zaidi kwa matumizi ya pesa kwa upande wa nishati. Waheshimiwa Wabunge, hili tusipolipatia ufumbuzi kwamba wewe una Bajeti ya Serikali na inatumia zaidi ya asilimia 20 kuweza kugharamia umeme; hii ni hatari. Ndiyo kusema huna pesa kwa ajili ya mambo mengine. Umeme kila mmoja anapenda na mimi ni mmojawapo ambao nawaambia ndugu zangu kule Bariadi tumepata vijiji vingi ambapo tutapata umeme kutoka Bariadi, tunapita Kilulu, tunapita mpaka Lagagabilili; vijiji vyote hivyo karibu vitapata umeme. Tunatoka Bariadi mpaka Nanga, vijiji vyote katikati vitapata umeme.

Tunatoka Mwapalala mpaka Gambasingu na Lagagabilili, vijiji vyote vile vitapata umeme, lakini umeme huu kama aghali, hakuna atakayetumia. Tunataka tupate umeme ambao una bei nafuu na njia pekee ya kuweza kupata umeme ulio na bei nafuu ni kuhakikisha kwamba, tunalijenga lile bomba la kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam. Tukishafika hapo tutakuwa na *TANESCO* tofauti. Serikali haitatumia karibu bilioni moja kwa ajili ya umeme na pesa yote hiyo inaweza kwenda kujenga barabara, inaweza kwenda kujenga miundombinu ya maji, inaweza kupelekwa kwenye shule au inaweza kupelekwa kwa wanafunzi wa vyuo vikuu badala ya kupelekwa kwenye matumizi ya kufua umeme.

Sasa hivi bei ya umeme ni senti senti 40 na ushee. Ukipata umeme, ukipata gesi ni senti sita. Kwa hiyo, nawaambia ndugu zangu, hata wale ambao wanahamasishwa bomba lisijengwe, mimi naona wanakoseshwa njia. Ndugu zangu wa Mtwara wangedai kitu kimoja kwamba, gesi yote ile ambayo inatengenezwa Mtwara, waangalie ile mita yao. Ile mita inapotoa hiyo gesi ndiyo pale wanasesma na kipande changu cha pesa kiko wapi? Hiyo gesi unaenda kuifanyia nini? Itakusaidia nini wewe mtu wa Mtwara; hata ikienda kujenga kiwanda kwani ndiyo itakuwa inasema leta Wamachinga wote ndiyo waingie kwenye kiwanda?

Watakaoingia mle viwandani watakuwa Watanzania wa kila aina. Kama ikienda kujenga mambo sijui ya mbolea, kwani itakuwa kwamba Wamakonde wote wataingia katika viwanda; hata kidogo. Utaingia kufanya kazi siyo kwa sababu ni Mmakonde, utaingia kufanya kazi kwa sababu wewe una uwezo wa kufanya kazi na ni kazi za Watanzania wote. Pale kwenye mita kuna sehemu yao. Kwa hiyo, wito ambao nautoa, kwa sababu lazima tuinasue Serikali kutoka kwenye matumizi makubwa ambayo badala ya kwenda kwa maendeleo yanaenda kwenye umeme, sasa tujenge hilo bomba haraka na uzuri wake wametuambia ni miezi 18. Kwa hiyo, tuna muda tunaweza kujinasua katika miezi 18. Kama hiyo inawezekana, basi huo ni mradi ambao sisi wote tungeuchangamkia ili katika miezi 18 tuweze kuwa nchi tofauti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, amefanya mambo mengine, lakini mahali ambapo haijanipendeza; tulizungumza katika Wizara ya Kilimo kwamba, wakulima ambao wana matatizo mawili; mkulima sasa hivi adui yake namba moja ni tabianchi, adui yake wa pili ni bei. Ndiyo maana Serikali katika kilimo nasema tujaribu kuangalia mfuko ambao utaweza ku-support bei za wakulima kama vile bei za wakulima wa pamba. Hili sijalionna katika Hotuba nzima ya Mheshimiwa Waziri, labda angeliangalia huu ndiyo wakati wa kuanza.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu pamba imeenda chini kwa sababu bei ya mwaka jana ilipungua kutoka shilingi 1,200 na kitu mpaka shilingi 650. Kwa hiyo, watu wengi hawakulima pamba kwa sababu bei haijulikani. Mwaka huu nasikia kidogo bei imepanda na ni matumaini yangu msimu ungefunguliwa sasa ambapo bei bado inaweza ikafika hata shilingi 850 kwa kilo. Kwa hiyo, tukielekeza...

(*Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji*)

**SPIKA:** Ahsante, naona kengele ya pili.

**MHE. JOHN M. CHEYO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli, atafuatiwa na Mheshimiwa Eustace Katagira, Mheshimiwa Anastasia Wambura, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa na Mheshimiwa Kafulila.

Sasa aanze yule niliyemwita wa kwanza; Mheshimiwa Kuruthum, nadhani!

**MHE. KURUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache katika bajeti hii muhimu, Bajeti Kuu. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, aliye niwezesha kusimama hapa nikiwa salama ili na mimi niweze kuchangia machache.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti Kuu kwanza napenda nizungumzie tatizo la bajeti yetu; bado bajeti yetu ina tatizo la kimsingi katika mfumo wake.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, niangalie katika mfumo wa bajeti; mapato ya ndani ya Serikali, bado yanakuwa madogo kuliko gharama zile za kawaida, matumizi yale ya kawaida. Kwa mfano, katika mwaka 2012/2013 mapato ya ndani ya Serikali, yalikuwa ni trillioni 9.8, lakini matumizi yake yakaja yakafikia trillioni 10.59, hapa palikuwa na nakisi ya zaidi ya asilimia 1.5.

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika bajeti hii ambayo mwaka huu Mheshimiwa Waziri ameisoma ndani ya Bunge letu Tukufu, Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 ukiangalia mapato ya ndani yanafikia katika trillioni 11.5 na ukiangalia matumizi ya kawaida sasa yanaenda kwenye trillioni 12.5, ambako kuna nakisi ya trillioni 1.3. Kwa mpango huu, ina maana kwamba, Serikali haitakuwa na uwezo wa kujivekea akiba.

Mheshimiwa Spika, kweli tunaweza tukapanga mipango yetu kwa mtindo huu; Serikali inakuwa haina fedha ya kujiwekea akiba; ina maana likitokea lolote katika mambo ya miundombinu na vitu vingine, Serikali inakuwa haina kabisa fedha za akiba! Mimi naiomba Serikali iangalie, Kamati ya Bajeti imeshauri matumizi ya kawaida na mapato tunayopata bado kuna tatizo kubwa sana la mfumo. Pia katika mfumo huu mimi nategemea kwamba, Serikali haiwezi kujisimamia na kujitawala yenyewe kwa bajeti hii inavyoelekea.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nataka niongelee kidogo tatizo la bajeti yetu kuwa tegemezi. Bajeti yetu bado ni tegemezi kwa kiasi kikubwa, ukiangalia katika Mwaka wa Fedha wa 2012/2013, bajeti ilikuwa inategemea fedha za nje, misaada kutoka nje kwa zaidi ya asilimia 26.1. Ukichanganya na mikopo ya masharti ya kibiashara, ilitegemewa kufikia asilimia 34, lakini pia katika mwaka 2013/2014 bajeti yetu inategemea asilimia 21.1 na ukichukua na ile mikopo ya kibiashara itafikia asilimia 30.4.

Mheshimiwa Spika, bado bajeti yetu ni tegemezi. Kwa hiyo, mimi naishauri Serikali, iangalie vizuri upande wa makusanyo. Twende vizuri katika makusanyo ili tuwesze kufanya bajeti yetu isiwe tegemezi sana. Kila siku ninaposikia hapa makusanyo yanapandishwa katika sigara na pombe, bado ninajiuliza; tunaacha vitu vingine muhimu ambavyo vingeweza kutuongezea makusanyo katika nchi yetu. Kwenye madini mpaka leo bado tunasuasua, kama tungkusanya vizuri kwenye madini katika zile /levy, tungepata pesa za kutosha ambazo zingeweza kupeleka bajeti yetu vizuri zaidi kuliko kutegemea kila siku sigara na pombe. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, hivi kwa mfano, sigara ikiwa haitumiki kamatunavyofikiria sasa aupombe haitumikikamatunavyofikiria sasa, ina maana nchi yetu itakuwa hajjiendeshi? Hatuwezi kutegemea kuendesha nchi yetu kwa kutegemea tu bajeti ya pombe na sigara kila mwaka, hii inachosha katika vitabu vyetu, kila mwaka ukisikiliza Hotuba pombe, sigara; madini yako wapi? Tungepata pesa nyingi za /levy kutoka kwenye madini zingeweza kutusaidia kupata mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Spika, katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, wakati anasoma bajeti ukurasa wa 76, aliongelea kipengele cha kusema kwamba, anafuta kodi kwa magari yenye ujazo wa cc 501. Ina maana hapa alikuwa anamaanisha kufuta katika bajaji na pikipiki. Mheshimiwa Waziri, alisema kwa furaha kabisa kwamba, sasa vijana wetu watakuwa huru kwa kufuta kodi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi bado nina wasiwasi, tulikuwa tunaangalia mchakato na kuna maoni mengi sana ya Wadau huko nje; inaonesha kwamba, kufuta kodi kwenye Bajaji na kwenye pikipiki wala sio suluhisho, kwa sababu bajaji na pikipiki, bado zitaendelea kuwanufaisha wale wanaomiliki na siyo vijana wetu. Kuna wafanyabiashara, mtu anamiliki mpaka bajaji 30, bajaji 20, kwa hiyo, unavyofuta kodi kwenye bajaji siyo kwamba, eti vijana wetu ndiyo watajikwamua kiuchumi, hiyo siyo kweli, watanufaika wale ambao wanafanya biashara ya bajaji na wanaomiliki pikipiki. Kwa hiyo, bado hii haijaweza kuwakomboa vijana wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunakosa mapato. Kama mapato yetu bado ya kusuasua hivi kwa nini tufute kodi kwenye Bajaji na pikipiki? Kwa kuwanufaisha watu wachache na sio wale vijana ambao tunawakusudia? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, aiangalie vizuri hii kodi kwa Bajaji na pikipiki, bado inanipa mashaka kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, mimi ni kijana na pia ni mwanamama; ameongelea kuongeza bajeti katika Mfuko wa Wanawake (*WDF*), lakini pia ameongelea kuongeza bajeti katika Mfuko wa Vijana (*YDF*). Ameongelea ile bilioni mbili kwenye Mfuko wa Wanawake na akaongelea bilioni tatu kwenye Mfuko wa Vijana, *YDF* na *WDF*. Changamoto iliyoko kwenye *WDF*na *YDF*ni ule utaratibu mzima wa kwenda kugawa zile pesa kule chini, pesa mimi sikatai kuongeza ni jambo zuri sana kwa sababu vijana watapata mkopo.

Mheshimiwa Spika, lakinimiminilikuwepokatika Halmashauri na nimeona hali halisi kwamba, pesa zile zinakwenda kwa watu ambao siyo walengwa. Kwa hiyo, tunakusudia kwenda kuongeza pesa kwenye Mfuko wa Wanawake na Vijana ili sasa wakapate mikopo waweze kujikwamua kiuchumi, lakini utakuta wanaambiwa Kikundi, ukienda utamkuta mtu mmoja badala ya kukuta Kikundi kama tunavyokusudia.

Mheshimiwa Spika, tumepata pia uzoefu kutoka kwenye mabilioni ya JK, yamekwenda kule katika Halmashauri zetu na sehemu nyingine. Ni vijana wangapi au ni akina mama wangapi ambao walikuwa wanastahili kupata zile pesa walipata na wakaweza kujikwamua kiuchumi? Kwa hiyo, nashauri kwamba, utaratibu kuanzia Wizara ya Vijana na pia utaratibu kwenye jinsia kule chini kwenda kwa Maafisa Maendeleo wetu, zile pesa zikagawiwe kwa *SACCOS* za akina mama ambazo zinafanya vizuri. Kuna *VICOBA*, ambazo zinafanya vizuri, zitaweza kweli kuleta tija, lakini zikigawiwa kama sadaka kama sasa hivi haziuliziki, wanaopewa wale marejesho hawarejeshi kwa hiyo, sitegemei kama pesa zinaweza zikaleta mabadiliko yoyote. Naomba nishauri utaratibu uangaliwe vizuri, ili tupate japokuwa hata kama milioni kumi kila Halmashauri zinakwenda, basi zionekane zimeleta changamoto na mabadiliko kuliko utaratibu uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho napenda kukizungumzia ni ule mfumo mpya ambao Serikali imekuja nao wa *Big Results Now*. Serikali yetu imekuja na mfumo wa *Big Results Now* kwa sababu wanasmae mfumo huu utapelekea kuangalia utekelezaji wa ile miradi mikubwa mikubwa. *Big Results Now* wakati tunajadili bajeti mwaka jana (2012/2013) haikuwepo, yaani hatukuiona kwa uwazi, sasa inakuwa kama Serikali yetu inakuja na mifumo, yaani vitu ambavyo vinapandiwa pandiwa tu, mimi ninavyoona, yaani vinakuwa havina utaratibu na mpangilio maalum. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunakuja na *Big Results Now*, sasa mbona katika bajeti ya mwaka jana hatujaiona? Utaratibu wake ukoje? Mimi sipingi *Big Results Now* kwa sababu mnasema italeta tija kwa miradi mikubwa, lakini sasa mbona tangu hapo

mwanzoni haikuwepo, mwaka jana mbona haikuongelewa? Tunaona imekuja tu katikati, tunasikia tu *Big Results Now, Big Results Now*, kweli italeta mafanikio? Kwa nini isiwe katika *plan tangu mwanzoni?* Imekuja kutokea tu katikati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi inanipa hofu hii mipango ambayo inakuja kupangwa katikati tu, haiwezekani inatoka *from nowhere*, unakuta mpango umekuja. Tunakuwa mabingwa wa kuwa na mipango, wa kuwa na sera, lakini hazitekelezeki. Mimi zinanipa shida, *Big Results Now* inanipa shida, kwa sababu imepandishiwa katikati. Huko mwanzoni hatukuona imetengenezwa vipi, bajeti ya mwaka jana haikuonekana, sasa hivi tunaona inatokea.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu na mimi nichangie katika Hoja hii ya Waziri wa Fedha. Nimetumwa na nimeombwa na Wananchi wa Kyerwa, kuishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi, Serikali sikivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kyerwa waliomba wapewe Wilaya, wamepewa Wilaya, wanaishukuru Serikali sikivu ya Chama cha Mapinduzi. Wananchi wa Kyerwa waliomba wapewe Halmashauri, Halmashauri imeshaanza; Wanaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Zaidi, Wananchi wa Kyerwa waliomba wapewe Mradi wa Umeme; wameahidiwa kutekelezewa Mradi wa Umeme, wameahidiwa si kwamba, umeme utafungwa mpaka Makao Makuu ya Wilaya mpya, lakini wameahidiwa kwamba, umeme utasambazwa katika Vijiji vyote vya Wilaya ya Kyerwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninashauri na ninaiasa Serikali na ninaiomba sana Serikali, katika kutekeleza huu Mradi wa Umeme, ili umeme usambazwe katika eneo lote la Kyerwa, Serikali iutekeleze Mradi kama ulivyo. Serikali iutekeleze Mradi kama ilivyoahidi, isambaze umeme katika Kata zote na Vijiji vyote vya Wilaya ya Kyerwa, kama jinsi ilivyo katika mpango. Hapa naongelea Kata za Mlongo, Kata za Kibingo zimeahidiwa,

Kata ya Rutunguru, Kata ya Kaisho, Kata ya Isingiro, Kata ya Kyerwa, Kata ya Nkwenda, kama ilivyokuwa zamani, Kata ya Rwagwere, Kata ya Kimuli, Kata ya Kamuri, Kata ya Mabira na Kata ya Bugomora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Kyerwa wanaahidi kwamba, wakisambaziwa umeme, kama Serikali ilivyoahidi, kwamba, umeme watautumia kujilettea maendeleo na watautumia kuzalisha mali ambayo itaimarisha uchumi, si katika Wilaya vya Kyerwa peke yake, lakini mchango wao katika Taifa zima. Watajenga viwanda vya kukoboa kahawa, watajenga viwanda vidogovidogo, ilimradi vijana wapate ajira na hamtawaona Vijana wa kyewa wakija kufurika mijini kufuata mambo ya biashara ndogondogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee ushuru kwenye magari madogo. Mheshimiwa Waziri, anaomba turidhie aweze kuongeza ushuru wa asilimia tano katika magari madogo yenye umri wa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, nataka nimwombe Mheshimiwa Waziri, aangalie na afahamu kwamba, haya magari ya miaka kumi na zaidi, ndio ambayo yananunuliwa na kuendeshwa na Watanzania walio wengi wa kiwango cha chini. Vijana wetu wanaomaliza masomo, wataanza kazi katika mabenki, katika Serikali, wanachukua mikopo lakini hawanunui magari ya miaka miwili, hawanunui magari ya miaka mitano, wananunua magari ya zaidi ya miaka kumi na kigezo kwamba, haya magari yanaharibu mazingira nadhani siyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nieleze kwamba, msingi mzuri wa kodi huwa ni kumtoza yule mwenye kikubwa, yule alienacho, kuliko kumtoza yule mdogo. Mimi ningefurahi na ningeshauri Mheshimiwa Waziri, arejee atoze wale wenye uwezo, wanaonunua magari mapya, wanaonunua magari ya miaka miwili, miaka mitatu, lakini asirejee kwenda kuwatoza wale vijana wetu ambao wanamaliza vyuo, wanakopa pesa ili waweze kununua magari madogo ya kuwasaidia. Ningemba hili suala liangaliwe upya na magari ya zaidi ya miaka kumi, hii nyongeza ya asilimia tano isiwepo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hali hiyohiyo, Mheshimiwa Waziri, anatuomba turidhie katika speech yake ukurasa wa 69 kwamba, kodi ya ushuru iongezwe kwenye magari ya kazi kwa kiwango cha asilimia tano, ambayo ni magari yenye umri wa zaidi ya miaka kumi.

Mheshimiwa Spika, nazidi kumsihi Mheshimiwa Waziri, aliangalie upya; magari ambayo yanatumiwa na Watanzania Wazawa, yanayonunuliwa na Watanzania Wazawa ni yenye umri wa zaidi ya miaka kumi. Kama unatembea barabarani, unatoka Dar es Salaam unakuja Dodoma, ukikutana na magari ya *Iveco*, magari ya *Leyland* mapya, magari ya *Mercedec Benz* makubwa, haya siyo magari ya Watanzania Wazawa wanaohangaika. Ukikutana na *Fuso* la miaka 12, limebeba nyanya, limebeba korosho, limebeba vitunguu, linatoka Singida, linatoka Tanga, haya ndiyo magari ya Mtanzania anayoyatumia kule vijiji kuweza kuendesha maisha yake na kuweza kuihudumia jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, namshauri Mheshimiwa Waziri, arejee tena katika maelezo yangu, awatoze walionacho, asiwabane ambao wana kidogo. Hawa Wananchi wetu awaache waendeleekununu magari, haya magari hayaharibumazingira kama tunavyoambiwa; haya magari yanasakiya kuchochea maendeleo katika shughuli ndogondogo kule vijiji.

Mheshimiwa Spika, nazidi kurudia; naomba Mheshimiwa Waziri, aangalie haya magari yanayotumika kama *utility vehicles*, abadilishe nia yake ya kuyatoza ushuru. Pia aangalie haya magari madogo yanayotumiwa na Watanzania ambao hawana pesa nyingi sana, asilaongezee ushuru.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee suala la kuondoa msamaha wa VAT kwenye utalii. Mheshimiwa Waziri, katika ukurasa wa 63, ana nia ya kuondoa msamaha wa VAT kwenye shughuli za utalii. Sina ugomvi na mapendekezo yake, lakini ni vizuri akafanya *effective date*, terehe ya kuanza kuondoa msamaha huu, badala ya kuwa tarehe 1 Julai iwe tarehe 1 Januari. Nasema hivyo kwa sababu shughuli za utalii, watalii wanaokuja huwa wana-book shughuli zao mapema, huwa

wanalipa mamepa, ambao watakuja mwezi wa 8, watakuja mweziwa 9, watakujamweziwa 10, sasa hiviwotewameshafanya mikataba na pia wameshalipa. Kwa hiyo, kubadili Sheria kwa wakati huu kwa haraka ni sahihi, lakini ningependekeza kwamba, *effective date* ya kuweza kuondoa msamaha huo iwe ni tarehe 1 Januari, badala ya tarehe 1 Julai.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu nichangie, lakini pia napendekeza niliyoyapendekeza yafanyiwe kazi. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. ANASTASIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa, nianzie na changamoto ambayo imejitokeza, ambayo tunaifahamu kwamba, sasa hivi tunahangaika ili tuweze kujua tunatatua vipi tatizo la ukusanyaji wa mapato katika nchi yetu; kwa sababu tumekuwa tukivutana hapa na pale kila mara katika kila Wizara kwamba, kipengele hiki kiongezwe, lakini tunapata wapi fedha.

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja labda nianzie kuishauri Serikali kuwa, irejee upya suala la Mikataba ya Kibiashara. Katika uzoefu nimeweza kubadilishana mawazo na baadhi ya Viongozi wa nchi jirani; kuna nchi moja ya Kenya, wao Katiba yao imeweka sharti kwamba, mikataba yao yote ya kibiashara isisainiwe mpaka ipite Bungeni; inapita Bungeni, Bunge linaangalia, linatoa ushauri na pale ndipo mikataba inapoweza kusainiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna nchi moja ya Nigeria, wao wanasema kwamba, Serikali inapata asilimia 50 kutokana na uchimbaji wa mafuta, asilimia 50 ya faida Serikali inapata. Nchi moja ya Liberia wanapata asilimia kumi, lakini sasa ukija kuangalia nchiyetu kutokana na uchimbaji wa madini, tunapata mrabaha wa asilimia nne; kwa kweli bado tuko chini sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya suala la mikataba, tuweze kuboresha mikataba yetu, asilimia tunayopata ya mapato ya uchimbaji wa madini na masuala mengine, baadaye nadhani tutakuja kwenye masuala ya mafuta tuhakikishe kwamba, mapato haya yanamnufaisha Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kuna Biashara za Kimataifa, nadhani sote tutakubaliana kwamba, sasa hivi katika nchi yetu ni kitu ambacho kimeanza muda mrefu kidogo, siyo siku za karibuni sana. Kuna suala la *dumping*, hili ni tatizo kubwa katika nchi yetu na hata jana nimeona kwenye mtandao kuna mabati ambayo yamekamatwa bandarini ya thamani ya shilingi milioni 900 hayana viwango na hii ni *typical dumping*. Sasa wenzetu wanafanya nini?

Mheshimiwa Spika, wenzetu wanatumia *anti-dumping duties* kupunguza hili tatizo, kwa sababu tatizo hili ndilo ambalo linauwa viwanda vyetu. Viwanda vyta nchi yetu vinakufa na sote ni mashuhuda, *POLYTEX* imekufa, *Textile Industries* karibu zote ziliathirika na tatizo hili la *dumping*. Pamoja na kwamba kutakuwepo na michango mingine ambayo ilisababisha kufa kwa viwanda vyetu, lakini *dumping* limekuwa ni tatizo kubwa na hasa masuala ya matairi, nadhani sote tumekuwa ni mashahidi matairi yanaingia siku hiyo hiyo mtu unaweka tairi kwenye gari na tairi lina-*burst*.

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukajikwamua katika eneo hili kwa ku-introduce *anti-dumping duties* na hizi unaweza ukaweka kiwango chochote ilimradi isizidi *dumping margin* na *dumping margin* ni ile kwamba, kama bidhaa ya nchini; kwa mfano, bati moja linauzwa labda shilingi 13,000 na lile linalotoka nje linauzwa shilingi 10,000, sasa ile shilingi 3,000 ndiyo inayotakiwa iwe *anti-dumping duty*, ambayo haizidi ile bei ya kawaida ya lile bati likiuzwa nchini. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile tuki-introduce hii *anti-dumping duties*, tutaweza kulinda viwanda vyta nchi yetu, lakini vilevile tutazuia uingizwaji wa bidhaa feki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tunaweza tukaenda katika maeneo mengine, vipuri vingi sana ni feki katika nchi hii, vinaleta umaskini kwa Wananchi kwa sababu ananunua leo mtu kesho kimeharibika ananunua kingine. Kwa hiyo, katika hili suala la bidhaa feki tunaweza tukaweka kuna kitu kinaitwa *TBT*

*measures kwamba ni lazima bidhaa zinazokuja zioneshe trade mark na origin yake na kama hawafanyi hivyo, basi wanaweza wakachajiwa duties ambazo zinastahili kwa kutokufanya hivyo.*

Mheshimiwa Spika, labda niingie katika masuala ya unyanyasaji wa kibiashara kwa wenzetu ambao wanafanya biashara za *export*. Nadhani tumeshasikia hawa wanao-*export* Konyagi nchi ya Kenya, wamepata matatizo sana. Baada ya kuona kuna soko zuri sana Kenya kule, wanaambiwa sasa tunataka Konyagi ya *mills* 200, wakifanya hivyo wanaambiwa tunataka ya 250; kwa hiyo, imekuwa ni usumbufu. Sasa kuna kitu kinaitwa *Advisory Centre on WTO Law*, Serikali inaweza ikatumia chombo hiki kuomba ushauri na pengine ikafungua mashitaka kwa ajili ya usuluhishi wa matatizo kama haya. Huo ni mfano tu wa Konyagi, lakini pia kuna wafanyabiashara wa maziwa wananyanyasika sana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mapato ya biashara za ndani, Serikali imejitahidi sana ku-*improve* mapato ya nchi yetu, kwa mwezi tunakusanya hela nydingi. Ninachotaka kusema ni kwamba, kwa utafiti nilioufanya kwa kutumia *frequency* ya kwenda ku-*purchase* katika maduka mimi mwenyewe binafsi, hizoz *frequencynimezichukulia* kama ni mtu tofauti amekwenda kila wakati, kwa kweli hali ni mbaya, tunachokikusanya labda ni robo tu ya mapato, kila ninapokwenda, yaani labda *exception* ya *supermarkets* ndiyo utakuta asilimia 80 wanatoa risiti bila kulazimishwa, lakini maduka mengine ni asilimia 20 tu ndiyo wanaotoa risiti *including* vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, sasa labda nitoe wito tu kwa Wananchi, watambue kwamba, anapokuwa hapati ile risiti anakuwa amelipa kodi, lakini kodi inabaki kwa mfanyabiashara haiendi Serikalini; hilo ni wazi kabisa. Atakapokuwa amepata risiti hasa kwa kutumia hizi *electronic fiscal device*, ina maana kwamba, taarifa zinakuwa zinaenda *TRA* na atawezekulipa ile kodi. Kwa hiyo, Wananchi tunapokaa tunalalamika, wakati mwingine tunachangia sisi wenyewe kujiangusha na kwa mtindo huu basi ina maana tunaongeza ile *gap* kati ya aliyenacho na asiyenacho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawaomba sana Wananchi na pengine Serikali iweke Namba za *TRA* katika maduka ambayo yanatakiwa kulipa *VAT* ili mtu unapopata tatizo fulani uweze kupiga simu kwa wahusika, kwa sababu mara nyingi unakuta unachanganyikiwa. Unapoomba risiti unaweza ukazubaishwa pale dakika 40. Kuna *Super Market* moja mimi nimekwenda, waliamu kugeuza karatasi za risiti zikawa zinatoka *plaintu*, sasa nilipoangalia nikashangaa, lakini wateja wengine walikuwa wanachukua hivyo hivyo, nilipolalamika ndiyo sasa wakaanza kutafutana na baadaye baada ya kulazimisha sana, dakika 40 nimesimama pale ndiyo wakatoa ile risiti na kuanzia hapo wakageuza lile karatasi na wateja wengine wakaanza kupata risiti. Inabidi Wananchi wenyewe tuchachamae na masuala haya, kwa sababu tunaumizwa sisi wenyewe, huduma tunakosa wote.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kuwaomba Wananchi katika ngazi mbalimbali; ngazi za vijiji na ngazi nyingine, wawe wafuatiliaji wazuri wa matumizi kwa sababu tutakapotumia vizuri hizi *resources* ambazo tumeletewa; kwa mfano, juzi tu hapa tumeambiwa na Dokta Gwajima kwamba, pesa za afya zinapotea lakini si matatizo ya *MSD* wala si matatizo ya Serikali, ni kutokana tu na kutokufatilia. Dawa zinakwenda vijijini lakini zinaibiwa. Bahati nzuri juzi nilipouliza hapa swali la Mheshimiwa Al-Shaymaa, kuna Wananchi ambao waliskia, kuhusu huduma za elimu kwa watoto walemvu. Sasa kwa mujibu wa huyo Mwananchi aliyenipigia simu, walikaa kikao wakakuta watoto waliopo katika mazingira hatarishi hawalipiwi, wakalalamika lakini Mtendaji wa kile Kijiji alitoa majina ambayo hayapo pale kijijini, majina feki kabisa.

Mheshimiwa Spika, Mwenyekiti wa kile Kijiji akawa ametoa majina ya watoto wanaostahili kulipiwa, lakini Mtendaji ametoa majina yake anayoyajua na pesa zimetumika. Kwa hiyo, ni wajibu wa Wananchi kufuatilia matumizi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Serikali ya mwaka huu ni triliioni 18.2. Katika hizo, triliioni 5.7 ni bajeti ya maendeleo. Hii triliioni 5.7 yote mia kwa mia inaenda kwenye manunuzi. Bajeti ya matumizi ya kawaida ni triliioni 12.67, hii asilimia 60 au 70 inaenda kwenye manunuzi, sasa kwa ujumla wake wote ina maana asilimia 80 ya triliioni hii 18.2 inaenda kwenye manunuzi. Hii maana yake ni kwamba, ukitaka bajeti hii ifanikiwe, ukitaka kupeleka huduma kwa Watanzania kwa kutumia bajeti hii, lazima udhibiti manunuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba unipe ruhusa ninukuu ukurasa wa 50 wa bajeti, Mheshimiwa Waziri anasema:

*"Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu Serikali itatekeleza sera za matumizi zifuatazo; ya mwisho inasema kuzingatia Sheria za Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi wa Umma."*

Mheshimiwa Spika, nikienda ukurasa wa 82 naomba ninukuu tena anasema:

*"Kwa kutambua kwamba, Sekta Binafsi ndiyo yenye msukumo mkubwa katika maendeleo ya uchumi Duniani kote, napendekeza kufanya marekebisho katika Sheria ya Public Procurement Act, 2011 na Public Private Partnership Act, 2010 ili kuwezesha unsolicited PPP proposals kutohusika na utaratibu wa ushindani."*

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Manunuzi hiyo tumeitunga mwaka 2011 mpaka leo hamna Kanuni, mpaka Mheshimiwa Waziri anapendekeza kuirekebisha hiyo Sheria ili aweze kuingiza kipengele hiki. Sheria imemruhusu Mheshimiwa Waziri baada ya kuitunga Sheria tunakupa mwaka mmoja utunge Kanuni ili Sheria ianze kutumika.

Mheshimiwa Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, anapokuja kutoa majumuisho hapa, aliambie Bunge lako hili Kanuni za Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2011 ziko wapi? Ili utakapofanya marekebisho Sheria ianze kutumika kuwe na Kanuni na bajeti hii haiwezi kutumika mpaka tudhibiti manunuzi ya umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nataka niongelee matumizi, nanukuu vilevile Bajeti ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa 50 anasema:

*"Manunuzi ya magari mapya yamepunguzwa na yananunuliwa kwa kibali cha Waziri Mkuu tu na ukubwa wa engine umepunguzwa na kubaki zenyenye ukubwa uliokubalika CC 3000 au chini ya hapo."* Safi sana, hii ina maana Serikali inapunguza matumizi. Hapa nina hoja mbili; la kwanza, ni kweli Waziri Mkuu yuko hapa amesema manunuzi ya magari hayawezi kununuliwa mpaka atoe kibali yeye. Leo ndiyo yuko Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanda Peter Pinda, kesho akiwa Waziri Mkuu mwingine na akalitupilia mbali hilo! Naiomba Serikali itunge Sera, *Car Policy*, Sera ya Manunuzi ya Magari tujue kwamba, manunuzi ya magari ni CC 3000 kuwe na Sera ambayo ipo kabisa inaweza ikatungiwa hata Sheria; hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili katika hili hili, Sheria ya Manunuzi inasema, mali ya umma unainunua kwa *tender* na hata kui-dispose kwa *tender*. Kuinunua kwa *tender*, kui-dispose kwa *tender*, sasa imetokea tabia ya ajabu sana kwa Viongozi wa Serikali kujiuza magari. Wanajiuzia magari wenyewe; kwa nini hatufuati utaratibu wa zamani ambapo magari yakitumika yalikuwa yanawekwa kule *Government Stores* kule *Nyerere Road*, baadaye yanapigwa mnada by *tender*. Siku hizi kila mtu anajiuzia na namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu Wizara ya Fedha ndiyo *custodianwa Procurement*, magari haya ambayo yanauzwa yauzwe kwa *tender* kama yalivyonunuliwa kwa *tender*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze maana kuna Idara nyingine za Serikali ambazo zinanza magari kwa *tender*, kwa hiyo, ningeomba Idara nyingine ziige mfano huo; Watu wa Usalama wa Taifa, magari yote yanayotumika likishachoka yanakusanywa kule Kijitonyama baadaye wanatangaza mnada kwenye magazeti, watu wanaenda kununua *by tender*. Kwa hiyo, ninaomba Idara na Wizara nyingine zote ziige mfano huo wa Usalama wa Taifa wa kuuza mali ya umma *by tender* kama ilivyo-*acquire by tender*.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee kuhusu Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi. Barabara imeanza zamani, imeanza mwaka 2008; kwanzia, kandarasialiyekuwepowa Kenya amegombana na *TANROADS* wakapelekana Mahakamani miaka miwili, mitatu, wamechelewesha barabara yetu hiyo baadaye wamepatikana makandarasi wengine wawili; mmoja anaanzia Mbeya mpaka Lwanjilo, mwingine anaanzia Lwanjilo kwenda Chunya, baadaye tutampata mwingine kutoka Chunya kwenda Makongorosi. Sasa Mheshimiwa Rais, akiwa pale Mbeya kwenye Sherehe za Mei Mosi, alisema, Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi anaipa uzito mkubwa sana; na akasema yejote atakayechelewesha barabara hii kukamilika kabla ya 2015 tumwambie Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, sipendi nianze kumshitaki Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa Mheshimiwa Rais kuwa, hatoi mafungu ya kujenga barabara hiyo. Mheshimiwa Waziri ni rafiki yangu, naomba sana mwaka huu mafungu yanayotakiwa kwenda kwenye Barabara ya Mbeya – Chunya – Makongorosi, yaende kwa wakati ili kutimiza Ahadi ya Rais alioisema mwaka huu kwenye Sherehe za Mei Mosi.

Mheshimiwa Spika, niongelee tumbaku kidogo. Kilimo cha tumbaku ni kilimo kigumu sana. Kilimo cha tumbaku, mkulima anaanza kilimo mweziwa tisa, wakatiwa kiangazindiyo anaanza kuweka vitalu wanaita mabedi; kuanzia mwezi wa tisa yuko shambani mpaka atakapokuwa anauza mwezi wa tano, sita, saba, nane. Kwa hiyo ni mwaka mzima anahangaika na kilimo, inatakiwa kilimo hiki kimpe mafao mkulima, hali ya maisha yake ibadilike. Hali ya maisha ya mkulima mwaka na mwaka

ibadilike kutokana na kilimo hicho, maana wakati wa kukausha tumbaku kuna *taboos* wanasesma mwanaume ukilala ndani ya nyumba tumbaku inaharibika, ina maana wewe unakausha tumbaku unalala nje kwa muda wa mwezi mzima, wanasesma ukilala ndani tumbaku inaharibika, wana maana yao ambayo sijui maana yake nini.

Mheshimiwa Spika, ninachotakaku-*underscorenikwamba*, wakulima wanamenyeka mno na kilimo cha tumbaku, bei yake kwa mwaka huu ni nzuri sana, lakini kuna mdudu yupo katikati hapa Ushirika; Ushirika wanafanya ujisadi wa kutisha sana kwa wakulima wa tumbaku. Kwangu Wilaya ya Chunya, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mheshimiwa Deusdedit Kinawilo, alipoona ujisadi huo wa Ushirika katika kilimo cha tumbaku, ameunda Tume imechunguza imeyapata hayo ambayo imeyapata anayo.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri wa Kilimo ushirikiane na Mheshimiwa Kinawilo, muifanyie kazi hiyo Ripoti aliyoipata ya Ushirika kuwafisadi wakulima wa tumbaku. Naomba Waziri wa Kilimo ushughulike sana, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo alipokuwa Naibu Waziri wa Nishati, ni rafiki yangu, ni mdogo wangu, amekuja Chunya amesaidia sana kupeleka umeme kwenye vijiji mbalimbali Wilayani Chunya. Naomba katika hili pia aje Chunya, atumwe na Waziri wa Kilimo aje Chunya, ashirikiane na Mkuu wa Wilaya waifanyie kazi hiyo ripoti kuweza kuwaondolea wakulima mzigo wa Ushirika ambao unawanyonya wakulima.

Mheshimiwa Spika, napenda katika hili, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, huyu mama jasiri sana, alipoona ujisadi huu kwenye Mkoa wake, ujisadi huu kwenye Mkoa wa Tabora, ameamua kuupiga chini Ushirika kama Serikali; na baada ya kuupiga chini Ushirika ameongea na Waziri wa Kilimo alete Mkaguzi Mkuu wa Serikali kuja kukagua badala ya kukagua huyu COASCO wao huyu anaendelea kukagua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namwomba Waziri wa Kilimo pamoja na kupeleka CAG kwenda Tabora kukagua Ushirika unavyowafisadi wakulima, naomba upeleke maeneo yote. Mumpeleke CAG maeneo yote aende Chunya, aende Iringa, aende Mpanda kote huko aende Mkaguzi Mkuu wa Serikali aende akakague Ushirika unavyowafisadi wakulima wa tumbaku na kuwafanya wanyonge mwaka hadi mwaka.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali iangalie sana kilimo cha tumbaku, Ushirika unawanyonya sana wakulima mpaka APPEx hii ya Morogoro inawanyonya wakulima sana, wamejifanyia kama kajimafioso fulani hivi. Naiomba sana Serikali kupitia Waziri wa Kilimo, iwaangalie Wakulima wa Tumbaku Tanzania, isikie kilio chao, ikague, iviwezeshe Vyama vya Msingi vikope vyenyewe kwenye mabenki vilete pembejeo, huu Ushirika hapa katikati tuondokane nao.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia Hotuba hii muhimu kabisa, Hotuba ya Bajeti ya Nchi ikiwa ni mara yangu ya tatu sasa.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu kwa kiasi kikubwa imejaliwa mambo mengi sana na Mwenyezi Mungu, lakini bahati mbaya sana tunafanya mambo ambayo nadhani hata Mwenyezi Mungumwenyeweyanamkera. Waziriwa Fedha na Mheshimiwa Wasira, kwa pamoja wamezungumza kwamba, Tanzania kwa mujibu wa Kamisheni ya Masuala ya Uchumi ya Umoja wa Mataifa ni mionganoni mwa nchi 20 ambazo kasi yake ya ukuaji wa uchumi iko juu Duniani.

Mheshimiwa Spika, lakini hawasemi kwamba, Tanzania hiyo hiyo ni mionganoni mwa nchi 20 maskini kabisa duniani. Kwamba, wakati Tanzania ni mionganoni mwa nchi zenyeye kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi Duniani, nchi 20, kwa maana ya ukuaji wa asilimia saba, wakati huo huo Tanzania hii ni mionganoni mwa nchi 20 maskini kabisa Duniani; sababu ni nini?

Mheshimiwa Spika, sababu ziko wazi; moja ya sababu ni kwamba, uchumi huu ambao tunauzungumza kukua, ni uchumi ambao haubebi watu wengi. Wakati Uchumi wa Taifa unatangazwa kukua kwa asilimia saba, uchumi wa vijijini unakua kwa takribani asilimia tatu. Kule vijijini ndiko ambapo kuna asilimia 75 ya Watanzania, tunazungumza kila kukicha kwamba tunapaswa kukuza uchumi vijijini, lakini bado Serikali haioneshi utashi wa kukuza uchumi vijijini na sababu ziko wazi. Kwamba, Serikali ili iweze kukuza uchumi wa vijijini, inahitaji kutengeneza miundombinu ya uhakika vijijini; kwa maana ya umeme, kwa maana ya maji, kwa misingi ya biashara, misingi ya kilimo kule vijijini; na ili iweze kufaya hayo, lazima iwe na fedha na ili iwe na fedha lazima ikusanye kodi. Tuna bahati mbaya sana kwamba, kwa muda mrefu tuna Serikali ambayo haikusanyi kodi. (*Makofi*)

Tuna Serikali ambayo ni bingwa wa kutoa *exemption*; ni bingwa wa kutoa misamaha ya kodi katika Afrika ya Mashiriki, sisi ndiyo tunaongoza, tunatoa kati ya asilimia 3.5 mpaka nne. Wenzetu wa Afrika ya Mashariki wanatoa asilimia moja. Sisi tunatoa misamaha ya kodi kwa asilimia 3.5 ya *GDP*; hii ni hasara ya mabilioni ya shilingi. Fedha hii ingelikusanya ingeliweza kutosha kuelekezwa kujenga miundombinu ya maji vijijini na kujenga miundombinu ya uhakika ya umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, Tanzania utafiti ulifanywa na *C/NOVET*, Taasisi hii ni miongoni mwa Taasisi kubwa sana inayokusanya maoni Duniani. Katika mwaka 2009, kero nambari moja Tanzania *C/NOVET*, wameonesha ni maji. Ni aibu kwa Taifa ambalo lina kiasi kibuwa cha maji Duniani, eti nalo linalia ukosefu wa maji.

Pale Ziwa Tanganyika, nilikuwa na Waziri wa Mazingira juzi, nawaambia maji yote, *fresh water* yote Duniani ni kilomita za ujazo milioni 35. Ziwa Tanganyika peke yake lina kilomita za ujazo 5,800,000. Tafsiri yake ni kwamba, asilimia 17 ya maji tunayo Tanzania, lakini bado Tanzania haina maji; hii ni aibu. Siyo Tanzania tu, pale Kigoma ukienda kule Kalya, Sunuka, Igala, Sigunga, watu wako mita 200 kutoka usawa wa Ziwa ambalo lina maji safi, lakini hawana huduma ya maji. Hawa watu hawana namna ya kuisamehe Serikali hii.

Tuna Serikali ambayo haikusanyi kodi. Nimewaambia mara kadhaa kwamba, moja ya njia ya kudhibiti uchumi, moja ya njia ya kufanya watu wengi washiriki kwenye uchumi, ni kuhakikisha sehemu kubwa ya mitaji inakuwepo kwenye Soko la Mitaji, ili watu wengi waweze kushiriki. Kikubwa zaidi, kodi zipatikane. Duniani kote wanafanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, leo hiitunayomakampuniyanayotafuta gesi, tunayo makampuni ya madini, yanakwenda kuorodhesha, yanakwenda kutangaza hisa kwenye *Toronto Stock Market*. Wanakwenda Canada, wanakwenda UK, wanakwenda kuorodhesha kule, lakini *Dar es Salaam Stock of Exchange* hawaorodheshi. Hasara yake ni kwamba, wanatengeneza mitaji kupitia rasilimali zetu, lakini sisi kama sisi hatushirikishwi. Pia tunakosa uwazi katika mitaji yao na matokeo yake wana-*under estimate profit*. Matokeo yake wanafanya makadirio ya chini ya faida na matokeo yake tunapungukiwa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yote haya yanafahamika. Mwaka 2010 imetungwa Sheria hapa, Makampuni ya Madini yote yanatakiwa yaorodheshwe kwenye Soko la Mitaji (*DSE*), lakini mpaka leo Kanuni tu kutengenezwa, haijatengenezwa. Mwaka 2010 ilipitishwa Sheria ya Makampuni ya Simu yaorodheshwe pale ili yawe wazi, lakini mpaka leo hii mwaka wa tatu.

Mheshimwia Spika, safari ya kwenda mwezini, ni kama mwaka mmoja tu unakwenda mwezini na mwaka mwingine unarudi. Huyo mtaalam wa kutengeneza hizo Kanuni, hata angelikwenda mwezini na kurudi, angeshakwenda mwezini akaleta Kanuni na akarudi kwao mwezini.

**SPIKA:** Unakwenda kwa miguu? (*Kicheko*)

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, tunazungumza haya kwa machungu kwamba, kigugumizi hiki siyo bure ni kwa sababu Serikali hii ni ya kifisadi; huu ndiyo ukweli, unaweza ukakubali, ukazunguka, ukaenda kushoto. Mwalimu Nyerere alisema, Serikali ya Kifisadi haiwezi kukusanya kodi. Mmebaki mnawatoza kodi, maskini mama zangu wa vijijini, ukienda kule vijijini watu wanatozwa ushuru wa mihogo. Wenye

vibanda, wenyе *viosk*, wenyе maduka madogo madogo, hawa ndiyo wanaotozwa ushuru, wanalipia taratibu zote za kodi. Watu wenyе mitaji mikubwa ni *untouchable* hawashikiki hapa. Wanatucheka kweli, ukienda kwenye hoteli kubwa, wanazungumza, kama hawajakuona wanatukana wanasema hii nchi ni shamba la bibi, mtu ye yote anaweza akazoa tu, hakuna utaratibu hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi napenda kusema kwamba, kama tutaendelea na utaratibu huu wa kutotoza, wa kutokuhakikisha Makampuni ya Madini yanalipa kodi, Kanuni ziandaliwe waanze kulipa kodi sahihi. Kama tutaendelea na utaratibu huu wa Makampuni ya Simu yasiendelee kulipa kodi, tutawaambia Wananchi hawana sababu ya kulipa ushuru sokoni. Haiwezikani mtoze ushuru wa mihogo halafu makampuni makubwa kama haya hayalipi kodi! Tungeliweza kuwasamehe wote hawa akina mama wanyonge, tungeliweza kuwasamehe vijana wote hawa wanyonge. Makampuni haya ni lazima yalipe kodi la sivo hatuwezi kukubaliana. Tunazungumza tujenge nchi pamoja; tutajenga nchi pamoja wakati mnasamehe vitu viko wazi, haiwezikani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni nchi yenye *potential* nyingi, nilikuwa ninashangaa; Tanzania ni nchi ya tatu kwa kuwa na ng'ombe wengi katika Bara la Afrika, kule Ethiopia ng'ombe ni moja ya sababu kubwa sana katika uchumi wao, sisi kwetu ng'ombe ni kero kabisa. Hivi ni vituko kabisa, yaani tumekosa akili ya kututoshakuona kwamba hawawenyeng'ombeni Wawekezaji. Mnasafiri kwenda Ulaya kutafuta Wawekezeji, kuna Wafugaji hapa wana ng'ombe wengi, mnashindwa kuwapanga kufanya hiki kitu kiwe uwekezaji! Mtapewa fursa zipi ili muweze kujenga Taifa hili? Mimi ninafikiri mmeshindwa.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza hapa kwamba, mipango mingi inapangwa hapa, mifumo yake ya kiutekelezaji haiko bayana. Ndiyo maana tulipitisha mpango hapa kwenye Bunge hili wa *Stimulizer's Package*, kiasi cha takriban 1.7 billion. Shilingi 1,700,000,000 kwa ajili ya *Stimulizer's Package*.

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi uliwahi kumwelekeza Waziri wa Fedha humu kuna uchakachuaji mkubwa kwa mujibu wa Taarifa ya CAG kuhusu fedha hizo. Ukaelekeza hapa Waziri wa Fedha alete majina ya hao watu waliofaidika nazo, mpaka leo hawajaleta. Kwa hiyo, tuna matumizi mabovu na ya hovyo. Kuna genge la watu wachache wanatafunu nchi hii wakati wanyonge wanakosa hata maji; haiwezekani.

Mheshimwia Spika, juzi hapa nimezungumza kwamba, *NBC* wakati ipo chini ya Serikali, kuna watu walikopeshwa takribani shilingi bilioni 60, wakaweka dhamana kama asilimia tano ya mkopo wote. Hawa watu wana fedha, wako mjini, tukaiambia *CHC Kwamba*, hawa watu lazima walipe. *CHC* wakasema watalipaje wakati dhamana zao hazilingani na mkopo wao?

Mheshimiwa Spika, ninaomba tena Waziri wa Fedha alete majina ya watu wote waliokopa fedha hizi. Shilingi bilioni 60 ni fedha nyingi sana. Haya mambo yanatia uchungu. Wenzetu Kenya pale Bajeti yao imesomwa juzi, wanaonesha Bajeti ya *Jubilee* ya Kwanza wanafuta umaskini wa watu 10,000,000. Wanatengeneza ajira 1,000,000. Sisi Bajeti yetu hii hata haina *focus*. Haioneshi, mnapunguza umaskini kwa asilimia ngapi, mnatengeneza ajira ngapi kwenye Bajeti hii, haiko bayana na haipimiki. Kenya wanazungumza kupeleka *Laptop*, kupeleka *computer* kwa kila Mwanafunzi wa Shule ya Msingi; Sisi Tanzania hata madawati yanatushinda. Hii ni Bajeti ya 50 mnakaa hapa Bungeni, madawati mnashindwa, nchi yenye misitu kama hii!

Chama Tawala Kamati Kuu yake, kazi yake ndiyo yenye jukumu la kuisimamia Serikali. Kwa mwaka inakutana mara nne. Kwa miaka 50 imekutana mara 200, lakini imeshindwa kutoka na majibu ya madawati. Mtaaminiwa mara ngapi muweze kuitumikia nchi hii; kwa nini tusiamini kwamba mmeshidwa? Kamati Kuu 200 zimekutana tangu tupate Uhuru mpaka leo, *issue* ya madawati imeshindikana kabisa, watoto wanakaa chini. Nchi tajiri kama hii, haiwezikani, lazima kuna mambo yafanyike, ni mambo ya aibu, hakuna maelezo. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nitamwita Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Amour na Mheshimiwa Injinia Ramo Makani, nafikiri atakuwa ni wa mwisho kwa siku ya leo hii.

**MHE GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi nichangie. Nianze kwa kuipongeza Serikali kupitia Wizara hii ya Fedha, kwa kuja na Bajeti ambazo mimi nimekaa Bungeni hapa huu ni mwaka wa saba sasa, lakini Bajeti ya mwaka huu ni tofauti na Bajeti za miaka iliyopita. Hii ni Bajeti ambayo kimsingi iko *focused*, tofauti na wenzangu wanavyosema, maana imenuia kutatua matatizo ya Watanzania wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sisi Wabuge ni mashahidi hapa Bungeni, kupitia Kamati zako za Kisekta, kupitia Kamati ya Bajeti, tuliomba zaidi ya shilingi bilioni 600 za ziada. Zimeongezwa zaidi ya shilingi bilioni 500 za ziada na Serikali imekubali. Hii ni *willingness* kubwa ya Serikali kuhakikisha kwamba, inatatau matatizo ya Watanzania. Sasa watu wasioona hii, inaweza ikawa bahati mbaya sana, lakini mimi ninataka niipongeze sana Serikali kwamba, hapa tulipo nadhani tumeendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie jambo la mwanzo, hiyo ilikuwa ni *preamble* tu; ninaomba nianze na suala la rushwa.

Mheshimiwa Spika, rushwa inatupunguzia pesa sana ambazo tunapitisha kwenye Bajeti hii. Wenzangu wamesema pesa ambazo zinaenda kwenye shughuli ya maendeleo moja kwa moja ni karibu shilingi trillioni tano, lakini inawezekana rushwa katika hizi, ikatuchukulia zaidi ya trillioni moja; kwa hiyo, tukakosa pesa za kwenda kwenye maendeleo. Kwa hiyo, tunapaswa kuwa waangalifu sana katika jambo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kilichonisukuma nizungumzie hili, ni jambo ambalo Mkurugenzi Mkuu wa PCCB, Dkt. Hosea amelisema juzi alipokuwa anazungumza na Wabunge. Waheshimiwa Wabunge, mlikuwepo, mimi bahati mbaya nilikuwa kwenye majukumu mengine sikuwepo. Dkt. Hosea amesema, anafungwa mikono kushughulika na wala rushwa

katika nchi hii hasa katika Serikali. Kauli hiyo ya Dkt. Hosea ilikuwa nzito sana. Ningeliomba Serikali itoe tamko juu ya kauli ambayo imetolewa na Dkt. Hosea, kwa sababu ni kubwa. Kama hivyo ndivyo, kwa kweli hata sioni maana ya kuwepo *PCCB*, kama watu wanaweza wakafungwa mikono wanaposhughulika na rushwa; hii ni kauli nzito sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nilijiuliza pia hivi kwa nini Dkt. Hosea mpaka leo hii bado ni Mkurugenzi Mkuu wa *PCCB*? Nilijiuliza sana, kama anafungwa mikono kwa nini asiondoke awaachie wanaoweza kufanya kazi? (*Makofî*)

Mheshimwia Spika, ningelikuwa mimi ndiyo Dkt. Hosea, ningeliwataja wala rushwa. Moja, mbili, tatu, wanakula rushwa, nimezuiwa kushughulika halafu ningelijiuzulu. Akitoa matamko makubwa kama yale halafu akiachwa, nadhani ni hatari sana kwa Serikali na kama ni Mtumishi wa Serikali hilo ni jambo la hatari sana. Ninaomba Serikali ilitolee tamko linalostahili. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, yako malalamiko ya Watanzania kwamba, pesa hazikusanyi, ni kweli hatukusanyi pesa inavyotakiwa. Nitoe mfano mmoja tu; juzi juzi, nadhani wiki iliyopita, pale Bandarini zilikaguliwa kontena zaidi ya 500; ambazo zilikuwa zinakisiwa kuwa na bidhaa tofauti na ambazo ziko *declared* kwenye fomu. Kontena zile zilipokaguliwa, 180 zilikutwa na bidhaa tofauti na zile ambazo ziko *declared* kwenye fomu na kwa maana hiyo kwenye fomu zilikuwa zimeandikwa bidhaa ambazo ni za thamani ndogo kuliko ambazo zipo kwenye kontena. Zilipolipishwa ushuru, nadhani zaidi ya shilingi bilioni 1.2 zilikusanywa pale pale. Sasa huu ndiyo mchezo ambao umekuwa unaendelea kila siku pale bandarini.

Mheshimiwa Spika, nilichosikia cha ajabu na vichekesho, wale waliokamatwa na vitengo vinavyohusika pale Bandarini na *TRA*, wamehamishwa vitengo. Sasa unazuia wizi au unataka wakaanze *syndicate* ya wizi mahali pengine?

Mheshimiwa Spika, na mimi nilitegemea Waziri alitolee tamko mnawafukuza au mnawahamisha hamisha, maana ndio tunafuga wizi, hatukusanyi pesa kwa sababu ya wizi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali pia itoe tamko kupitia Wizara hii, Waziri atakapokuwa ana-*wind up* ayasemee haya. Watu hawawezi kuwa kwenye mtandao wa wizi, badala ya kushughulika nao mnawahamisha, mnawapa nafasi ili wakale vizuri pesa zile walizoiba, wakastarehe nazo vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba, baadhi ya Wafanyakazi wa Serikali wanaishi maisha ambayo ni tofauti kabisa na mishahara yao. Wafanyakazi ukienda Bandarini kule, ukienda *TRA*, watu wanaishi maisha ambayo siyo ya Watanzania, wanazipata wapi pesa? Tunasema tunayo Taasisi ambayo inachunguza watu wanapata wapi mali, lakini Tanzania leo nkinunua gari la shilingi milioni 400 mpaka 500 hata siulizwi nimepata wapi hizo pesa. Kwa hiyo, mnashangaa, hata humu ndani watu wana magari ya shilingi milioni 400 au 500, lakini kipato chao hakifanani na magari wanayomiliki, hakifanani na nyumba wanazo miliki na hakifanani na utajiri wanaomiliki. Serikali tumenyamaza; haiwezekani.

Ninaiomba Serikali ya Chama cha Mapinduzi ichukue hatua, maana mengine haya tunazalisha wenyewe kwa Wananchi. Mimi ninapoishi maisha ambayo siyo ya kwangu halafu ninakwenda kuhubiri kwamba katika nchi hii uko wizi na mimi mwenyewe ninaishi maisha ambayo hayafanani na mimi, sijui kama Watanzania watakuwa wanaelewa! Ninaomba Serikali hilo nalo iliangaliwe vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, yako malalamiko ya Wananchi hasa wastaafu; bado wastaafu wetu wanalipwa hela ndogo sana. *Monthly pension* kima cha chini nadhani wanalipwa shilingi 51,000, jamani shilingi 51,000 kwa leo ni nauli ya kutoka hapa Dodoma kwenda Mbeya, *one way*, unamlipa Mtanzania ambaye ametumikia nchi yake sawa sawa; na hili ninamwomba Mheshimiwa Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, ninajua

Bajeti imeshapita, lakini *Inshallah* Mwenyezi Mungu akijalia, mwaka 2014, ninaomba Kamati za Kisekta zinazohusika, Kamati ya Uchumi na baadaye Kamati ya Bajeti, hebu tu-review viwango ambavyo wanalipwa wastaifu wetu, ni vidogo mno. (*Makof*)

Watanzania wanapiga kelele kila mwaka viwango hivi ni vidogo. Mimi nina hakika nchi hii hatujakosa pesa za kuwaongeza hawa Watanzania waliotumika vizuri. Sambamba na hilo, hizi pesa wanapaswa kulipwa kila baada ya miezi mitatu au siku 90, wengi wamekuwa wanalamika wanapata baada ya siku 120. Hebu ninaomba Waziri wa Fedha, hili liko ndani ya uwezo wako, tuwapatie hawa Watanzania, hata kama ni kidogo wanachokipata basi wakipate kwa wakati. Nadhani tutakuwa tunapunguza malalamiko ili waweze kuishi vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningelipenda nilizungumze ambalo tunajiuliza pia; tumepitisha bajeti ya shilingi trilioni 18.2, lakini *disbursement* yake itakuwaje Mheshimiwa Waziri na mimi ninataka *commitment*ya Serikali? Tumeongeza pesa za maji, tumeongeza pesa kwenye REA, tumeongeza pesa kwenye Taasisi mbalimbali zaidi ya shilingi bilioni 500, hizi tuhakikishe zinakwenda; maana kama tumepiga makofi hapa Bungeni halafu pesa hizi zisiende, Watanzania wataona ndiyo yale yale, wanaongeza pesa kwenye makaratsi, kwenye maendeleo hakuna kinachoonekana na hili linaweza likatuangusha.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri alishawaeleza Watanzania kwamba, hizi pesa zitakwenda. Tunaomba tutakapokuja kwenye Bunge lingine, kila baada ya miezi mitatu, Mheshimiwa Waziri utoe taarifa kwamba *quarter* hii tuliahidi zingelikwenda bilioni kadhaa zimekwenda zote. Mkituletea hadidhi tofauti hapa, itakuwa tunawadanganya Watanzania na mimi nisingelipenda Serikali ya Chama cha Mapnduzi ionekane inawadanganya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni misamaha ya kodi. Misamaha ya kodi ni mikubwa sana, Mheshimiwa Waziri ameshazungumza sana na ninyi kwenye Wizara mmeliona. Mnasema mnataka kuandika sheria upya, kuzi-review sheria upya, mzilete hapa Bungeni ili tupunguze misamaha ya kodi. Mimi ninawaunga mkono, lakini tuombe hizi sheria tuzipate Bunge linalokuja. Bunge ijalo mzilete hizo Sheria tuzipitie, maana sasa hivi tunapoteza pesa nyingi sana kupitia misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Spika, hata mimi nilishangaa kwa sababu *CAG* alitoa Taarifa yake ya mwaka 2010/2011 kwamba, kulikuwa na misamaha ya kodi ipatayo karibushilingi trillioni moja, akaishauri Serikali ipunguze misahama hiyo ya kodi. Kinyume chake, mwaka 2011/2012 kwa Taarifa ya *CAG* ambayo ndiyo *latest*, badala ya misamaha ya kodi kupungua, imeongezeka kutoka shilingi trillioni 1.00 kwenda karibu shilingi trillioni 1.8 au 1.9 hivi. Sasa *CAG* anashauri kwamba, punguzeni misamaha ya kodi, kinyume chake misamaha ya kodi inaongezeka. Wizara ina excuses kwamba, sheria zetu ndivyo zinavyoruhusu, Sheria ziko *loose*, tunaomba mtuletee sheria ili tuweze kubadilisha misamaha hiyo ya kodi na iende kwa Wananchi wenyewe ambao wanakusudiwa, badala ya kila wakati misamaha hiyo kwenda kwa watu ambao wana pesa. Tulitegemea misamaha ya kodi iwe na *impact* kwa Wananchi walio wengi, maskini wa nchi hii, badala ya kuwasaidia wale watu ambao wanacho tayari.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalize kwa kusema kwamba, ninaomba Serikali iangalie upya, hebu tupidie upya suala la kodi ya dizeli ya shilingi mbili tu tulivoiongeza.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda Mbeya hivi karibuni, nimesikia maoni ya Watanzania, ile shilingi mbili tulivoiongeza kwenye dizeli, inaweza ikawa na athari mbaya. Kwenye *petrol* sina sababu ya kuzungumza, kwa sababu ninajua Watanzania wanaotumia magari ya *petrol* mengi ni ya starehe na siyo

ya kazi. Magari ya kazi yanayobeba mizigo ambayo ndiyo inakuwa na athari kwenye uchumi wa nchi na kwa Wananchi wa kawaida, tukiongeza hiyo shilingi mbili, bado athari yake itakuwa inaenda kwa Mwananchi wa kawaida maskini.

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali na kwa sababu Mheshimiwa Waziri bado ana siku hapa tuangalie je, hatuwezi tukaiondoa hii shilingi mbili tukaipeleka mahali pengine ili angalau Wananchi waweze kupata unafuu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ninaomba nizungumzie Benki ya *TIB*. Benki ya *TIB* sijaona kama umeitilia mkazo sana Mheshimiwa Waziri. Hii Benki kama ingepewa pesa za kutosha, maana yake Wananchi au wanaokopa kwa ajili ya kuendeleza viwanda wangeweza kuwa wana nafasi nzuri zaidi kukopa na kwa maana hiyo, tungeendeleza viwanda na Watanzania wangepata ajira. Ninaomba ulisemee hilo maana sijalionia kama linajitokeza sana Mheshimiwa Waziri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kuongea hayo, nahisi muda wangu umekwisha na ninasema ninaunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. (*Makof*)

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze kwa kuipongeza Serikali kwa Bajeti iliyokuja kwa mwaka huu. Bajeti ya mwaka jana siyo ya leo, kidogo kidogo tutakwenda na mwisho tutafika huko tunakokusudia. La pili, kwa kila kizuri hakikosi kasoro. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, ninaanza na viwango vyatiki kodi kwenye petroli na mafuta ya taa. Baada ya kuona suala la uchakachuaji limezidi, Serikali ikaamua kiwango cha kodi cha

petroli na kiwango cha kodi ya mafuta ya taa viwe sawa sawa ili kuondosha uchakachuaji. Ghafla leo hii ninaona petroli imepanda kiwango chake cha kodi na mafuta ya taa yako pale pale. Ninataka kumwuliza Mheshimiwa Waziri; je, katika tathmini uliyoifanya umeona uchakachuaji haujapungua na kama umepungua unataka turudi kule kule kwenye uchakachuaji? (Makofi)

Suala lingine, naipongeza Serikali kwa dhati kwa kuja na mfumo mpya katika kutoa makontena. Mfumo huu utawezesha kujua kitu gani kilichokuwepo mle ndani, tofauti na ile *system* inaona tu, lakini haijui *quality* ya kitu kilicho ndani na wafanyabiashara wanadanganya, wanaweza kusema hili shati ni la tetroni, kumbe shati ni zuri zaidi na bei yake ni nzuri, wakawa wanadanganya, likipita kunako *system* linapita tu. Mfumo huu mliokuja nao kwa makontena yote isiwe ya fulani au ya fulani, yote yafunguliwe pale na yatazamwe halafu ndiyo yalipiwe ushuru. Kama makontena yataleta msongamano, nakubali yatafutiwe pahala yawekwe, mjenge sehemu myaweke, lakini tuhakikishe kontena lolote lazima lipite kwenye *system*, lifunguliwe, lichekiwe, lichambuliwe kitu kimoja kimoja. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninakuja kunako masuala ya magari yaliyokuwa zaidi ya miaka kumi, ushuru umepanda kutoka asilimia 20 mpaka 25. Hapa nina masikitiko makubwa, haya ni magari ambayo tunanunua sisi walala hoi, hatuwezi kuyanunua magari ya bei kubwa kwa sababu ushuru wake unakuwa mkubwa.

Ninakuomba Mheshimiwa Waziri, kwa kuwa unataka tununue hayo magari mapya, punguzeni ushuru na sisi hatutanunua tena haya ya zaidi ya miaka kumi, tutakuja kununua hayo mnayotaka ninyi mnunue; lakini kuwa haiendi sambamba hivi, itakuwa wale waliokuwa nayo watakuwa nyo magari, sisi tusiokuwa na magari tutabakia hivyo hivyo tukipanda balskeli. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nitakuja kunako Watendaji wa *TRA*, hawa kila mwaka nawasema lakini hawataki kubadilika sijui kwa nini! Pamoja na juhudzi za Serikali ilizochukua kwa wengine kuwafukuza kazi wa *TRA* waliokuwa wabovu, walikuwa wabadhirifu, wala rushwa, lakini bado rushwa inaendelea. Ninaiomba Serikali adhabu wanayopewa ni ndogo mno ya kufilisiwa mali zao na kushitakiwa, haitoshi, watangazwe hadharani ili wajulikane Tanzania nzima, wasiweze kuajiriwa popote, hii ndiyo itakuwa dawa yao. Maana yake kila wanavyofanywa hawasikii, hawa ni wabadhirifu, pamoja na sisi tunajitahidi kutafuta vyanzo vya kodi, lakini vikifika pale vinaingia mifukoni; kweli tutafika tunakotaka kwenda na ni lazima hatua kali zichukuliwe kwa hawa watendaji wabovu, watangazwe hadharani, hawa ni wauaji hasa, sijui hukumu gani unaweza kuwapa wakaachana na mambo hayo?

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninakuja kunako ushauri, pamoja na kuwa kuna vyanzo vingi tumeviibua vya mapato, lakini *research* ya uvuvi hebu iangaliwe, tunaweza tukakusanya mapato mengi kunako sekta hiyo.

Kwa vile nimechangia mengi na nimetoa ushauri mwingi kunako Kamati ya Bajeti, naona niwapishe wenzangu hizi dakika zilizobakia waweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nami namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kupata fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu nikiwa mchangiaji wa mwisho kwa asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, nitaanza kama walivyofanya wengine, kwanza, kwa kukupongeza wewe binafsi kwa ubunifu ambao hatimaye ulipelekea mabadiliko haya ya mchakato mzima wa bajeti; na kwamba, sasa tumepata fursa zaidi kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,

kuweza kuisaidia zaidi Serikali, kuweza kulisa idia zaidi Taifa hili katika kupanga si tu bajeti, lakini pia kuweka mipango yote inayoendana na maendeleo au mustakabali wa maendeleo ya Taifa hili kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hapo awali ilikuwa siyorahisi kupunguza matumizi ya Serikali, ilikuwa siyo rahisi kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato katikati ya mjadala wa Bajeti, lakini imewezekana kuwa hivyo, hata sasa tunaweza kupata fursa zaidi ya kuweza kujadili katika maeneo hayo, kwa sababu ya utaratibu mpya ambao tunautumia hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini hapa niseme kitu kimoja kwamba, jambo kubwa ambalo wote tunapaswa kulifahamu na kulizingatia ni kwamba, liko jukumu au yako majukumu ya Serikali, lakini kwa kiwango kikubwa majukumu ya Wananchi mmoja mmoja kila Mwananchi ni muhimu zaidi. Kwa hiyo, katika ngazi ya Mwananchi mmoja mmoja, suala la kufanya kazi zaidi, suala la kujitoa, suala la kujinyima, haya ni masuala ya msingi na kwa hiyo, ukienda kuyaweka katika utaratibu wa kibajeti, maana yake ni kwamba, pale ambapo tutalazimika kulipa kodi, basi tusione kama vile tunaonewa au kama vile Serikali imekosea; hapana, ni jukumu letu kuchangia ili tuweze kufanya nchi hii iweze kupiga hatua. Kwa hiyo, Wananchi wapokee majukumu yao na hasa kushiriki katika mchakato mzima wa kuwezesha Serikali kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, mimi sitakaa sana upande wa mapato, nimejiandaa zaidi upande wa matumizi na niende haraka haraka kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana, utamaduni tuliojijengea ni wa kwamba tunachopaswa kukipanga au kama bajeti ni fedha tu peke yake, lakini ili nchi iweze kupata maendeleo siyo fedha tu peke yake. Rasilimali zinazowezesha mchakato huu wa kujitafutia maendeleo ziko nyingi, nikizitaja chache pamoja na fedha ni rasilimali watu, lakini pia rasilimali

nyingine ambazo zinaendana na vifaa na mambo kama hayo. Bahati mbaya, mahali ambapo hakuna fedha, shughuli za maendeleo hazipangwi au hazifanyiki. Mahali ambako hakuna fedha hakuna manunuzi yatakayofanyika, lakini kwa bahati mbaya sana mahali ambako hakuna rasilimali watu ambayo inaweza kukidhi haja, tunapeleka fedha.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari na kwa hakika, hii ni mojawapo ya maeneo makubwa sana yanayotusababishia sasa hivi tushindwe kupiga hatua, licha ya kutenga fedha kila mwaka, pamoja na uchache katika hatua ya awali kwamba, fedha hazitoshi, lakini pia matumizi ya fedha hizo huko tunakozipeleka ni eneo ambalo tunatakiwa kujipanga nalo vizuri zaidi.

Mimi ninayo machache kama mapendekezo. La kwanza, tunao utaratibu wa kaguzi na kwa kiwango kikubwa kaguzi zinafanyika na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, lakini pia *PPRA* kwa masuala yanayohusiana na manunuzi na kwawale ambaohawafahamu, *Professional Boards*, vileyoyombo mbalimbali vytaalam navyo pia vinafanya kaguzi.

Kwa hiyo, kama Taifa, sasa hivi tunatakiwa nguvu hizi zote za vyombo hivi vyote vinavyoshughulika na kaguzi mbalimbali, kwenye masuala ya fedha yanayoendana na shughuli za maendeleo na utekelezaji wa miradi kitaifa, vifanye kazi kwa pamoja, vibadilishane taarifa na vichukue hatua za pamoja pale inapobidi. Kwa kufanya hivyo, tutaondokana pia na utaratibu au kasoro inayojitokeza ambayo inasababishwa na watendaji tu wa kawaida, ambao kutokana na nafasi zao, pengine mara nyingi wanajinufaisha zaidi, lakini kumbe vyombo vyao vya kitaaluma vingeweza vikachukua hatua mapema tungeweza kudhibiti hali hiyo.

Kwa mfano, kwenye utekelezaji wa miradi ambayo inaendana na uhandisi, iko Bodi ya Usajili wa Wahandisi, kwa Wahasibu tunayo Bodi ya Wahasibu, hata kwa Wachumi. Nataka kusitiza kwamba, kila taaluma inayo Bodi Maalum inayoshughulikia maadili ya taaluma hizo. Sambamba na hilo, nimewahi kutoa maoni haya kabla, lakini ninapenda kutoa

maoni pia hivi sasa kwa kusema kwamba, umefika wakati sasa kama Taifa tukapitia upya Sheria ya Maadili ya Viongozi. Tutoke kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi tupanue wigo sasa iwe ni Sheria ya Maadili ya Taifa. Ndani ya Sheria ya Maadili ya Taifa, ndiyo kiwepo kipengele cha maadili ya viongozi, kiwepo kipengele cha maadili ya wanataaluma, wataalam, kiwepo kipengele cha maadili ya watoto, vijana, akina mama na kadhalika. Kwa namna hiyo, tutaboresha maadili ambayo ndiyo tatizo kubwa linalotusababishia wizi, rushwa na mambo mengine kama hayo, ambayo yanababisha upotevu wa rasilimali na kwa hiyo, kupunguza kasi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalopenda kulizungumzia sasa hivi ni vipaumbele au ugawaji wa fedha, maana kupanga ni jambo moja, lakini kutekeleza bajeti kwa maana ya kugawa fedha tutakazoweza kuzikusanya pia ni eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, utaratibu unaotumika mpaka sasa ni wa *cash budget*, maana yake ni kwamba, unachukua fedha ulizopata katika kuzikusanya ndizo unaenda kuzipeleka kwenye eneo la utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Sasa naamini mara nyingi hupati fedha zote kwa ajili ya mahitaji yote uliyonayo kwa wakati, sasa upeleke fedha wapi, kwa nini; hili ni eneo ambalo nafikiri Serikali inabidi kuliangalia vizuri zaidi. Licha ya vipaumbele vilivyopo katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, licha ya vipengele viliviyomo katika mpango wa kila mwaka; kwa mfano, mpango wa mwaka huu, lakini ndani ya vipengele vile au vipaumbele vile ni vizuri pia kuangalia vipaumbele ndani ya vipaumbele.

Katika ngazi ya kitaifa, napendekeza kwamba, Miradi ya Maendeleo mikubwa ile ya Kitaifa tuliyonayo, tupeleke nguvu zetu katika hatua ya awali kwenye Sekta ya Reli na Bandari. Sekta hizi kwa maoni yangu ndizo ambazo zinaathiri sekta nyingine kubwa vilevile na muhimu vilevile, lakini kama utataka kusema uweke kipaumbele cha kwanza halafu vingine vifuatие, basi cha kwanza kiwe ni Bandari na Reli. Katika eneo hilo la Bandari na Reli, unazungumzia Reli ya Kati, Bandari ya Dar es

Salaam, lakini kwa umuhimu ule ule katika hatua ya baadaye kidogo unazungumzia pia Reli inayotoka Bandari ya Mtwara na Bandari ya Mtwara yenye, lakini pia Reli inayotoka Bandari ya Mtwara kwenda Bandari ya Mbamba Bay.

Ukizungumzia Bandari ya kutoka Mtwara kwenda Mbamba Bay, unazungumzia *Mtwara Corridor*, katika *Mtwara Corridor* kuna miradi mingi ndani yake, unaweza kuiita *Mtwara Corridor* kama programu, ndani yake kuna miradi, ukiwepo Mradi wa Reli niliyoitaja, Mradi wa Bandari, lakini pia iko Miradi ya barabara. Vipande ambavyo sasa hivi vinatusumbua na ambavyo bado havijapiga hatua ni kile cha Namtumbo - Tunduru na kile cha Tunduru - Mangaka na Mangaka - Mtambaswala.

Naipongeza Serikali kwa kuwa Kandarasi aliyesababisha ucheleweshaji wa barabara kipande cha kutoka Namtumbo mpaka kufika Tunduru, tayari amekwishafukuzwa. Licha ya kuipeleka Serikali mahakamani, kesi ile Serikali imeshinda kwa sababu ya umakini mkubwa uliofanyika katika hatua za awali kabla ya kumfukuza, katika hatua hiyo napenda kuipongeza Serikali.

Napenda kutoa wito kwa Serikali kuongeza kasi ya kuweza kupatikana Mkandarasi mwingine na taarifa ninayo kwamba, Serikali tayari inaongeza kasi, lakini naomba waongeze zaidi ili tuweze kupata Mkandarasi haraka kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huu. Pia kipande cha kutoka Tunduru kwenda mpaka Mangaka, Wakandarasi watatu ambao wanatafutwa hivi sasa, ipo katika hatua za mwisho mwisho, lakini napenda tuongeze kasi ili tuweze kuanza utekelezaji wa Miradi ile kabla mvua hazijaanza.

Mheshimiwa Spika, kwa leo nilijiandaa kama ambavyo nimekwisha wasilisha, napenda kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona huyo alikuwa msemaji wetu wa mwisho kwa mchana, lakini tukirudi jioni ataanza Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Salim Hassan Abdullah Turkey, Mheshimiwa Silvestry Koka, Mheshimiwa Abia Nyabakari, Mheshimiwa James Mbatia, Mheshimiwa

17 JUNI 2013

Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Obama, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir, Mheshimiwa Blandes na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na wengine watatajwa.

Sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.51 mchana Bunge lillifungwa hadi saa 11. 00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilitrudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilishawataja wale ambao wangeendelea kujadili mchana huu, ambao ni Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Salim Hassan Turky, Mheshimiwa Silvestry Koka na Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari. Tuanze na Mheshimiwa Martha Mlata!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi ili na mimi niweze kuchangia bajeti hii.

Kwanza kabisa, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na Manaibu wake, Katibu Mkuu na Watendaji wotewa Wizara yake, kwa bajeti ambayo wameileta; kwa kweli ni nzuri. Bado nakupongeza Mheshimiwa Waziri, kwa juhudhi kubwa ambazo umezifanya hasa kuhakikisha Wizara zote, fedha walizoomba umeweza kuwapatla; nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Nitakuwa na maswali kidogo hasa kwa upande wa *TRA* kwenye ukusanyaji wa mapato. Ninaomba pale upakazie macho sana, kwa sababu shughuli zimeongezeka nyingi sana, lakini bado ukusanyaji wa mapato unaonekana haupandi kwa kiwango ambacho tunakitazamia. Utakuta *TRA* wanakwambia kwamba, safari hii tumekusanya na tumepita lengo, lakini bado fedha zile hazionekani, huku chini wafanyakazi mishahara labda huwa inachelewa, fedha za maendeleo zinachelewa na *TRA* wanakwambia wamekusanya kupita malengo waliyojiwekea. Kwa hiyo, nina mashaka kidogo kwamba, huenda malengo wanayojiwekea yanakuwa ni madogo sana; naomba sana Mheshimiwa Waziri uangalie katika *angle ile*.

Naomba uangalie pia masuala ya rushwa na uadilifu kwenye Kitengo kile, kwa sababu kuna magari mengine yanakuwa yameandikwa *on transit* kumbe yanabakia palepale, kuna mchezo ambao unafanyika pale. Uangalie hata wafanyakazi wanaofanya kazi kwenye Taasisi ile; maisha yao hayalingani na mishahara wanayoipata. Kwa hiyo, naomba sana ukazie macho kwenye Kitengo kile.

Vilevile ninaomba pia niulize; katika hotuba yako sijaona fedha za *TIB*, kwa sababu Benki ya *TIB*imekuwa ni mkombozi sana kwa wawekezaji wa ndani na katika Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano, *TIB* ilitengewa kupewa kila mwaka bilioni 100. Mwaka uliopita walipokea bilioni 50, lakini kwa safari hii sijaona. Naomba unisaidie hizo fedha zipo wapi, kwa sababu hata dirisha la kilimo lipo *TIB* kwa kuwa bado Benki ya Kilimo haijawa tayari. Sasa hata fedha hizo za dirisha la kilimo nasikia zimekwisha na wakulima ni wengi, ambao wanapata msaada pale. Katika suala hilo, fedha za *TIB* kwenye dirisha la kilimo, bado zile fedha za Mpango wa Miaka Mitano ya Maendeleo wanatakiwa wapate bilioni 100 kila mwaka. Naomba uniambie kama zipo.

Mheshimiwa Waziri, naomba nizungumzie upande wa wachimbaji wadogowadogo, maana kule pia tunategemea kupata mapato mengi sana na kuondoa umaskini kwa watu. Mimi nitajikita zaidi kuzungumzia katika maeneo ya Mkoa wa Singida hasa kwenye maeneo mapya, eneo la Wilaya ya Mkarama, Ibaga, ambapo kunapatikana *copper*.

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo ndiyo waliohangai ka kule, wamekwenda mpaka wakagundua kuna *copper*, lakini matokeo yake mwaka 2010 tunaishukuru Serikali iliagiza kwamba, litengwe eneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo hasa kwenye maeneo ambayo wachimbaji wadogo tayari walishaanza na Serikali ikasikia ikatenga kama hekta 200 hivi. Matokeo yake, mwaka 2012 agizo lingine linatoka kwamba, wagawanye tena katika zile hekta 200 wawagawie wale walioomba wachimbaji wa leseni kubwa, matokeo yake wamekwenda kuwachakachua wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, ni Serikali ndiyo tunaowachonganisha wachimbaji wadogo pamoja na wawekezaji wakubwa. Matokeo yake palepale kuna wachimbaji wengine wadogo wamenyang'anywa maeneo yao yakaingizwa kwenye leseni kubwa, lakini walewale wachimbaji wengine wadogo wakaachwa ndani ya leseni kubwa; imeleta mtafaruku sana katika maeneo ya Ibaga. Mimi naiomba Serikali iende, tena ninachowaomba chondechonde kwa sababu mnapotangaza wawekezaji wadogo au wachimbaji wadogo waombe leseni, matokeo yake anakuja mtu mwagine. Mimi naona hiyo ni mianya ya rushwa na kama siyo rushwa ninaomba Serikali ije itueleze hapa, hizo hekta 200 zilizotengwa kwa ajili ya wachimbaji wadogo wa Ibaga zimekwenda wapi na nani alitoa agizo la kuwapa wenyewe leseni kubwa kwa sababu nasikia kuna mchimbaji wa leseni kubwa eti aliomba mwaka 2009, wachimbaji wadogo wameanza lini? Turudi mezani twende Ibaga tukaanze moja na kama tunampa mchimbaji mkubwa, ninaomba wachimbaji wadogo wa Ibaga waliopo kwenye eneo lile walipwe fidia halafu wapewe maeneo yanayolingana na eneo walilonyang'anywa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya machimbo ya madini mbalimbali ukizunguka utakuta kuna milima tu, udongo umetolewa milima imeoteshwala halafu ile milima imeachiwa. Mimi naomba Serikali iangalie uwezekano wa kuwabana wanaotoa udongo chini wanaotesha milima, waoteshe misitu wapande miti ili tuweze kupata mvua, tubadilishe mandhari ya nchi yetu ilimradi wametoa udongo chini. Ukienda Malaysia, utakuta wamefanya hivyo, kwenye yale mashimo wameweka namna ya kuvuna maji ya mvua na Wananchi wa maeneo yale wamekuwa wakifaidika na yale mashimo ambayo yanakuwa yanaachwa pale. Bado ile milima ambayo ni udongo pia inakuwa ni faida kwa sababu mvua za wakati zinakuwa zinakuja mara kwa mara. Ninaomba tuboreshe mazingira kwenye maeneo ya uchimbaji ili tusiache nchi yetu ikawa na sura ya ajabuajabu.

Mheshimiwa Spika, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri kwamba, Serikali imetangaza kuanza kubandika stika kwenye kazi za wasanii kuanzia tarehe moja, Serikali mmejipangia kupata mapato kutoka kwenye kazi za wasanii, lakini bado hamjaboresha ni namna gani msanii huyu atawezu kunufaika hata na hizo stika.

Ninataka kuwauliza ni wasanii wangapi wanaofahamu faida ya hizo stika? Ni wasanii wangapi wanaojua huo mpango unakuja? Ni wasanii wangapi ambao watafaidika na hizo stika? Ninaongea hivyo kwa sababu hata hapa tulipo, tukimaliza utaona *TBC* wanaweka wimbo wowote, lakini *TBC* halipi kwa kazi ile anayoitumia ya yule msanii na Serikali mpo hamjaweka utaratibu wowote wa kukusanya. Chombo cha Serikali bado nacho kinadhulumu haki za kazi za sanaa. Ninaomba vyombo vya habari vyote vinavyotumia kazi za wasanii, vilipe mrabaha lakini bado hata kwenye milio ya simu, unakaa siku mbili unaambiwa mlion wako umekatwa shilingi 400, ukikaa siku mbili tena unaambiwa mlion wako umekatwa shilingi 400, hizo pesa zinakwenda wapi? Serikali msikimbilie kuweka stika, tatueni kwanza matatizo ambayo sisi tunaibiwa kazi zetu, maharamia wamejaa kila mahali mpaka kwenye simu kuna uharamia, tunaibiwa kazi zetu. Naomba ni-*declare interest* kwamba na mimi ni msanii na ni mmoja wa wanaobiwa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ninaiomba Serikali iachane na mpango wa stika mpaka itatue suala la uharamia kuanzia kwenye vyombo vya habari, kwenye magari, kwenye simu na maeneo mengine yote wanayotumia kazi za sanaa na pia waweke dawati la kazi za sanaa zinazoibiwa. Watu wanauzwa kama njugu, hakuna anayejali na baadhi yetu tunanunua zile kazi na tunazo majumbani, hazijalipiwa ushuru, hazijaenda kwa msanii, lakini aliyepata ni yule haramia. Ninamwomba Waziri na ninaiomba Serikali, iachane na stika mpaka ihakikishe imedhibiti mianya yote ya maharamia.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia, naomba Mheshimiwa Waziri atukumbuke Singida kwenye Hospitali yetu ya Rufaa kuna fedha ambazo tumeziomba, tunaomba utusaidie kwa sababu Hospitali ile itasaidia sana Wananchi wa maeneo yale, kwa sababu ni Hospitali ya Rufaa. Tutashukuru sana kama utatukumbuka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba pia Serikali iweke kipaumbele kujenga nyumba za watumishi, kwa nini msiweke *guarantee* kwenye vyombo vyetu kama *National Housing* ili waweze kujenga nyumba za walimu, wawekee *guarantee* wana uwezo. *NSSF* na wengine wengi ili wajenge nyumba za watumishi kuanzia walimu, polisi, wauguzi na wengine wengi ambaao wanahangaika, wataweza kujenga na fedha yenu itarudi, mbona kuna watu mmewadhamini mpaka leo na bado hawajarudisha hizo fedha? Thaminini vyombo vyetu hivi ili viweze kujenga nyumba za makazi ya walimu, za askari, za madaktari na mambo mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana na sasa namwita Mheshimiwa Abia Muhamma Nyabakari!

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda nimpongeza nahodha wetu, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, pamoja na Jemedari wake, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda na Serikali yote, wale wenye mapenzi mema na nchi yao kwa kuonesha ufanisi mkubwa wa kiutendaji katika awamu hii ya nne. Mwaka jana walitenga trilioni 15 na mwaka huu wametenga trilioni 18, huo ni ushindi wa Serikali ya Jakaya Mrisho Kikwete. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaona nchi nzima sasa hivi barabara zote zinapitika, ukiangalia Mkoa hadi Mkoa, nchi hadi nchi, zimebekewe barabara za lami na hata Dar es Salaam iliyokuwa kama kichaka sasa hivi inang'ara, jamani Kikwete Oyee! Wanaowalaani na wao walaaniwe na watu wote waseme amina!

## WABUNGE FULANI: Amina!

**MHE. ABIA M. NYABAKARI:** Mheshimiwa Spika, watu watasema mambo mengi yanayowapendeza, watasema kwamba, Serikali ya Kikwete haifanyi kazi, jamani mpachikeni miguu ya chuma, mambo aliyoyafanya hakuna Rais aliye yafanya katika kipindi chote kilichopita, barabara zili kuwa hazipitiki, kila mambo yalikuwa hivyo, baba anakimbia mpaka ulimi unataka kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni kweli watu watasema hivyo, lakini tutamkumbuka kama maji yaliyokwisha kupita na si hivyo tu, Wabunge wengine wanataka kulichukua sega la asali, wametazamia kuliangalia wala hawaoni maporomoko na matokeo yake kwa nguvu hata wanawaandamanisha watu ili wapate kulichukua hilo sega, lakini hatuwakatalii maana hata Biblia inasema, mpumbavu hata umtwange kinuni upumbavu wake hauwezi kumtoka!

Mheshimiwa Spika, Mfalme aliyeketi katika kitici cha hukumu huyapepe ta mabaya yote kwa macho yake na ulimi wa Mfalme aliye na hekima hunena maarifa vizuri, maana mwanadamu mwenye busara husitiri maarifa, bali vinywa vya wapumbavu humwaga upumbavu wala hawana maarifa ya kuzuia maneno yaletayo madhara.

Mheshimiwa Spika, naweza kusema sana, lakini nataka kwanza nijikite, Serikali yetu inafanya kazi kulingana na wakati, kama maendeleo haya yangeanzia nyuma, sasa hivi tungekuwa mbali mambo aliyoyafanya Mheshimiwa Jakaya Kikwete. Katika Mkoa wa Rukwa, naweza kusema jamani gari la wagonjwa katika Manispaa hatuna, je, katika bajeti hii mtatukumbuka? Na si hivyo tu, vifaa vya wapima ardhi katika Wilaya ya Nkasi hakuna, wanalazimika kwenda kuchukua Sumbawanga Mjini ndiyo warudi Nkasi watembee kwa miguu hata pikipiki hawana, tunaomba na kule ni karibu na hifadhi za wanyama. Si hivyo tu, barabara za lami katika Manispaa ya Sumbawanga tuna kilomita 5.8, jamani mtoto akizaliwa leo baba kamjengea ghorofa, ukaona anapewa nyumba, lazima utajisikia vibaya; Mkoa wa Katavi una barabara zaidi ya kilomita

16 nao umezaliwa jana tu. Si hivyo tu, umeme unawaka mpaka vijijini, sasa sisi tunajuliza kulikoni huyu mtoto yeye mbona anakimbia na Mwalimu Nyerere alisema binadamu wote ni sawa na Afrika ni moja. Biblia inasema amdharauye mwenzake afanya dhambi. Tunaomba na sisi mtusitiri!

Si hivyo tu, kabla ya utawala huu wa nne jamani tunawaombeni barabara ya Mpanda kwenda Kigoma, Barabara ya Nyakanazi kwenda Kigoma, msiache kutuwekea lami, tunataka tuwe tunapepea na sisi, kabla ya utawala huu maana kila utawala unabadilisha mambo yake.

Tunaomba pia muwaangalie madreva wa Wabunge na tunamshukuru yule mama aliyeweka mama ntilie pale, wanakula mihogo asubuhi, mchana mihogo. Tunaomba muwafikirie muwakumbuke katika bajeti yenu.

Mheshimiwa Spika, hodihodi imeingia Mkoa wa Rukwa iliyotoka huko Lusaba Kigoma, walimu wanajilli wanafunzi bila utaratibu. Sasa mimi najuliza; *RASHana* habari na mambo haya wala Afisa Elimu wa Wilaya hana habari na jambo hili? Je, wakaguzi wanaweza kukaa zaidi ya miaka mitatu bila kwenda kukagua shule wakaona matatizo haya? Je, Afisa Elimu wa Mkoa hajui hiki kitu? Kule Sopa yamepiga hodi, Kalambo na Kipeta. Tunaomba Wanarukwa, mkiona mtu anatoa nafasi za wanafunzi bure, huyo mwalimu mfungisheni milango siku hiyohiyo.

Mheshimiwa Spika, naweza kusema mengi lakini nasema hivi, watu wanaidharau sana hii Serikali ya Awamu ya Nne. Napenda niseme kwamba, afadhali Rais wetu Jakaya Kikwete, anayedharaulika ikiwa na watumwa, ikiwa na nini jamani; ikiwa na watumwa. Ajisifuye ikiwa hana kitu tunasema kwamba huyo ni sawa na pete ya dhahabu kwenye pua ya nguruwe! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, watu wanaandamanishwa kila kukicha, watu wanataka kulichukua hilo sega tu, wametazamia wanaangalia hilo sega. Someni jamani Biblia, kuna maandamano na ambayo hayakuwa maandamano.

Biblia inasema hivi; usiandamane na mikutano kutenda uovu wala usitie ushahidi katika neno lolote, wala kwa kugeuka kando na kuandamana na mikutano na kutoa hukumu. Watu wanaandamana, wanachoma majumba, barabara, magari, hayo siyo maandamano ya amani! Lazima tuseme, someni Biblia jamani, Biblia inasema kama mnataka kuyatoa mamlaka kwenye madaraka yapigieni kura maana ndiyo hukumu ya wakuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba wote mlioko ndani ya nyumba hii muandike fungu moja, Waembrania 13:17, inasema hivi: "Watiini wenyе kuwaongoza na kuwanyenyеkeea kwa maana wao wanakesha kwa ajili ya roho zenu kama watu watakaotoa hesabu kwamba wafanye hivyo si kwa kuugua, maana isingewafaa ninyi." (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tuzitoe mamlaka madarakani kwa kupiga kura, siyo kwa maandamano. Serikali hata ikitenda kile kizuri, watu hawawezi kusifia. Huu jamani ni uovu. Biblia hiyo inasema; usimtukane mkuu wa watu wako na kumdharaun na kuyadharau mamlaka. Nasema hivi, watu wanaodharau utawala huu wa Awamu ya Nne, wafedheheshwe, waaibike na mwaka 2015 wavikwe aibu na njia zao zikawe giza na utelezi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mungu alisema na nimeshasema Mfalme mwenye busara huyapepete mambo mabaya na mema kwa macho yake. Hivyo ni lazima mfalme mwenye hekima atumie busara. Pia Mungu alisema; mchague kwani kuna laana na mabaya na kuna uzima na mauti. Watu tumeamua kuchagua mauti, kwa nini? Ni kwa ajili ya uchu wa watu wachache.

Mheshimiwa Spika, Serikali hii inafanya kazi kama kifaru. Mwaka jana nilisema sana na nimekuwa nikisema, lakini jamani naombeni mtukumbuke watu wa Rukwa, Walimu wanaokaa pembezoni muwapatie *first priority* ya kwenda kusoma badala ya kuwapatia watu wa Mjini. Katika bajeti zenu hiso, watu wa mjini tu ndiyo wanaopewa upendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana watu wa Rukwa watukumbuke. Si hivyo tu, katika bajeti zenu mnazotenga mkumbuke kwamba kuna Walimu wanatoka Kipeta, Legezamwendo na wengine mbali sana kufuata mishahara huku wakitumia karibu mshahara wao wote. Kwa hiyo, naomba muwakumbuke. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:**Wanasemahivi, umewafumbuamachonikuongezee dakika, lakini sikupi. (*Kicheko*)

Nimwite Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, halafu Mheshimiwa Anne Kilango atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, kule kwetu kuna usemi mmoja Wapemba wanasesma: "Muangushaji wa nazi yake ni moja tu", hata akiangusha nazi mia basi yake ni moja. Akitaka kusaidiwa na mwenye nazi, basi pengine atasaidiwa dafu." (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema hili kwa sababu moja, Mheshimiwa Mchuchuli amesema hapa kwamba, vijana wale ambao wanaoendesha bodaboda Serikali imewafutia kodi za mapato. Niseme kwamba, bodaboda zile si za vijana wale, wamiliki wake ni matajiri. Kwa hivyo, vijana wa bodaboda wanachokipata ni ile ile nazi moja pengine na dafu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la pili niseme juu ya suala la miundombinu ya barabara. Mara nyingi Serikali inatenga fedha kidogo kwa ajili ya maendeleo ya barabara, jambo ambalo mara nyingi linasababisha ile miradi ambayo imeamuliwa kutomalizika kwa wakati na pengine kutotekelizwa kabisa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano hai, kuna barabara inayotoka Mzambarauni Takao – Pandani – Bahareni – Finya – Kinazini – Wingwi. Nishukuru kwamba, barabara hii iko katika

kiwango cha kuwekewa lami na tunatarajia hivi karibuni itamalizika. Hata hivyo, kuna waathirika ambao wamepitiwa na barabara hii wako katika maeneo ya Bahareni, Finya, Rui na Kinazini.

Mheshimiwa Spika, barabara hii niya *Millennium Challenge*, kwa hivyo, imo kwenye Muungano. Naomba wale waathirika wafikiriwe haraka iwezekanavyo. Ingawa wapo ambao walilipwa, lakini wapo pia ambao sasa hivi wanahifadhiwa na majirani kwa sababu hawana pa kukaa, licha ya ukweli kwamba fedha zimetolewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ni malengo ya Milenia juu ya kupunguza vifo vya watoto. Hili katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, naona halikupewa kipaumbele kinachostahiki. Nasema hivyo kwa sababu toka mwaka 2004 hadi 2010, Tanzania imepunguza vifo vya watoto kwa asilimia 5.3 wakati Senegal wamefikia asilimia 9.9, Rwanda asilimia 9.6 na jirani zetu wa Kenya wako katika asilimia 8.4.

Mheshimiwa Spika, teknolojia ya kuondoa vifo vya watoto na akinamama wajawazito haihitajigharama kubwa. Serikali ina wajibu wa kuhakikisha kwamba, watoto wetu chini ya umri wa mwaka mmoja hadi miaka mitano (1-5) pamoja na akinamama wajawazito, wamepatiwa vyandarua vilivyowekewa dawa ya kuzuia mbu. Vilevile, akinamama pamoja na watoto wanahitaji kuwa na lishe bora, kupata matibabu bora, hivyo hospitali zetu zina wajibu wa kuboreshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ili kupunguza vifo vya akinamama wajawazito pamoja na watoto, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ina wajibu wa kuhakikisha kwamba, ina uwezo wa kuwapatia vyandarua akina mama wajawazito na watoto wote walioko Tanzania. Nina hakika hili litakapotendeka tutaweza kupunguza vifo vya watoto na akinamama wajawazito kwa karibu theluthi mbili (2/3) ya Watanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vile vile Mheshimiwa Kuruthum Mchuchuli alisema kwamba, mwaka huu wa 2013/2014, Serikali yetu inategemea misaada ya nje ilipie asilimia 21.1

na tukichanganya pamoja na mikopo ya kibiashara tutafikia asilimia 30.4.

Mheshimiwa Spika, vile vile tukumbuke kwamba nchi nydingi wahisani wameondoa kwa kiwango kikubwa misaada yao kwa Tanzania na wengine wamefikia hatua ya kutotoa kabisa. Sasa wao wanachokitoa ni *figure*, lakini kutoa msaada kama huu ili uwasaidie Watanzania, hawatoi. Sasa ninaloomba ni kwamba, Watanzania tujitahidi kuwaiga wenzetu wa Kenya ili tuweze kujitegemea wenyewe, tusitegemee misaada kutoka nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile tuna wajibu wa kutunza kile ambacho tumekipata ndani ya nchi yetu, kwa sababu kilichofanya baadhi ya hawa wahisani wazuie kuleta misaada kwetu, wanasema tuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Sasa ni lazima tufikirie kuwa na vyanzo vipyta vya mapato ndani ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kusema tunazidisha ushuru kwenye bia na sigara ilituweze kupata mapato, naona limepitwa na wakati kabisa. Vile vile suala la kuongeza gharama ya dizeli na *petrol*, hatujamsaidia mwananchi wa chini. Tuangalie gharama ya ufikishaji wa haya mafuta ya taa vijijini, ikiwa petrol na dizeli ziko juu mwananchi wa chini atayapataje haya mafuta ya taa? Je, bei ya mafuta ya taa itakuwaje? (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kombo. Mheshimiwa Anne Kilango atafuatiwa na Mheshimiwa Albert Ntabaliba na kisha atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa dhatikabisa kwa ubunifu mkubwa ulioufanya wa kuleta huu mfumo mpya wa kuwasilisha bajeti ya Serikali. Nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote tumeona kwamba, huenda huu ukatubadilishia hali halisi ya bajeti ya Serikali. Kwa kweli tunakupa pongezi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nipeleke pongezi kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwamba, imeonesha kuwajali wananchi wa vijijini kwa kiasi kikubwa. Baada ya Wabunge kutoa mawazo yetu Serikali ikaona iongeze fedha kwenye zile Wizara ambazo zinagusa wananchi wa vijijini moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kuna Wizara ya Maji kwenye miradi ya maji salama vijijini imeongezewa shilingi bilioni 84.5, Wizara ya Nishati na Madini, upande wa Nishati Vijijini (*REA*) tumeongezewa shilingi bilioni 186, tunaishukuru Serikali. Wizara ya Kilimo ambako huko ndiko ambako karibu asilimia 80 ya wananchi wanategemea, imeongezewa shilingi bilioni 21.15. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba nitoe angalizo na hapa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha naomba anisikilize, isije ikawa inaishia kwenye kuongezewa kinadharia. Fedha hizi kweli ziende zifanye kazi na tuone matunda kwenye miradi ya vijijini. Tuone miradi ya maji salama ambavyo inawakomboa wananchi maskini vijijini. Tuone namna ambavyo hivi vijiji vyote vimetengewa fedha kwenye kuunganishwa na nishati ya umeme na tuone kweli kukiwa na mabadiliko kwenye kilimo.

Mheshimiwa Spika, tumepiga kelele sana mpaka hizi fedha zikaongezwa. Sasa kupitia Bunge hili nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, nilimpelekea maombi ya kuboresha *scheme* ya umwagiliaji Ndungu, kwamba inahitaji kufanyiwa ukarabati. Fedha zinazohitajika siyo nyingi, ni sh. 32,000,880/=. Naomba niseme kwamba, nitakuwa mkali kama fedha hizi hazitafika kwenye mradi wangu wa umwagiliaji wa Ndungu, kwa sababu tumesaidia mpaka hizi fedha zikaongezwa, naomba na sisi atusaidie.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba niongee udhaifu wa mapato. Kwa kweli katika nchi yetu tusingepaswa tuwe tegemezikama Serikaliingekuwa makinihaswa katika kukusanya

mapato. Kuna mianya mingi mno ya mapato ya Serikali inavuja na fedha nyingi sana zinapotea. Naomba nitoe mfano kwenye madini, kwenye madini tunapoteza pato kubwa sana la Serikali. Kwanza, linapotelea kwenye mikataba mibovu ambayo haina tija wala manufaa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, pili ni utoroshaji wa madini kwenda nje ambao aliyeugundua ni *TMAA*, Taasisi iliyo chini ya Wizara ya Nishati na Madini. Ndani ya miezi mitano tu kuanzia Oktoba 2012 mpaka Aprili, 2013 waliweza kukamata madini yaliyokuwa yanatoroshwa nje kupitia viwanja vya ndege vitatu vya Kilimanjaro, Dar es Salaam na Mwanza, yenye thamani ya shilingi bilioni 13.2. Hii ilikuwa ni ndani ya miezi mitano tu. Kwa hiyo, inaonesha kwamba mapato ya nchi yetu mengi sana yanakwenda nje ya nchi kwa sababu Serikali haiko makini katika kulinda mapato yetu.

Mheshimiwa Spika, ukija kuangalia kwenye migodi mikubwa, pia hatukusanyi mapato vizuri. Kuna *document* hapa ambayo nitaomba kuiweka mezani ili imfikie Mheshimiwa Waziri wa Fedha aone ni kiasi gani *TMAA* wanafanya kazi ya kulinda mapato ya nchi hii kupitia madini, lakini wanahitaji kuwezeshwa ili wafanye kazi nzuri zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tukienda kwenye ulinzi hafifu katika bandari ya Dar es Salaam. Bandari hii ni lango kubwa sana na hakuna ulinzi kamili katika bandari hii ambao unalinda mapato ya nchi hii; makontena mengi yanapitisha vitu ambavyo sivyo, mambo yanafanyika kienyeji na Serikali pale ndipo kuliko na mapato mengi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali sasa kufuatana na hii *document* ambayo nitaiweka mezani, hebu iwawezeshe *TMAA* wafungue kitengo kikubwa pale, waweze kulinda na kuangalia kama wanavyoangalia kwenye viwanja vya ndege, huenda tukaokoa mapato ya nchi hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye kazi. Kuna tatizo ambalo hatujaliangalia kwa undani. Tuanzie kwenye Serikali Kuu kwa wenzetu Mawaziri wote na tuje kwa sisi Wabunge wote tulioko humu ndani, kama kweli wote hapa ndani ambao ndiyo tunaojenga nchi hii, kama kila mtu kwa nafasi yake, kila Waziri kwenye nafasi yake, kila Mbunge kwenye nafasi yake, wote kama tungefanya kazi ipasavyo hii nchi isingekuwa na hali hii.

Mheshimiwa Spika, kwa nini nasema hivyo? Ulinipa nafasi nikaenda Malaysia, nilijisikia vibaya sana kwani nilipokwenda kule na wale tuliokwenda nao ni mashahidi wangu, tuliikuta nchi ya Malaysia asilimia 68 ya uchumi wake unategemea zao la michikichi, mafuta ya mawese. Nikawauliza jamani hizi mbegu za michikichi mmezitoa wapi? Wakaniambia Kigoma. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, mbegu imetoka Kigoma, Tanzania, Malyasia wanaolima michikichi ile waliyochukua mbegu Kigoma wao sasa hivi asilimia 68 ya uchumi ni michikichi, mafuta ya mawese. Ina maana wenzetu wanafanya kazi vizuri, sisi tuko wapi ambao tumetoa mbegu? (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, sasa nirudi kwenye Wizara ya Mheshimiwa Mary Nagu, kuhusiana na uwekezaji usio na manufaa kwa Taifa. Kuna uwezekaji ambao hauna mapato yoyote kwa nchi hii. Mashamba mengi sana kwenye nchi hii, wawekezaji wamechukua ardhi wanasesma wanalima mikonge, lakini hakuna zao lolote la katani, wamehodhi ardhi ile, wananchi hawana ardhi ya kulima na kujenga nyumba.

Mheshimiwa Spika, nikikupeleka kwenye Kata yangu moja inaitwa Ndungu mpaka Mroyo yaani utalia, ardhi yote amepewa mwekezaji ambaye halimi Katani wala mkonge, ni vurugu mechii na wananchi hawana ardhi.

Mheshimiwa Spika, naomba wakati Mheshimiwa Waziri anahitimisha, haya mambo yangu yote yajibiwe, lakini hii ardhi ya Kata ya Ndungu hebu Mheshimiwa Waziri Mary Nagu aende, nataka ile ardhi irudi kwa wananchi wangu ambao wana shida.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naomba kuunga mkono hoja. (*Makof*)

**SPIKA:** Haya. Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba atafuatiwa na Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kunipa fursa hii nami niweze kuongea machache kwenye bajeti hii. Kwanza kabisa, naunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambazo imezonesha kwenye bajeti hii. Tuna miaka miwili na nusu sasa tumehudhuria bajeti hizi, lakini bajeti hii imekuja na mtazamo mpya na mambo yanakwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameweza kuongeza fedha kwenye maji kama tulivyoona wote. Umeme Vijijini na vijiji vyetu vimo, akinamama wameongezewa fedha, vijana wamepata fedha, ruzuku kwenye kilimo imekuwa nzuri sasa tunataka bajeti ya namna gani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile tujue tulipokuwa tunataka fedha ziongezeke, tulikuwa tunajua kwamba, lazima Serikali itafute vyanzo vya kutafuta fedha na ni lazima kodi fulani fulani zituumize ili tuweze kutimiza mengine, ni *give and take*, kwa hiyo lazima zifike mahali sio kulalamika tu kwamba kodi imeongezeka, lazima tujue sisi ndio tulikuwa tunadai fedha ziongezeke kwenye sehemu za Wizara fulani. Kwa hiyo, sio utamaduni mzuri wa kukaa unalalamika kila wakati na huku ndio sisi tuliokuwa tunaomba fedha.

Mheshimiwa Spika, kuna wajumbe wengine wamesema kwamba, misamaha ya bodaboda inatajirisha matajiri. Tanzania hii tatizo tulilonalo hatujazalisha matajiri wengi, lazima nchi hii iwe na matajiri wengi waweze kuajiri watu wengi. Kwa hiyo, kwa msamaha huo matajiri watakuwa na uwezo wa kununua bodaboda nyingi, wataajiri vijana wetu, nafikiri ndionia ya Serikali ya kufanya hilo. Kwa sababu wako wawekezaji wanaotoka nje,

wanapewa misamaha, sasa matajiri wa Tanzania wakipewa msamaha, tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha ametuambia deni la Taifa linahimilika na kama linahimilika kwa nini asikope fedha nyingi sana tukamaliza matatizo ya vijijini kwa Walimu, kwa nini asikope fedha nyingi tukajenga nyumba kwa mkupuo nchi nzima, kwa nini hataki kumaliza haya matatizo. Ningeomba uendelee kukopa na mwanamume yejote asiyedaiwa huyo sio mwanamume.

**SPIKA:** Ina maana wanawake hawastahili kukopa?  
(*Makof/ Kicheko*)

Haya endelea!

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, pia nchi isiyodaiwa hiyo sio nchi.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu bado lina malalamiko mawili. Lalamiko la kwanza, ni fidia ambayo haijafanywa na Wizara ya Ujenzi kwenye barabara ile ya Manyovu; kulikuwa na vibanda karibu 120 vilivunjwa kupisha ujenzi, lakini wakawa wamewaambia kwamba, wangeweza kuwalipa na walikuwa wameingia mkataba na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Waziri wa Fedha aliangalie hilo na kwenye bajeti hii aanze kufikiria namna ya kuwalipa wale wananchi, wanapiga kelele kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, wakulima wangu wa kahawa waliotapeliwa. Nalisema hili kila siku ili Serikali iweze kuangalia namna ya kuwafidia hawa wakulima ili waweze kuendelea kulima kahawa zao. Hili suala tumeliweka kwenye Wizara, nina imani Serikali italiangalia.

Mheshimiwa Spika, ombi linguine, kwenye hotuba tumeonesha kwamba, tunajenga masoko ya mipakani, sasa kule kwangu kuna masoko matatu yanayojengwa ya mipakani. Tunachoomba ni namna gani fedha za kujenga madaraja sasa

kuvuka kwenda Burundi tunaweza tukapata fedha za kujenga madaraja. Kwa hiyo, ni ombi kwamba, haya madaraja nayo tuanze kuyaangalia namna ya kuvuka Burundi ili yale masoko ya Kimataifa yaweze kuwa na maana zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, fedha za rada naona mnachelewesha kununua hivyo vitabu, mnachelewesha kununua madawati, mnafurahia tu *interest* za kwenye benki, watoto wetu wanakaa chini. Ni ombi langu kwamba tulifanye haraka.

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema mengi kwa sababu tumeanza kuchangia Wizara hizi kuanzia Wizara moja mpaka sasa, kwa hiyo, huu si muda wa kuwa na mambo mengi, bali ni muda wa kuipongeza Serikali na Chama cha Mapinduzi. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante nashukuru. Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa atafutiwa na Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir na Mheshimiwa Gosbert Blandes ajiandae.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti hii kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba nikushukuru wewe binafsi pamoja na Serikali kwa kuamua kuleta mtindo mpya wa bajeti, *budget circle* ambayo sisi Wabunge tunashiriki moja kwa moja katika kuhakikisha ni sehemu katika bajeti. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma kulikuwa kuna malalamiko kwamba, sisi Wabunge ni *rubber stamp*, lakini sasa hivi sivyo kwa sababu sisi tumekuwa sehemu ya bajeti, tumetoa mawazo yetu na Serikali imetusikiliza na imetukubalia, naomba niishukuru sana Serikali kwa hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mtovu wa fadhila nisipomshukuru Waziri wa Fedha pamoja na Manaibu wake ambao wamekubali kwa dhati kabisa kuyatupia macho

maeneo muhimu kama maji, umeme, barabara, elimu pamoja na maeneo mengine ambayo ni muhimu kwa ajili ya uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Bajeti hii imewalenga zaidi wanyonge kwa sababu huu umeme unapelekwa vijijini kwa wingi zaidi na haya maji yanapelekwa vijijini kwa wingizaidina hii miundombinu imewekwa kwa ajili ya kuwasaidia watu wa chini zaidi.

Mheshimiwa Spika, nataka kuzungumzia hasa hasa katika eneo la mapato. Tunapozungumzia bajeti, bajeti ina mambo makubwa mawili; la kwanza mapato na eneo la pili ni matumizi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu inategemea sana mapato kutoka kwenye kodi, tunategemea kupata karibu shilingi triliioni 10 kutoka kwenye kodi. Lakini kwenye eneo hili kama Serikali itajipanga vizuri, tunaweza tukapata fedha nyingi zaidi kuliko hizo shilingi triliioni 10.

Mheshimiwa Spika, katikaanchihiituna Watanzania takribani milioni 44. Lakini watu ambao wanalipa kodi ni 1,000,600,000. Ukiangalia kitakwimu walipa kodi ni wachache sana na wa-*big tax fares* wanafika laki nne tu. Kama Serikali itajipanga vizuri watu wote wakalipa kodi na wale ambao katika sekta ambazo sio rasmi, nina hakika eneo la kodi katika eneo hili litaongezeka na hatutakuwa tena tegemezi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika shilingi bilioni 44 kama Watanzania watalipa shilingi bilioni 10 ambayo ni asilimia 25, tunaweza kuongeza zaidi ya shilingi triliioni tatu katika kodi hizi, tutakuwa tumepiga hatua zaidi kuliko hapa tulipo.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, ninalotaka kulizungumzia kwenye mapato ni eneo ambayo inatokana na vyanzo vingine. Katika bajeti hii ya safari hii eneo linalotokana na vyanzo vingine ni shilingi bilioni 741. Hesabu hizi ni ndogo, tuna Wizara nyingi za kutosha, lakini kila Wizara inaonekana ni Wizara ambayo inataka ku-*consume* tu, hakuna Wizara hata moja iliyosema mkitupa shilingi bilioni 300 tutaleta shilingi bilioni 600.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya nchi duniani zinaishi kwa umeme, kuna baadhi ya nchi duniani zinaishi kwa utalii na kuna baadhi ya nchi zinaishi kwa bandari, lakini Wizara zetu zinashangaza sana hapa, kila Wizara inataka ipewe fedha kwa ajili ya kutumia tu. Waje na mikakati juu ya meza, watuneshe tukiwapa fedha kiasi gani, watatupa kiasi gani. Naomba tuliangalie sana eneo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalonataka kuchangia ni uwazi katika ulipaji wa kodi. Hili ni eneo muhimu sana hapa hakuna uwazi. Kwa mfano, tumeweza kubinafsisha katika nchi hii zaidi ya Makampuni 300, lakini tujiulize ni Makampuni mangapi yamekwenda kwenye Dar es Salaam *Stock of Exchange* ambao wameziweka *share* zao wazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kadri ya uwezo wake kuhakikisha inatoa *incentives* kwenye eneo hili, lakini watu hawataki kwenda kwenye eneo hili wanaogopa nini. Sasa nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri wa Fedha, sheria ilishatungwa na kanuni zilitakiwa zianze kufanya kazi zaidi ya miaka minne iliyopita, lakini hazifanyi kazi, tunaomba tuhakikishe Makampuni mengi yaliyobinafsisha yanakwenda kwenye Dar es Salaam *Stock of Exchange*.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kama Makampuni yanakwenda kwenye Dar es Salaam *Stock of Exchange* sasa hivi tuna *TBL* ambayo sisi Serikali tuna-*own* asilimia nne, lakini tunapata kodi pale na tunapata *dividend*. *AIRTEL* tuna-*own* asilimia 40, lakini hatupati kodi wala hatupati *dividend*.

Mheshimiwa Spika, sasa tuiombe Serikali, sehemu ambapo Serikali tuna *share* kwenye hayo Makampuni tuyapeleke kwenye Dar es Salaam *Stock of Exchange* na *automatically* zile *share* zingine za Makampuni hayo zitalazimika zipeleke kwenye Dar es Salaam *Stock of Exchange*.

Mheshimiwa Spika, eneo ninalotaka kuchangia lingine ni eneo la mfumuko wa bei. Mheshimiwa Waziri amezungumza vizuri kwamba, mfumuko wa bei umeshuka ulianza kutoka kwenye asilimia 16 mpaka sasa hivi tunazungumzia asilimia 8.3,

ni kweli umeshuka. Lakini tuangalie kabla hatujazungumzia suala hili kwa sababu nimeona Mheshimiwa Waziri na timu yake wanaangalia upande mmoja, tuangalie kwa kina *factor zipi ambazo zinasababisha mfumuko wa bei.*

Mheshimiwa Spika, kuna *factor za aina mbili pale*; kuna *demand pool inflation* na *cost pushing inflation*. Lakini naona Mheshimiwa Waziri wame-concentrate sana kwenye *demand pool inflation*. *Solution* inaonekana kwenye *demand pool inflation*. Lakini kama tungekwenda kwenye *cost pushing inflation* nina hakika kabisa *inflation rate* ingeshuka zaidi ya hapa ilipo. Kwa mfano, gharama za usafirishaji kwenye barabara ni kubwa sana, lakini tungejikita kwa kuhakikisha tunapata *infrastructure* ya reli iliyokuwa nzuri, *automatic* gharama za usafirishaji zingepungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, gharama za umeme sasa hivi ni kubwa, lakini tuna vyanzo vingi sana vya umeme hapa nchini. Sasa sisi tume-concentrate na kununua tu mafuta. Mafuta *unit* moja yanauzwa senti 44, lakini tukienda kwenye gharama za umeme kama umeme wa upepo, umeme wa makaa ya mawe, umeme wa maji tunauza kwa senti saba mpaka senti 10. Kwa hiyo *automatically, production cost* kwenye eneo hili ingeshuka na hapo hapo *inflation rate* ingeshuka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni suala la ukuaji wa uchumi. Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba, ukuaji wa uchumi umekua. Ni kweli uchumi wetu umekua, lakini tunatakiwa tuangalie, je, ukuaji wa uchumi huu unakwenda sambamba na hali halisi za Watanzania?

Mheshimiwa Spika, maana yake tuliangalie sio tunasema uchumi umekua, lakini tuna Watanzania wengine walio maskini zaidi na maskini wa kati na walalahoi. Tunapozungumzia ukuaji wa uchumi tuangalie na makundi haya tunawatoa kutoka kwenye umaskini wa chini, unawapeleka kwenye *level fulani*,

unapunguza *gap*, lakini kama Serikali itadhamiria kwa dhati kushirikiana na taasisi kwa maana ya sekta binafsi, nina hakika kabisa hali ya Mtanzania itakuwa katika hali nzuri na maisha bora kwa kila Mtanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni eneo la viwanda, hakuna nchi yoyote duniani ambayo iliwahi kuendelea bila ya kuwekeza katika maeneo ya viwanda. Kama Serikali yetu itaamua kwa dhati kuwekeza katika yale maeneo ambayo sasa hivi Wizara ya Viwanda na Biashara imeyapigia kelele, kwa mfano, kutengeneza *logistics hubs* pale Kurasini na EPZ kule Bagamoyo, nina hakika kabisa tutatengeneza ajira nyingi.

Mheshimiwa Spika, pale Kurasini sisi kama Watanzania tunatakiwa tutoe mchango wa shilingi bilioni 60 na Wachina ambao wanataka kuingia kwenye huo mradi wako tayari kutoa shilingi bilioni 600 ambayo ni *proportion* ya *one to ten*. Serikali msisite kwenye jambo hili lita-*create employment* ya watu zaidi ya 25,000 katika nchi hii na nchi zote katika *east and central Africa* zitakuwa hazina *logistics centre* kama hii, zitaitegemea hii *logistics centre* Kurasini pale ilipo. Kwa namna moja au nyingine tutakuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, natamka tena na namwomba ndugu yangu, tunakuunga mkono kwenye bajeti hii, fedha zitoke, ziende zikafanye kazi kwa wananchi. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Al-Shaymaa Kwegyir atafuatiwa na Mheshimiwa Gosbert Blandes, halafu watafuata Mheshimiwa Dustan Kitandula na Mheshimiwa Haroub Shamis.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, ahsante, sikutegemea kuipata hii nafasi, lakini nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa nakupongeza kwa kazi nzuri unayoifanya. Huko nilikokuwa nilikuwa naangalia kupitia luninga, hongera sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitajikita kwenye eneo ninaloliwakilisha, watu wenyе ulemavu, yaani hilo suala kila nitakaposimama nitalenga hapo hapo. Watu wenyе ulemavu ni kundi ambalo linasahaulika kwa wakati mwingi. Waziri wa Fedha Mheshimiwa Mgimwa nampongeza, lakini sikusikia akizungumzia kabisa watu wenyе ulemavu, hakuwataja.

Mheshimiwa Spika, watu wenyе ulemavu wana matatizo, nimezunguka katika mikoa kutokanana kaziniliyokuwanayosasa hivi ya kukusanya maoni ya Katiba. Watu wenyе ulemavu wana hali ngumu, nimepita kwenye vijiji. Tunapokwenda kukusanya maoni watu wenyе ulemavu wanakuja wanatambaa, haja yao waje watoe maoni, wazungumzie Katiba yao, lakini wanakuja wanatambaa.

Mheshimiwa Spika, kuna eneo nilikwenda Mafia mlemavu ametoka kilomita nane ametembea kwa miguu, alikuwa haoni amefanya kushikwa mkono, amesema mpaka nifike hapo kwenye maoni na mimi nikaseme. Nilipitia pia Kisarawe kuna mlemavu hivyo hivyo asiyeona ametembea kilomita nane au tisa anasema mimi nifike hapo wanapokusanya maoni na mimi nikatoe maoni yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa basi nitaanza na viziwi. Hawa watu wenyе ulemavu wa uziwi wana tatizo la kukosa habari, hawapati *information*. Angalau basi Serikali ingeweza kuwapa hawa *TBC*, maana yake hii ndiyo *TV* ya Taifa wangewapatia fedha waweze kuweka mkalimani wa lugha ya alama na wao wapate habari. Kwa sababu hawajui kinachoendelea kwenye nchi yao, basi Serikali itoe fedha wapewe hawa *TBC*. Nafikiri kwenye Wizara ya Habari na nilishaongea na Naibu Waziri analijua hilo.

Mheshimiwa Spika, nimeshazungumza naye kuhusiana na suala la lugha ya alama akasema kwanza tatizo ni fedha, sasa hizi fedha tatizo lake linatokea wapi? Kwa sababu utakuta bajeti inafika mwisho, fedha zinabaki, zinarudishwa Hazina. Hizi fedha zinarudi Hazina kwa nini, si bora ziende basi kwa hawa watu wenyе ulemavu zikawasaidie, haya mabaki mabaki wapelekewe wao, wana matatizo mengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nitoke hapo kwa viziwi maana yake nimeona nianze na viziwi, niende kuongelea alama za barabarani. Suala la alama za barabarani nimeshalizungumzia ndani ya Bunge humu mara kadhaa, mara moja, mbili na mara tatu. Watu wenyе ulemavu barabarani wanagongwa na magari.

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi wa kijana mmoja ana ulemavu wa ngozi anaitwa Mccheka, amevunjwa mguu, alikuwa anavuka barabara, pikipiki lilikotokea, limemvunja mguu yule kijana, yeye ana huoni hafifu, sasa kungekuwa na alama inayoonesha kwamba, watu wenyе huoni hafifu wanapita, yule mwenye pikipiki angepunguza mwendo, lakini sasa amegongwa na amevunjwa mguu hali yake *dhofu-l-hali*. Mimi binafsi ndio nimhudumie yule kijana, aende hospitali na inabidi aende kwa teksi, atatembea vipi wakati hana uwezo na nitahudumia wangapi na nitaweza wapi maana wengi ni *dhofu-l-hali*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimezunguka hii nchi nimekuta watu wenyе ulemavu huko Ndogosi, Mkoa wa Ruvuma, Mheshimiwa Jenista anajua Ndogosi ni wapi. Ruvuma nimekwenda wako watu wenyе ulemavu wa ngozi, wale wanatakiwa wapate madawa *sunscreen lotions* zipatikane, zinunuliwe na zisitozwe ushuru, lakini *sunscreen lotions* zinakuja bandarini, zinakaa mpaka zina-expire kwa sababu ushuru ni mkubwa. Nani atakuwa na uwezo wa kununua *sunspring lotions* kwa shilingi 20,000 au 30,000, hakuna mwenye uwezo, wengi ni *dhofu-l-hali* hawana kitu, hiyo ndiyo hali halisi na halikutajwa kabisa hili kundi.

Mheshimiwa Spika, niingie kwenye kesi za mauaji ya walemavu wa ngozi, juzi tulikuwa kwenye semina hapa ya APNAC, alikuwepo Jaji Kiongozi nilizungumza naye kuhusu hizi kesi akasema, Mheshimiwa hakuna pesa, kesi haziwezi kuendelea. Sasa hizi kesi haziwezi kuendelea, ina maana *Albino* tuendelee kuchinjwa? Kwa sababu kesi haziendelei

wale wauaji wataendelea kwenda kwenye vichaka, maana wengi wanakaa maeneo ya mbalimbali, waendelee kwenda kule na waendelee kuua kwa sababu wanajua hata tukiua hakutakuwa na kesi, maana hakuna hela ya kuendesha hizi kesi.

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kuchinjwa mpaka lini na kukatwa mikono na miguu? Nimeona nilifikishe hili lipate kusikika, nimeshaliongea sana lakini sitochoka, nitaendelea kuongea mpaka mwisho wa uhai wangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niongelee suala la ushuru wa magari; watu wenye ulemavu wana vifaa vyao vingi vinavyolipiwa ushuru kuna aina tofauti za magari kwa ajili ya watu wenye ulemavu, watu wenye matatizo ya ulemavu wa miguu, wana magari yao, wenye matatizo ya mikono wana magari ambayo inawezekana kuletwa hapa nchini, yako nje, lakini ushuru watu hawana uwezo.

Mheshimiwa Spika, wasamehewe ushuru, kutolewe msamaha, wasilipe ushuru. Hivi vyombo vyaa magari viletwe nchini watu wenye ulemavu wasitozwe ushuru, vipo vingi kuna *braille machine* kwa wasiiona, kuna zile fimbo nyeupe, *imagine yule mlema* aliyetoka kilometra nane ameshikwa mkono, angekuwa na fimbo nyeupe ingemsaidia. Lakini ametembea kwa miguu kutoka alikotoka huko Mafia sijui wapi huko, anafika mpaka pale tulipokuwa tunakusanya maoni, anasema nimetembea, nimekuja kutoa maoni yangu nina uchungu na nchi yangu.

Mheshimiwa Spika, hivi hili kundi wamekosea kuzaliwa na ulemavu? Nalisema hilo kwa uchungu kweli kweli, napenda kusitiza kwa Mheshimiwa Waziri, mara nyingi kunakuwa na pesa zinabaki, napenda sana atakapokuwa anajibu hoja, anipe jibu kuwa zile pesa zinazobaki kwa nini zisiende kwa watu wenye ulemavu wakasaidiwa yale masuala yao tofauti waliyonayo, maana wana matatizo mengi watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, maghorofa yanajengwa, hawaweiki miundombinu safi kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu, wanashindwa kupanda, mtu anataka kwenda ghorofa ya tatu pengine, hawezi kwa sababu miundombinu siyo rafiki. Hata hapa Bungeni sidhani kama kuna miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenyewe ulemavu. Mama Mkanga kuna maeneo ambayo hawezi kufika anasema mimi siendi, siwezi kwa sababu miundombinu siyo rafiki. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, unafikiri Mama Mkanga akitakakwenda Uhasibu atawezaji? Ghorofa ya nne, hawezi, atakwenda vipi, hawezi kwenda. Kwa hiyo, langu kubwa lilikuwa ni hilo, kulia na masuala ya watu wenyewe ulemavu, kutetea kwa sababu Mheshimiwa Waziri Mgimwa hakugusia kabisa masuala haya.

Mheshimiwa Spika, haya masuala ya alama za barabarani, kuna Mtanzania mwenzetu anaitwa Mr. Kabatere, amepeleka kabisa Serikalini, Kabatere namtaja, amepeleka mpaka Wizarani mpaka leo miaka na miaka inakwenda. Watu wanapata ajali.

Mheshimiwa Spika, hizo dawa nilizozungumzia *sunscreens lotion*, Watanzania wanapata Kansa ya Ngozi nenda *Ocean Road Hospital* utakuta wagonjwa wa Kansa ya ngozi wamejaa pale, utalia machozi. Sijui kama ulishafika pale, siku moja tembelea pale *Ocean Road Hospital* kwa wagonjwa utajionea.

Mheshimiwa Spika, wagonjwa wanatoka Mikoani, wanakuja kupata matibabu pale wanapata tiba, lakini wengine wanakuja pale, tunashindwa kusafirisha maiti, tunachangishana maiti irudi ilikotoka, kwa sababu wanakuja hawana uwezo, mtu anatibiwa, akimaliza tiba anataka kurudi kwao hana nauli, tunachangishana nauli. Mimi binafsi nimeshalaza wagonjwa wengi nyumbani kwangu wane au watano, nawalaza halafu nawasafirisha kwenda Mikoani. Wanakosa hata nauli, hali ni ngumu sana kwa watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mgimwa na Manaibu Waziri nawapongeza sana mnafanya kazi nzuri sana, lakini naomba mliangalie hili kundi na mtakapokuwa mnawasilisha tafadhali msikose kugusia suala la watu wenyewe ulemavu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa hii nafasi. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Gosbert Blandes atafuatiwa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula na Mheshimiwa Haroub Shamis ajiandae.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Naanza kwa kusema kuwa naunga mkono hoja ili bajeti ipite na Serikali iweze kufanya kazi kupeleka maendeleo kwa wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea naomba kuitia Bunge lako Tukufu nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais wetu mwaka 2005, katika Kampeni zake Karagwe aliahidi ujenzi wa barabara ya lami ya kutoka Kyaka, Bugene mpaka Benako na barabara hiyo inajengwa katika kiwango cha Kimataifa, ninamshukuru na kumpongeza sana. Pia leo nimeona fedha zingine zimeongezeka katika upande wa barabara hasa katika tozo la dizeli na *petrol*, nia yake najua ni kuendelea kutengeneza barabara nzuri, napongeza sana juhudini za Serikali katika hili.

Mheshimiwa Spika, nimeona nianze na hili kwa sababu kuna watu wengine kule Karagwe wanapotosha, wanasesma barabara wameomba wao, kwamba hakuleta Mheshimiwa Rais na Blandes Mbunge wake. Nataka wananchi wa Karagwe waelewe kuwa, barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, mimi Mbunge nimekuwa nikifuatilia humu ndani ya Bunge na fedha hapa naziomba mimi mwenyewe, hakuna mtu mwingine anaomba huko Karagwe, ni mimi Blandes pamoja na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nimeisoma hotuba hii ya bajeti vizuri sana kwenye ukurasa wa 77 nimeona kuna tozo ya mafuta ya *petrol* ambayo Serikali inapendekeza kutoza shilingi 50/= kwa lita ili kupeleka umeme vijijini. Naunga mkono sana wazo hili na nali-*support* kwa nguvu zote kwa sababu tunahitaji kupeleka umeme katika vijiji vyetu kwa wananchi wetu amba ni masikini, Mheshimiwa Waziri namwunga mkono.

Mheshimiwa Spika, lakini nilitamani kwa mapenzi yangu ingawa wengi wape, natamani tozo hii ipande juu kidogo kwa sababu vijiji ni vingi. Natamani ipande kutoka sh. 50/= ambayo tunapendekeza hapa na iwe ni sh. 100/=. Tunahitaji kufunga mkanda kama tunataka kupeleka umeme vijijini kwa wananchi walio wengi, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anapokuja hapa aje na *Amendment* badala ya sh. 50/= kwa lita ije sh. 100/= ili REA waweze kufanya maendeleo vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri asiogope sisi ni Watanzania, tuna moyo wa kujenga nchi yetu na tuna moyo wa kupeleka umeme vijijini kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nizungumzie tozo ya ushuru wa bidhaa. Katika mafuta hapa inapendekezwa kuongeza sh. 2/= kwa dizeli na sh. 63/= kwa *petrol*. Sina tatizo sana, lakini naona ongezeko hili lingeweza kutafutiwa sehemu nyingine kwa sababu lina madhara makubwa sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ukiongeza dizeli na *petrol* maana yake ni kwamba, unaongeza kila kitu hapa nchini bidhaa zote ni lazima zipande na ukishaongeza hivi ni kwamba, hata bei za vyakula lazima zitapanda utake usitake, kodi za nyumba zitapanda.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa, kama inawezekana kodi hii itafutwe katika vyanzo vingine vya mapato. Najua viko vingi sana, tunaweza kwenda kwenye

madiini tukaangalia, tuka-*adjust* kidogo kwenye kampuni za simu ingawa tumeshatoza, tukaenda kwenye sehemu ya utalii, tukaangalia kodiza majumba yetu, tukawaomba *TRA*waongeze *speed*, lakini hii tozo inaweza kuleta madhara makubwa sana kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiangalia *OC*, *OC* Kiswahili chake ni posho ya matumizi mengineyo. Mwaka jana 2012/2013, tulipiga kelele sana hapa tulipitisha matumizi mengineyo ya trilioni nne na yenye we tulipitisha kwa shida sana, lakini mwaka huu naona kuna ongezeko, imeongezeka tena hiyo *OC* inakwenda mpaka trilioni 4.5. Maana yake ni kwamba, kuna ongezeko la shilingi bilioni 500.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwa kuwa hii ni hela ya posho, ni hela ya mapochopocho, ni hela ya vitu vya kawaida, napendekeza hili ongezeko la shilingi bilioni 500 ibanwe iende sehemu zingine. Kwa mfano, kama sehemu za umeme vijijini, upande wa maji, upande wa Afya na sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, inawezekana hili tukajibana matumizi yetu, badala ya kula sambusa nne ofisini, tukala sambusa moja, hizi shilingi bilioni 500 zikaenda kwa wananchi wetu ambao ni walala hoi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mishahara ya watumishi; nampongeza Mheshimiwa Waziri sana kwa juhudhi ambazo amezionesha za kupunguza ile *pay as you earn*, lipa kadri unavyopata, kwamba Mtumishi anakatwa kodi kutokana na mshahara anaoupati. Hii itaongezea nafuu kidogo Watumishi wetu ambao wamekuwa wakipiga kelele kuwa mshahara ni mdogo.

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kuangalia kwa undani, nimesoma sana kitabu hiki punguzo ambalo linatokea hapa, ilikuwa inakatwa 14% sasa Watumishi wote watakatwa 13%, ya mshahara wao, ni sawaswa na kushuka kwa 1%. Hili punguzo sawa lipo lakini ni dogo sana, haliwezi kuonesha maana yoyote kwa Mtumishi.

Mheshimiwa Spika, napendekeza ili Watumishi wetu Walimu, Manesi, Madaktari, Mabwana Shamba, Mabwana Kilimo na Wafugaji na Mabawana mifugo ili angalau hili punguzo liwaletee maana yoyote, badala ya kuwakata 13% ya mshahara wao. Napendekeza tuwakate angalau 10%, hizi 4% wabaki nazo na wao waweze kujikimu. Hii inawezekana, Mheshimiwa Waziri aliangalie ili Watumishi wetu na wao wapate raha ya maisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kodi ya magari; nimesoma bajeti ya Mheshimiwa Waziri anapendekeza kuwa magari yaliyozidi umri wa miaka kumi yaongezewe ushuru kutoka 20% kwenda 25%, zinaongezeka 5%. Sababu alizozitoa ni kwamba, magari mengi yamechakaa pamoja na sababu za kimazingira. Hizi sababu siyo kweli, siyo kweli kuwa gari likikaa miaka kumi limechakaa, kuna gari linaweza kutumika miaka miwili likawa bovu likachaa, gari linaweza kutumika miaka kumi na tano na likawa bado ni zuri sana na jipya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia Watanzania wetu tunawajua, Mtanzania wa Karagwe kule Cha Mchuzi, kule Kituntu, Iyembe, Nyashozi, Nyabyonza, kununua kagari kenyewe haka kwa 20% ilikuwa ni kazi, leo unamwongezea zaidi maana yake ni kuwaambia watu wale kuwa wasinunue gari hata siku moja. Napendekeza kwamba, ushuru huu wa magari ubaki kama ulivyokuwa kwa 20% ili watu wetu na wa kawaida waweze kumiliki magari.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo nataka kuzungumza, tunapitisha bajeti leo hapa, lakini imekuwa ni kawaida fedha hizi kutopelekwa Mawizarani, sehemu ambazo tumelenga au kwenye Halmashauri ndani ya muda tulio upanga. Napendekeza bajeti hii iwe ni bajeti ya kwanza kuhakikisha kuwa fedha zote tulizopitisha hapa zinakwenda kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa sababu ya muda, mimi natoka Wilaya ya Karagwe na kule Karagwe kwenye bajeti hii nimeangalia kuna fedha za maji zimeongezeka nyingi sana, Serikali ifike wakati imalize kilio cha wananchi wa Jimbo la Karagwe kwa kuweka mtandao wa maji katika Wilaya ya

Karagwe na fedha zenyewe ziko hapa. Mheshimiwa Waziri apeleke maji katika Wilaya ya Karagwe, wananchi wa Karagwe wana vyanzo vingi vya maji; Ziwa Kajunju, Mto Kagera, Ziwa Victoria na sehemu zingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho, pamoja na mipango ya kukuza uchumi sijaona ni vipi Kanda ya Ziwa tunasaidiwa kuinuka kiuchumi. Ili Kanda ya Ziwa iinuke kiuchumi tunahitaji kuwa na viwanda mbalimbali, tunahitaji kiwanda cha saruji. Kiwanda cha saruji kwa ajili ya Shinyanga, Mara, Mwanza, Geita pamoja na Kagera lakini hatujaona hapa mkakati wa kuanzisha viwanda ili vijana wetu waajiriwe katika viwanda hivyo waweze kujongezea kipato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, lakini naomba Mheshimiwa Waziri ayachukulie maanani wakati anajumuisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Dunstan Kitandula atafuatiwa na Mheshimiwa Haroub Shamis halafu watafuatia Mheshimiwa Desderius Mipata, Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Mtutura Mturura, Mheshimiwa Henry Shekifu na Mheshimiwa Dkt. Peter Kafumu.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya nchi yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema ili niweze kuendelea kulitumikia Taifa langu.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kama wenzangu walivyosema mwanzoni, kukupongeza kwa uamuzi huu wa kuanzisha mfumo mpya wa bajeti, lakini mimi nitakwenda hatua moja mbele, kwamba mfumo huu peke yake hautoshi, tuna kiu ya kuona sasa tunaanzisha bajeti ofisi, tunakuwa na Sheria itakayowezesha Kamati yetu ya Bajeti kuweza kufuatilia utekelezaji wa bajeti hii. Tunaomba hili lije kwa haraka sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naseme kwamba, naiunga mkono bajeti hii. Niseme kwa nini naiunga mkono bajeti hii. Naiunga mkono bajeti kwa sababu yale ambayo yalikuwa kilio kwa Wabunge wengi, Serikali imeyasikia.

Mheshimiwa Spika, kuitia bajeti hii sasa naamini kwamba umeme vijijini utapatikana, ni imani yangu kuwa Kata ya Mwakijembe ambayo Kata nzima haina umeme, sasa itapata, imani yangu ni kuwa Kata ya Daluni kule Mkinga ambayo Kata nzima haina umeme, sasa itapata, imani yangu ni kwamba Kata ya Kigongoi itapata umeme, imani yangu ni kuwa Vijiji vya Mapatano, Gombelo navyo vitapata umeme. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono bajeti hii kwa sababu nina matumaini ya kupata maji katika Wilaya yangu ya Mkinga. Naipongeza Serikali kwa ukuaji wa uchumi, hata hivyo, ukuaji huu wa Uchumi haunufaishi walio wengi.

Mheshimiwa Spika, *Household survey* ya mwaka 2007, inatuambia kuwa, 37% ya wananchi walioko vijijini hawapati huduma muhimu, 33% ya watu walioko mijini hawapati huduma muhimu lazima tuhakikishe kuwa ukuaji huu uchumi unajibu hoja hii, unahakikisha kuwa wananchi hawa wanapata huduma muhimu.

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa Benki ya Maendeleo ya Afrika katika *study* zao wanasema kwamba, moja ya tatizo letu kubwa ni kuruhusu mali zetu tuzipeleke katika masoko ya nje tukiwa hatujaziongezea thamani. Ni lazima sasa sisi kama Taifa tubadilike, katika hili lazima tuhakikishe kuwa bidhaa zetu tunaziongezea thamani.

Mheshimiwa Spika, mwaka mmoja uliopita tuliruhusu uuzaji wa mazao nje ya nchi, wananchi wakaitikia kwa mwamko mkubwa, tukauza mahindi kwa kiasi kikubwa sana. Ni lazima tufike mahali tuseme kwamba, ndani ya kipindi cha miaka miwili ijayo haitakubalika kuuza mahindi nje ya nchi isipokuwa tutalazimika kuuza unga.

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe pole kwa ndugu zetu waliopotezamaishakule Arusha, pamojanamengiyaliyosemwa, lakini nataka nilizungumzie tukio hili kiuchumi, nilikuwa nasoma kitabu cha hali ya uchumi, kitabu hiki kinatuambia kwamba, Sekta ya Utalii inatuingizia bilioni 1.37 Dola za Kimarekani. Sasa kama hali ni hiyo maana yake ni kuwa, Sekta ya Utalii ni muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ile ambayo inatokea vurugu ndiyo kitovu cha utalii katika nchi hii. Nilikuwa nasoma ripoti ya *National Geographic Survey* ya leo, wanasema Wakenya wanapoteza takribani Dola milioni moja kwa siku kwa sababu ya tatizo la Uharamia na ugaidi, jambo ambalo limeathiri Sekta ya Utalii, wenzetu wamekwishaathirika kiasi hicho, nawasihi sana ndugu zangu Watanzania, tusikubali kuachia Sekta yetu ya Utalii ikaathirika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sekta ya fedha; taarifa za Benki Kuu zinasema, tuna mabenki yasiyopungua arobaini na tisa sasa, lakini taarifa ya *FINSCOP* ya mwaka 2009 inatuambia kwamba, ni Watanzania wanane kati ya Watanzania 100 ndiyo wanaopata huduma za kifedha, ni asilimia nne tu ya Watanzania ambao wanapata huduma za kifedha kupitia taasisi za kati za fedha. Maana yake nini, maana yake *penetration rate* ya huduma za kifedha vijijini ni ndogo sana. Maana mabenki haya tuliyonayo pamoja na wingi huu bado yanahudumia maeneo ya mijini. (*Makof*)

Mheshimwia Spika, asilimia 75 ya Watanzania wapo vijijini. Tunaporuhusu mfumo wa kifedha huu ambao hauko sahihi, unaoacha kundi kubwa kama hili lisihudumiwe maana yake tunasema Watanzania asilimia 75 wasishiriki kwenye kuumiliki uchumi wa nchi yao, hii haikubaliki hata kidogo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunapokubalihalihiendelee, tunabariki mifumo ambayo siyo halali ya ukopeshaji inayoendelea katika maeneo ya vijijini. Tunapokubali mfumo huu kuendelea,

tunawaambia wakulima, waendelee kukubali mazao yao yanunuliwe yakiwa bado kwenye mashamba yao. Hatuwezi kukubali unyonyaji huu uendelee. Naishi sana Serikali iliangular suala hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni usimamizi mbovu tulionao katika *Bureau De Change* zetu. Tumekuwa na usimamizi mbaya sana, *Bureau de change* zimeachwa zifanye kazi zinavyotaka. Leo hii *bureau de change* zinatumika kusafirisha fedha nje ya nchi bila kusimamiwa na mtu yejote, wakati hili likiendelea Serikali haipati mapato yake, ni lazima suala hili likome. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana tulisimamia vizuri suala la mafuta wakati ule tulipokuwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi, kwa kuhakikisha kwamba kodi ya *diesel* na mafuta ya taa hazipishani ili kuepuwa uchakachuaji. Mwaka huu tumefanya kosa, tofauti iliyopo ni ya shilingi themanini kati ya *diesel* na mafuta ya taa. Naiona hatari ya suala la uchakachuaji kurudi, naiomba Serikali yangu itafakari upya suala hili. Wakati ambapo ni suala la msingi kuongeza bei hizi, lakini vile vile tuhakikishe kwamba bei hizi haziwi sababu ya suala la uchakachuaji kuendelea. (*Makoff*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, wamefanya kazi kubwa sana katika kupandisha makusanyo tangu waliporuhusiwa kufanya kazi hii. Wakati ule walipoanza *TRA* walikuwa wanakusanya milioni 900 kwa mwaka, leo hii Bodi ya Kubahatisha inakusanya bilioni tisa kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni nini? Mapato haya yanakwenda wapi?

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Kengele ya kwanza au ya pili?

**SPIKA:** Ni kengele ya pili, ahsante sana.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa nimwite Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, na Mheshimiwa Mipata na Mheshimiwa Assumpter Mshama wajiandae na Mheshimiwa Mkosamali ataingia kabla ya Mheshimiwa Mtutura.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Serikali ya Wizara ya Fedha au Bajeti Kuu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza namshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataalah* kwa kunipa afya na uwezo wa kusimama katika Bunge lako Tukufu kuchangia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wakati Waziri wa Fedha tulipokuwa nae *back bench* akichangia katika hoja za uchumi wa nchi, nilikuwa nikisema kama atakuwa Waziri wa Fedha huyu, basi hakika nchi itapaa! Lakini sasa sijui kasahau! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, namheshimu sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, lakini nataka nimkumbushe tu kwa sababu sisi Wabunge tuna jukumu kubwa la kuishauri Serikali na kuielekeza. Pia nataka nichukue fursa hii niseme na Rais wangu Jakaya Kikwete, asitutenge sisi Wabunge wa Vyama vya Upinzani, sisi ni Wabunge wa Bunge la Jamhuri na tunaweza tukachangia mambo mengi yenye maslahi ya nchi hii, lakini tangu tulipomwona wakati tunaapishwa hapa, hatujamwona tena, akija anakutana na Wabunge wa Chama chake peke yake. Tunajisikia unyonge kidogo. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Serikali ya mwaka huu imepangwa kutumia shilingi trilioni 18.2, ambazo shilingi trilioni 12.5 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi trilioni 5.6 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo nilipopata mashaka na Waziri wa Fedha, pamoja na kwamba namheshimu lakini namkumbusha kwamba, ili nchi iweze kwenda na hatua za

kimaendeleo za kiuchumi, basi angalau iwe inalingana bajeti ya maendeleo na ile ya matumizi ya kawaida, lakini hili pengo liliopo ni kubwa sana. Asilimia ndogo ambayo labda ni 31 ndiyo fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli fedha nyngi zinatumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hapo hali ya ukuaji wa uchumi bado itakuwa inadorora tu. Kama lengo tunalojiwekea la kufika asilimia 7.2 mwakani na mwaka huu tunaomalizia uchumi umekua kwa asilimia 0.1 ni kama haukukua, asilimia 0.1 ni kama vile hakuna kilichoongezeka.

Mheshimiwa Spika, pia fedha hizo hizo za bajeti ya mwaka huu tunaozungumza triliungi nne na nusu ambayo ni asilimia 25 ya bajeti yote zimepangwa kutumika katika matumizi yanaitwa *OC*. Kweli matumizi haya yana umuhimu wake, lakini siyo kiasi hiki. Fedha hizi zinahitajika zipunguzwe angalau kwa asilimia 10 zipelekwe kwenye bajeti ya maendeleo na bajeti ya maendeleo iwe angalau theluthi moja ya bajeti yote. Iwe asilimia 34 au 35 ya bajeti yote, lakini mmeweka chini sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tatizo ni kwamba, bajeti yetu inakuwa ni tegemezi pamoja na kwamba nchi hii ina uchumi mkubwa, siku zote tunaikumbusha Serikali hapa, lakini bado uchumi huu hauonekani kwa wananchi, wananchi bado ni maskini, wanakula mlo mmoja pamoja na uchumi wote uliopo. Tatizo wale wenye fedha hawalipi kodi. Serikali inaelekeza nguvu kubwa kukusanya kodi kwa wale ambao hawana cha kulipa, ndiyo tatizo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, sekta zetu za madini, migodi, mbuga na vivutio vya utalii havijatumika vizuri. Makampuni ya madini fedha walizonazo, lakini kodi haipatikani. Nchi za wenzetu wenye mafuta na gesi na madini mengine ya dhahabu wanapata fedha nyngi. Nchi ndogo tu hapa ya *Seychelles* sera yao walikuwa wanasmae wapewe asilimia tano ya mrabaha katika mapato yatakayopatikana katika gesi au mafuta, lakini wakakubaliana wakasmae asilimia tano ni kidogo sana wakastopisha, wakakubaliana wakasmae tuweke asilimia kumi, sisi asilimia tatu! Asilimia tatu, *this is nothing!*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha kwa kweli, ni mali tumeichuma, tunawapa watu wakatumie kwao halafu watugawie sisi, tunawapa katika bakuli la dhahabu, wao wanatugawia katika kisahani biskuti! Hili ni jambo la kuhuzunisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia watu wenyewe fedha tunasema hawalipi kodi, hatusemi tu hivi hivi, ushahidi upo, viwanda havilipi kodi. Ni watuwachache wenyewe uzalendo wenyewe viwanda katika nchi hii wanaolipa kodi inayostahili. Tunahimiza wawekezaji ili watu wapate kazi sawa, tunawapa *benefit za exemption* sawa, lakini basi ile kodi halali ya Serikali ipatikane! Lakini haipatikani. Kwa nini haipatikani, ni kwa sababu kuna ushaghalabaghala katika ukusanyaji kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania *Revenue Authority* wanabargain na hawa watu, wanataka rushwa. Utashangaa wewe Mbunge unakwenda *TRA* pale una jambo lako dogo, basi yule Afisa wa *TRA* anakukazia macho ili umpe rushwa. Huwa nawaambia huogopi kazi yako, mimi Mbunge unaniambia nikupe rushwa? Hali tuliyonayo ni hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini hapa ushahidi uliotolewa na Tanzania *Bureau of Standards (TBS)* wanasema kiwanda cha sabuni kinachotengeneza sabuni inayoitwa *Kleensoft detergent* cha Dar es Salaam hata mahali kilipo kiwanda hakijulikani. Kiwanda kina nembo ya ubora wa *TBS*, lakini hata mahali kilipo hakijulikani. Sasa kama kiwanda hakijulikani mahali kilipo kodi itapatikana vipi?

### **MBUNGE FULANI:** Hamna!

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, sabuni hii imejaa Dar es Salaam katika *supermarkets*, hali tuliyonayo ni hiyo. Kiwanda ni kitu kikubwa siyo kama kalamu utaitia mfukoni isionekane kama hii. Leo kiwanda hakijulikani kilipo, haiingii akilini, ni kwamba wanafichwa makusudi kwa lengo la kujinufaisha watu wachache, haikubaliki! (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunataka Rais uje hapa tuzungumze na wewe, tukueleze hali ilivyo, nchi inamalizwa hii, uje uonane na Bunge usionane na Wabunge wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mambo yapo mengi mazito hapa, lakini naona kengele ilishaanza kulia, ngoja nichague kidogo ya kuruka.

Mheshimiwa Spika, viwanda pia vinaongeza *production cost*, gharama ya uzalishaji iwe kubwa *that means una-minimize profit*, watasema tumezalisha kwa gharama hii, kumbe ni gharama nyingine, ndiyo hayo hayo katika madini, wanatuletea ripoti wao, tumpata madini hayam *then* wanatugawia wanachotaka. Haya ni mambo ya kuhuzunisha.

Mheshimiwa Spika, lakini pia hali ya uchumi bila ya kufanya jitihada za makusudi za kuwekeza kwenye kilimo, uchumi hautakua, uchumi utakuwa unakua kwenye makaratasi, lakini hauonekani kwenye maisha ya watu. Ajira zote asilimia takribani 75 mpaka themanini ya Watanzania ipo kwenye kilimo, hapa ripoti ya Waziri inaonesha kwamba pamoja kwamba kilimo kimekua kwa asilimia 4.3, lakini kimechangia pato la Taifa kwa asilimia 24.7, imekuwa kinyumenyume na sekta ya mawasiliano iliyokua kwa asilimia 24 imechangia asilimia mbili pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika utaona tatizo hapo, haiingii akilini, sekta ile ambayo imekua kwa asilimia 24 inachangia kwa asilimia mbili, ile iliyokua kwa asilimia nne inachangia kwa asilimia 24. Kwa hiyo, lazima nguvu zielekezwe pale kwenye kipato yaani kilimo ndio watu wataondokana na umaskini na uchumi utapatikana na utakuwa mzuri na fedha zitapatikana Serikalini. Lakini leo tuna-*invest* fedha nyingi kwa kuwanufaisha watu wachache.

Mheshimiwa Spika, hii haikubaliki, tunasema haikubaliki na Waziri Mgimwa kwa nafasi yake tunamheshimu sana mzee wangu, elimu yake na cheo chake ayafanyie kazi haya. Tuone yale matunda tuliyokuwa tunazungumza huku *bench* pamoja. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, pia fedha za maendeleo *impact* yake haionekani kwa sababu vipaumbele vimekuwa vingi. Tuweke vipaumbele vichache, vizalishe halafu vile vinavyozalishwa vitazalisha wenzake, kama vile mtu anaoa, anazaa halafu anakuwa na wajukuu. Huwezi ukasema umeoa uzae watoto wengi utashindwa kuwalea.

Mheshimiwa Spika, napendekeza tuwekeze nguvu zaidi kwenye Kilimo, Uchukuzi, Nishati na Afya, kwa sababu bila ya afya watu watakuwa hawawezi kufanya kazi. Mambo manne haya tuyafanyie kazi kwanza kwa nguvu kubwa, *then* miaka miwili, mitatu tunaongeza vipaumbele vingine, hapo tutaweza kwenda kwa *speed* kubwa.

Mheshimiwa Spika, tukitegemea uchumi ukue mwaka 2014 ufikie asilimia 7.2 utakuwa kama haujakuwa kitu na nchi inatakiwa ifikie asilimia nane mwaka 2015, haifiki kwa ukuaji huu wa uchumi, kwa mwendo huu, uchumi unaongezeka kwa mwaka kwa asilimia 0.1 haifiki asilimia nane mwaka 2015. Kwa hiyo, ni lazima tujikaze, tushirikiane ili tuweze kulisogeza Taifa.

Mheshimiwa Spika, sitaki kengele inililie na nakushukuru. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mipata atafuatiwa na Mheshimiwa Assumpter Mshama, Mheshimiwa Felix Mkosamali na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2013/2014. Kwanza, naunga mkono hoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, napongeza wazo la kuanzishwa kwa Kamati ya Bajeti kwa sababu matunda yake tumeyaona. Lakini pia naipongeza Kamati yenyewe kwa namna ambavyo imefanya kazi nzuri sana. Naipongeza pia Serikali kwa kuja na bajeti ambayo kwa kweli inaonesha usikivu kwa michango mbalimbali ambayo imekuwa ikitolewa na Wabunge.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii naiona kama inatafsiri kazi nzuri ambayo imekuwa ikifanywa na Wabunge tofauti na wenzetu ambao wanaiponda. Naiangalia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti iliyopita, nimeona kwamba, tumefanya vizuri hasa katika kutoa pesa za kwenda kushughulikia miradi. Changamoto ambayo unaweza ukaikuta pale ni changamoto ya fedha za wafadhili, lakini fedha zetu tumetoa zaidi ya asilimia 99. Huu ni mwanzo mzuri.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiiangalia bajeti tumetenga kwa mwaka huu asilimia 31 kwenye miradi ya maendeleo tofauti na mwaka jana ambayo ilikuwa asilimia 30. Kwa hiyo, ni hatua kwenda mbele, ingawaje sasa hatuwezi kukubaliana kwamba tunatosheka hapo, tuongeze jitihada ili ifikie angalau asilimia 40. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nalinganisha na nchi nyingine, Kenya iko kwenye asilimia kama 28, kati ya matumizi na fedha za miradi, kidogo Rwanda ndiyo wanakwenda vizuri, wapo karibu asilimia 48, sisi tupo asilimia 31 si haba tunakwenda vizuri katika *region* yetu. Kubeza juhudhi hizi siyo kuitakia Serikali mema kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto, katika makusanyo nimeona changamoto, *TRA* nadhani wanajiwekea makisio madogo, lakini vile vile makusanyo ya maduhuli ya Serikali bado ni hafifu.

Mheshimiwa Spika, upande wa changamoto zinazoonekana *TRA*, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya *PAC*, nimeona katika vitambulisho vya Taifa na leseni mpya za madereva, tusipowaangalia wale mabwana watatuingiza kwenye migogoro mkubwa wa Kitaifa na makampuni au mawakala wakubwa duniani. Ni mambo ya ajabu ajabu yanakwenda huko na hayana tija kabisa kwa Taifa, ni jambo la kuangalia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile makusanyo yanayoelekea upande wa Halmashauri yasiyo ya kodi, tuliweka lengo la kukusanya zaidi ya bilioni 362.2, kilichopatikana ni bilioni 177.4, ufanisi wake ni asilimia 49 peke yake, hii ni hatari vile vile. Hii inatokana na mambo yafuatayo: uaminifu mdogo, weledi wa ukusanyaji wa mapato hakuna na hata vyanzo vyenyewe havijaainishwa nya kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la mapato nashauri, Serikali imeeleza mikakati yake huku, lakini iangalie utaratibu wa kuwezesha kuyatembelea maeneo ambayo tunatakiwa kupata mapato yanayoshughulikiwa na *TRA*. Kama sisi wenyewe hatuwezi, basi tuweze hata ku-*hire* makampuni mengine duniani ambayo yana uwezo na uzoefu mkubwa katika kuangalia vyanzo nya mapato vizuri, viainishwe ili waweze kuwekewa *target* ya kutosha. Halmashauri kadhalika vile vile zisaidiwe, hazina uwezo wa ku-*hire* kampuni ambazo zinaweza zikafanya hivyo. Serikali izisaidie wabainishe vyanzo vyao na mfumo wa ukusanyaji uweze kuboreshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii tumeweka vipaumbele kama miundombinu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu na uendelezaji wa huduma za jamii. Nashauri na nakubaliana na wale wanaosema kwamba, vipaumbele vikiwa vingi hatutakwenda kwa kasi inayotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nikubaliane na Kamati tuwe na vipaumbele angalau vitatu na kati ya hivyo vitatu, napendekeza viwili, Kilimo. Kilimo kiwe ni moja ya kipaumbele na ukiangalia mchango wa kilimo wenzangu wameeleza, kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania. Mchango wake kwa pato la Taifa ni zaidi ya asilimia 24.7. Licha ya ukuaji mdogo wa asilimia karibu tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kilimo kinazalisha chakula na Wachumi wanatuambia kwamba katika mfumko wa bei bidhaa za huduma zinatokana na chakula ndizo zinazochukua asilimia

kubwa katika mfumko wa bei, zaidi ya asilimia 47.8. Kwa hiyo, ukiacha kilimo huna namna ya kukuza pato la Taifa. Ukiacha kuhudumia kilimo, utashindwa kubeba watu wengi ambao wanategemea kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwangu kule huwa nawaambia vijana wa Nkasi Kusini kwamba, jamani sisi huku tumezungukwa na ardhi nzuri na Mungu bariki hali ya jiografia ya kwetu inaruhusu uvunaji. Nikawaambia tuachane na watu wa mjini hawa, twende tukajikite katika kilimo na watu wanabadilika, kilimo kinawabadiisha. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, zipo changamoto za kilimo ambazo lazima nazo tuziangalie. Kama tunakubaliana kukuza kilimo, lazima tukabiliane na changamoto za kilimo, ikiwa ni pamoja na pembejeo kuwa ghali sana, kutokuwafikia wakulima kwa wakati. Hakuna mfumo unaoeleweka na ulio bora kuwafikia wakulima, ufeki mwingi mno, wizi na hakuna mtu aliyejizatiti kikamilifu kushughulikia wezi wanaoshughulika katika Sekta hii. Inakuwaje kinakuwa kipaumbele cha Taifa na tunakitegemea, lakini hakuna wezi wanaokamatwa, kila mwaka tunapeleka fedha za pembejeo, zinaharibiwa lakini hatukamati mwizi. Utaratibu wa wapi huu? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lazima kama nchi tuwe na mkakati wa kuboresha kilimo. Tukabili changamoto zote zinazoathiri wakulima. Wakulima ni watu wanyonge na hao ndio wamewapunguzia mzigo. Wanajitegemea wao wenyewe, hawasemi ajira, hawasemi chakula, wanajihangaikia huko waliko na wala hawafanyi maandamano. Sasa mnataka nini? Wasaidleni wakulima kwa mifumo mizuri ili waweze kuzalisha na kutulia na kupandisha pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, lakini katika kilimo kuna uchache sana wa Maafisa Ugani. Kuna uchache sasa wa uzalishaji wa Vituo vya Mbegu. Pale Milundikwa kwenye Jimbolangu kimeanzishwa kituo hatuna hata hela, hakijawezeshwa, kimekaa tu, mwisho, ardhi yake nzuri ambayo ilipewa na Halmashauri inakodishwa kwa watu wanalima mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie kwa makini sana jambo hili. Lakini muhimu sana ni miundombinu ya barabara vijiini, huko wakulima wanakolima, tunatakiwa kuwa na barabara zilizo bora ili kuyachukua hayo mazao kuyapeleka kwenye masoko. Hapo kilimo kitaweza kustawi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kidogo kuhusu umeme. Umeme vijiini kwa hali ilivyo sasa hivi na kwa bajeti hii, nina uhakika tutapata maeneo mengi. Maeneo yangu yale ya Kate, Makao Makuu ya Jimbo langu, maeneo yangu yale ya Katani, Chonga, Chalatila na Sintali, nina imani yatapata. Laki ni tufikishe umeme Wampembe ambao tunapigia kelele kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule hatuna barabara, lakini sasa tukifikisha umeme, ni kilometra 67 tu, tukifikisha umeme tutakuwa tumewakomboa watu wote ambao wapo kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika ambao ni maskini sana, lakini kuna Ziwa, rasilimali tajiri zipo kule. Tutaweza kuwainua kiuchumi kwa sababu tutaweza kusindika mazao yanayotokana na ziwa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia barabara zetu, nazitaja kila wakati na leo nilikuwa nazisema hapa; Kanakala – Kitosi - Wampembe ni barabara muhimu sana katika Jimbo langu. Ziangaliwe kupitia bajeti hii japo zipo kwenye Halmashauri. Hatua kidogo mmeshaanza, nimepata milioni 400 kwa barabara moja na milioni 400 nyingine nimeahidiwa kwenye barabara nyingine kwa bajeti. Huu ni mwanzo mzuri. Hali hiyo nzuri muiendeleze katika bajeti zijazo ili mhakikishe kwamba, pesa hizozinapatikana ili wananchi waweze kupata mawasiliano mazuri na huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, viro vituo vya afya. Kituo cha Afya cha Wampembe kesho tutakabidhiwa gari zuri ambalo wenzetu wa *Plan International* na *Africare* wanatuletea baada ya kubaini watu wanakufa sana na watoto wanakufa sana kule. Naomba wenzetu kule muipokee vizuri misaada hiyo na muitumie vizuri.

Mheshimiwa Spika, haya ni matokeo ya uongozi mzuri wa Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete na ahadi zake alizozitoa kwetu. Watapita wengi wakiona mafanikio na kusema maneno mengi, lakini sisi ndiyo tunayoyasemea humu ndani na Rais ndiye aliyeahidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nimwite Mheshimiwa Assumpter Mshama, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Mkosamali na Mheshimiwa Mtutura Abdallah ajiandae.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi leo ili niweze kuchangia katika suala la Bajeti ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda tu nikupongeze wewe binafsi na Serikali nzima kwa kukubaliana kuanzisha Kamati ya Bajeti. Kwa kweli imeonesha mabadiliko makubwa katika bajeti yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kuipongeza Serikali au kuishukuru kwa namna ya pekee kwa bajeti hii ambavyo wametuwekea. Vijiji vyangu 24 vitapata umeme katika bajeti hii na zaidi ya yote nashukuru kwa ajili ya milioni 400 nilizopewa kwa ajili ya daraja la Kabingo. Kwa hiyo, kutoka Kanyigo kukatisha kwenda Kyaka kutakuwa ni rahisi sana. Nashukuru sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, niende tu moja kwa moja kwa kuchangia bajeti hii. Kwanza nianze na vipaumbele. Kuna vipaumbele tulikuwa navyo mwaka uliopita katika bajeti na vipaumbele hivyo vilikuwa ni miundombunu, kilimo, viwanda, maendeleo ya rasilimali watu ambavyo watu wengi ukiuliza hawalielewi hili. Namaanisha elimu, tulikuwa na huduma za utalii na huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa wakati ule nilipochangia mpango wa Mr. Mpango, ulionekana kabisa kwamba, mpango ni mzuri lakini ulikuwa una mambo mengi ambayo inaonesha kabisa kwamba ule mpango kutekelezwa utakuwa mgumu na kweli imejitokeza. Mwaka huu tena tumerudi na vipaumbele vile vile.

Mheshimiwa Spika, kwa maana nyingine kama tungekuwa tumeamua kuchukua vipaumbele vitatu, ina maana leo tungekuwa tunaongelea vitatu vingine. Matokeo yake vipaumbele sita, hata robo tatu haijafika wala nusu haijafika. Mwaka huu tena tumerudia vipaumbele vile vile. Kwa hiyo, naona maana ya vipaumbele ndani ya vipaumbele ni kosa.

Mheshimiwa Spika, ningeomba tu nishauri, kama inawezekana tukaamua hata sasa hivi, hata jana vingine viko nusu, tukasema tunaamua kuchukua vitatu tu. Tukaamua kwamba sasa tunakwenda na miundombinu, kilimo pamoja na elimu. Huwezi kuwa na miundombinu na elimu ni kipaumbele cha tano ukadhani utapata matokeo. Naona kwamba ni bora tuamini huwezi kupata daraja zuri bila kusomesha watu. Huwezi kupata kilimo kizuri bila kusomesha watu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunganeza na elimu, tukafanya miundombinu ambayo mazao ya kilimo yakizalishwa yatasafirishwa, kwenda kwenye soko na hivyo utapanua wigo wa ajira pia, tayari vitatu tungevimaliza, lakini sita vyote vimerudi tena, tuvipitishie hela tena. Kwa hiyo, nashauri tuwe na maamuzi mazuri katika suala la vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, niongelee juu ya mishahara ya wafanyakazi. Mwaka huu tumetenga shilingi triliioni 4.763 yaani 4,763,000,000. Ni fedha nyingi sana, lakini ukilinganisha na mwaka jana, imeongezeka kama *percent* 26. Inawezekana wanayo maelezo mazuri, lakini utashangaa hizo pesa hazilingani na uwiano wa ile tija ya kazi inayopatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, tunatenga hela zote hizi lakini nenda Ofisini, utakuta watu hawako Ofisini. Nenda maofisini saa nne,

huwezi kujua Tanzania majira ya queu kupungua barabarani na majira ya watu kuwa kazini. Saa zote magari yamejaa barabarani, ina maana hawa watu hawana malengo. Mtu kama utapewa malengo, nina uhakika huwezi kutoka kwenye kiti chako mpaka umemaliza malengo yako. Tatizo kubwa hatuweki malengo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utakuta wafanyakazi wengi wako Kariakoo wanachagua mitumba, wanachagua nguo, wanafanya vitu vya *kitchen party*, harusi na kadhalika, maana hana mtu wa kumwuliza kwamba kazi yako leo iko wapi uliyofanya leo. Pesa analipwa kama mtu ambaye amefanya kazi masaa yote kazini. Matokeo yake inavunja moyo kwa watu waadilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mtu mwadilifu yuko kazini tangu asubuhi mpaka jioni na yule mtu mtoro, mwongo leo baba kafa, mama kafa, mama mdogo, shangazi, kila siku ana-excuse, lakini anapewa mshahara sawasawa na yule anayeshinda pale kazini ambaye ameamua kufanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali, kwa nini tusiweke utaratibu wa motisha kwa watu ambao wamejitoa kufanya kazi, wakalipwa tofauti na wale wanaoshinda wanazurura na hivyo lazima tuwawekee watu malengo. Mwezi huu lazima tufanye mpaka hapa, mwezi huu tufanye mpaka hapa. Bila malengo tutakuwa tunarudi hapa kupitisha bajeti zile zile kwa sababu hatuwapi muda wa kufanya hizo kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hebu niongelee matumizi ya Serikali. Ninachokiona, niongelee tu habari za magari, magari ya Serikali au STK na vyovyote vile, kwa kweli matumizi ya magari siyo sawasawa. Nilifanya jambo moja pale Dar es Salaam tulipokuwa kwenye Kamati, nikaenda kwenye gari moja, sitaitaja kwa sababu nitamwambia Waziri hilo gari na dereva mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, unakuta Madereva wamewasha AC kwenye gari kwa kuwa Dar es Salaam kuna joto, yuko ndani ya gari tangu tunaanza Kamati mpaka yule mwenye gari atakapokuwa anaondoka mkutanoni. Hivi kweli tunaweza kubana matumizi kwa namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, dereva anakaa Gongolamboto, kiongozi anayemwendesha anakaa Mbweni. Anatoka Gongolamboto anamfuata Mbweni, wanarudi Dar es Salaam katikati kufanya kazi. Hayo ni mafuta yametumika. Hivi kweli tunaweza kupunguza matumizi? Ni vipi tufanye, nashauri, wenzetu wanafanyaje ili kupunguza matumizi ya magari. Petroli sasa hivi iko juu sana, sasa ni namna gani tunaweza kupunguza matumizi mabaya ya magari.

Mheshimiwa Spika, pia niongeleematengenezo ya magari. Zile *profoma* zinavyoandikwa, labda tungeweza kujenga *dispensary* hata 20 katika Wilaya zetu. Unakuta *profoma* ni za uongo kabisa, gari kila siku ni *Toyota*, ni *millions of money* zinapotea kwa ajili ya ku-service magari.

Mheshimiwa Spika, sasa tufanye nini? Nashauri katika moyo wangu ninachofikiri, kama kiongozi anakaa Tabata, basi na dereva wake acae Tabata. Kama kiongozi anakaa Mbweni na dereva wake acae Mbweni. Au tufanye ule utaratibu alioshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, kiongozi aje na gari lake apaki ofisini, baada ya kazi achukuliwe arudishwe nyumbani, lakini siyo mwisho wa kona hii na mwisho wa kona hii, matokeo yake unatumia petroli nydingi.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye makusanyo ya mapato. Katika makusanyo ya mapato tatizo kubwa ambalo linatukabili katika ukusanyaji ni uwezo mdogo wa kukusanya kodi. La pili, kukosa wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kuwa katika Kamatiyako ambayo ilikuwa inaandaa muundo huu. Niliona watu tuliokuwa tunawaauliza, wanasema tufanye nini, hatuna wataalam wa kutosha wanaoweza kutusaidia kukusanya kodi ya kutosha. Mifumo yenye ni dhaifu, inatoa nafasi ya mtu kutoa rushwa.

Unamtuma mtu kwenda kukagua mtu mwenye mabilioni, bilioni 50 halafu ana-negotiate na yule mtu, anacholeta ni kidogo, ye ye anachukua kikubwa. Kwa hiyo, mifumo ya ukusanyaji wa kodi hairuhusu kutuongezea mapato. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mtu hapa alipokuwa anachangia, alisema hajaona Wizara inayokuja hapa ikasema sisi tuna hiki, mkitupa hela hii, tutaongeza hiki. Katika Kamati yetu tulikutana na Wizara mbalimbali zilizokuja zinasema sisi mkitupa bilioni 300, tutazalisha trillioni moja au tutazalisha bilioni 900. Lakini tumeshauri, sijaona kama vinatokea hapa, kuna watuwamekuja wanasema sisi mkitufanyia kama utalii, ardhi na wengine wali-suggest kitu cha kupewa.

Mheshimiwa Spika, nadhani kinachotakiwa ni kwamba, ule u shauri wa kitabu chako. Ule ushauri uliofanyika mara ya kwanza wakiuangalia vizuri, una uwezo wa kutuongezea mapato na watu wakaondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni la kuondoa ushuru katika bodaboda. Nitaje mtu aliyenipigia na napenda wapiga kura wangu wasiseme nimewakandamiza, lakini nimepigiwa simu na kijana anaitwa Jimmy kutoka katika Kata ya Buyango. Ananiambia mama tunachoomba ututetee, walivyoongeza petroli hawajatusaidia, maana hizi pikipiki siyo zetu. Tunachoomba ni bora tu hizo tozo ziwepo, lakini mkiongeza petroli eti mkaundolea ushuru mmemsaidia nani? Umeongeza petroli, umetoa ushuru, lakini kwa yule mtu wa chini hujamsaidia.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie sikatai ile hamsini na sikatai ile 63, lakini tuangalie je, tuna uwezo wa kuongeza kutoka kwagine? Kama watasoma vizuri ile ripoti, tumeshauri uvuvi wa bahari kuu, haujatajwa hata kidogo mahali hapa. Kuna hela nyingi sana pale. Hiki kitendo cha kuongezeka petrol, mchele utapanda, unga utapanda na kila kitu kitapanda na tunadhani tumewasaidia watu wadogo kumbe hatujawasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana, kama tunaweza kwa kweli tuliangalie suala hili na twende kabisa tuangalie mapato mengine, siyo lazima tuongeze katika *petrol* na kumbe hatujawasaidia. Akawa ametoa *suggestion* kwa nini pikipiki yenye matairi matatu isitozwe shilingi kumi na tano, pikipiki za kawaida ziko nyingi mno, zikatozwa 10,000. Tutakuwa kweli hatujakusanya kitu kidogo hata kufidia katika kuongeza hiyo *cost* ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Felix Mkosamali atafuatiwa na Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura. Pia Mheshimiwa Henry Shekifu ajiandae na tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo nitapenda nijibiwe wakati Mawaziri wanahitimisha, ningependa kujibiwa juu ya chombo ambacho tumeanzisha, *The Presidential Delivery Bureau* ambacho kitakuwa kinafutilia miradi mikubwa ili tuweze kupata maendeleo makubwa na kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kupewa majibu Sheria ya chombo hiki italetwa lini? Kwa sababu tumekitengea chombo bilioni 29 na chombo hiki kinakwenda kuwa na kazi kubwa, kazi ya kufutilia Mawaziri kufanya kazi. Tumesema kwamba Mawaziri sasa wataanza kuingia mikataba, tuone wanafanya kazi namna gani?

Mheshimiwa Spika, sasa chombo hiki kisipotungiwa Sheria mapema, kikabaki kama ni chombo tu cha kushauri, hakina meno, hakiwezi kumwambia Waziri kwamba, tulikubaliana hivi, Mkataba wako unakoma hapa na unatakiwa uende hivi. Hizi fedha zitakuwa hazina maana.

Mheshimiwa Spika, ningeshauri chombo hiki kwa sababu kimeanza mwaka huu, kama kutakuwa na nafasi wangeleta Sheria tuijishe, tuangalie Mawaziri watakuwa wanafanya kazi namna gani, kwa sababu chombo hiki kitakuwa ni *link* baina ya Wizara moja na nyine, kitakuwa kinataka Wizara moja ifanye kitu hiki na Wizara hii kufanya hiki. Sasa isije ikatokea Wizara nyine watu wanachapa kazi, halafu wengine wakawa hawachapi kazi, tukashindwa kujua kwamba tunaanzia wapi na tunaishia wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyonataka majibu, Sheria inaletwa lini? Chombo hiki tumekipitishia fedha bilioni 29, sasa tunataka Sheria yake iletwe ili tuone kwamba kitakuwa na *efficiency* kiasi gani. Najua wanasema kwamba kiko chini ya Ofisi ya Rais, lakini siyo *Bureau* ya kwanza kuwa chini ya Ofisi ya Rais. *PCCB* ni *Bureau* na iko chini ya Ofisi ya Rais, lakini tumekuwa tunaona bado wana matatizo, wanasema kwamba, wanashindwa kufanya baadhi ya majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa kujua Sheria ya *Presidential Delivery Bureau* italetwa lini ili tuweze kuona kweli haya matokeo makubwa na ya haraka yanawezekana au hayawezekani. Kama Sheria hii isipoletwa mpaka mwaka kesho kwenye bajeti tusipitishie fedha kwenye chombo hiki kwa sababu itakuwa ni *toothless organ* ambayo haiwezi kuwajibisha watu.

Mheshimiwa Spika, jambola pili, watu tumezungumza sana, lakini tunataka tujue, tunataka utozaji wa kodi katika maeneo ya madini, maeneo ya utalii na kadhalika. Waziri atujibu, Viongozi wa Dini walitoa taarifa yao kwamba, wamebaini upotevu wa trilioni 1.7 mwaka 2010, ambayo ilikuwa ni 17% ya bajeti, walitoa hiyo. Sasa Mheshimiwa Waziri atujibu, ule utafiti uliofanywa ni ukweli na kama ni kweli, Serikali, imeufanyia kazi namna gani?

Mheshimiwa Spika, lakini pia tujibiwe, tumekuwa tunaeleza kwamba, kwenye sekta ya madini hatukusanyi kodi vizuri; kwa

mfano, misamaha ambayo inatolewa kwenye mafuta kwa makampuni ya madini yanayofanya utafiti na uchimbaji wa madini, yanapewa *exemption* ya kodi kwenye mafuta na baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Spika, sasa wakati Mheshimiwa Waziri anajibu, naomba anipe majibu sahihi kwamba, kwa nini, wananchi mnawaongezea pesa kwenye petroli, kwenye dizeli shilingi mbili, lakini makampuni ya madini na kadhalika wao hamuwatozi fedha ya mafuta?

Mheshimiwa Spika, naomba nijibiwe majibu sahihi. Mnatumia vigezo vipi kufanya *exemption* kwenye makampuni makubwa haya yasilipe kodi, *exemption* kwenye mafuta yanayotumika kwenye mitambo na magari, lakini watu wa kawaida watoe kodi? Naomba nijibiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nataka kujibiwa, Mheshimiwa Waziri amesema kwenye Hotuba yake kwamba, kwenye vitalu vya utalii, sasa wataanza kwenda kuvitangaza kwenye mnada, lakini bado nahoji maana nataka kujua, tumekuwa tunawaauliza watu ambao wanaomba vitalu; wamekuja kule kwetu, wanatwambia kitalu watakuwa wanatulipa shilingi milioni 447.

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka tuhame huko au nchi yetu ihame kutoka kwenye maeneo haya ya watu kuja, mtu anakwambia nataka kitalu, tunampatia kitalu bila kujua yeye anapata kiasi gani kwenye kitalu kile, tunataka Serikali, ifanye utafiti ijue kwamba, tukimpatia mtu kitalu cha utalii mahali, atapata kiasi fulani cha fedha na sisi tutapata kiasi fulani.

Mheshimiwa Spika, tumehoji, kwa mfano, vitalu vya Kasulu. Tunaambiwa atatulipa shilingi milioni 447; sasa tunamuuliza wewe unapata ngapi? Hiyo *issue ni question*, hatupewi majibu. Sasa tunataka tuhame huko na tumekuwa tunayaeleza haya mara nyingi sana. Pia mara nyingi nimekuwa naeleza, nchi yoyote lazima iwe na *focus*, je, ni kweli hatuna Wataalam wa kujua vitu hivi?

Mheshimiwa Spika, kwenye madini sasa hivi tunaendelea hivyo hivyo, watu wanakuja wanachimba na nimekuwa nazungumza sana kuhusu hili jambo la *prospecting license*, najua Wizara ya Nishati na Madini imetoa Leseni zaidi ya 3,000 za utafiti wa madini. Lakini ninachotaka kufahamishwa Serikali, ina mpango gani, hata kama hatuna Wataalam sasa, lini tutaanza kufanya utafiti wenyewe, tujue tuna madini kiasi gani ili tuweze kutoza kodi yenye uhakika kuliko kuendelea na utaratibu huu?

Mheshimiwa Spika, tumesema muwawezeshe *STAMICO*, Chuo cha Madini na kadhalika, sasa lini mmejipanga tuache haya mambo ya kuwapa watu kufanya utafiti, ye ye ndio anakwambia kwamba, tuna madini kiasi hiki? Lakini pia tujibiwe, magari yanapita hapa kila siku.

Mheshimiwa Spika, moja ya vitu ambavyo nilishangaa sana, ni mgogoro huu wa gesi. Yaani kuna madini yanapita hapa, ma-*container* yanafurishwa, yanapita hapa nje ya Bunge kila siku, yanakwenda Ulaya, lakini Watanzania wameona ni kitu cha kawaida kuliko gesi inayotoka Mtwara kuja Dar-es-Salaam. Sasa haya mambo lazima tuanze kuhoji, lazima tuwe na uhakika wa mambo ambayo tunayafanya. Pia tufahamu ni lini au ni baada ya miaka 10 tutaanza kufanya utafiti wenyewe? Ili mtu anapokuja tunamwambia hatuhitaji ufanye utafiti, tunajua tuna madini kiasi fulani, tunaingia mkataba wa namna hii. Je, tunakwenda huko lini? Baada ya miaka mingapi sasa tutaanza kufika huko?

Mheshimiwa Spika, pia tulihoji ku-*control* hii mitandao ya simu. Nimeuliza maswali hapa 2011 na 2012, kuhusu ukusanyaji wa kodi kwenye mitandao ya simu, tukaambiwa Serikali, italeta chombo kama wanavyofanya Ghana na sehemu nyingine ambacho kitafuatilia *transactions* zote za kwenye mitandao ya simu. Nikatoa mfano Vodacom peke yake trilioni 6.6 zimepitishwa kupitia *M-Pesa*, sisi tumepata kitu gani?

Mheshimiwa Spika, sasa lini mtakuwa na chombo ambacho kinafuatilia kujua *transactions* zote zinazofanyika? Kuliko hii ambayo sasa hivi tunabaki tunawatoza watu kodi kwa namna wanavyojisikia na kwa jinsi ambavyo wanafanya *transactions* jinsi wanavyotaka.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua Serikali imejipanga vipi na chombo hicho cha kuratibu mitandao hii ya simu kinakuja lini na kinaanza kufanya kazi lini ili tuweze kuwa na uhakika wa mapato yao na sisi tuweze kuwatoza kodi na kupata mapato ambayo ni stahiki kwa Taifa letu?

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri tena, kama ambavyo nilishauri kwenye maeneo mengine, kuhusu fedha za mabilioni ya Kikwete, maarufu kama Mabilioni ya JK na fedha za *TASAF*. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria, ambayo tunasimamia Mifuko hii ambayo iko chini ya Ofisi ya Rais. Nilieleza kwamba, Wizara ya Kazi, ule utaratibu wanaoufanya wa kuwapatia watu fedha ambazo watu wameandika miradi, ile miradi inakaguliwa na Wataalam wa Wizara, kisha wanapewa zile fedha, baadaye zile fedha zinarudishwa, nikashauri kwamba, utaratibu huu utumike pia kwenye Mifuko hii mingine.

Mheshimiwa Spika, sisi tumekwenda kukagua, kwa mfano, mradi wa *TASAF* ambao wamefanya mfano wa vijiji viwili; Kijiji cha Mataya kilichoko Wilaya ya Bagamoyo na Vijiji vya Mwalusembe huko Wilaya za Pwani. Mtu anapewa fedha zile, anakwenda kununua viatu. Nilimuuliza mmoja, umepewa fedha, ulifanya nini? Anasema nilikwenda kununua viatu.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachoshauri, hizi bilioni zaidi ya 400 ambazo tunakwenda kuwapatia *TASAF*, tuziwekee utaratibu ambao fedha zile zitakuwa zinarudi kama ambavyo wameanza Wizara ya Kazi. Fedha zile wanakopesha watu, baada ya hapo fedha zile zinarudishwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, atafuatiwa na Mheshimiwa Henry Shekifu na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu atakuwa wa mwisho!

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa siingii kwenye Baraza la Mawaziri, naomba swalii hili nimtume ndugu yangu Mheshimiwa Lukuvi, akatuulizie kule. Ni swalii ambalo nimetumwa na wananchi wa Tunduru, wanaauliza, sisi wana Tunduru tumewakosea nini Watawala? Kwa hiyo, Mheshimiwa Lukuvi, naomba achukue swalii hilo na Bunge ijalo anijibu.

Mheshimiwa Spika, Wanatunduru wanaauliza swalii hilo na msingi wa swalii hilo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tunduru ambayo iko ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyo Wilaya nyingine ilipata uhuru mwaka 1961, lakini ilifaidi kidogo sana uhuru huu kwa sababu, Wilaya hii ilikuwa ni moja ya Makambi ya Wapigania Uhuru wa Msumbiji. Kwa hiyo, kila siku ilikuwa ni mitikisiko, mabomu yanapigwa Tunduru, tumekaa sana kwenye Mahandaki, kwa hiyo, hatukuweza kujikita zaidi katika kilimo kikubwa cha uzalishaji, ili tuwe matajiri kama maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, tulikubali kuwa wahanga wa mapambano yale kwa kuwa, tuliamini kwamba, Msumbiji ikipata uhuru, basi nchi yote ya Tanzania nayo, itakuwa na uhuru wake wa uhakika kama alivyokuwa akisema Mwalimu Nyerere.

Mhesimiwa Spika, baada ya Msumbiji kupata uhuru tulitegemea kwamba na sisi sasa tutapumua, lakini haikuwa hivyo kwa Tunduru. Tukawa tuna mashambulizi makubwa sana, kila siku tunaliwa na simba, ikawa vile vile uzalishaji mashambani ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Marehemu Simba wa Vita, Mzee Kawawa, alikuja kutusaidia tukawaangamiza wale samba. Tukasema sasa tutulie tuanze kuzalisha, ndoto za Wanatunduru hazikuwa hivyo tena, bado

Wizara inayoitwa Maliasili ikawa inatanua maeneo yake ya kufuga wanyama. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mara tunasikia leo *Ushoroba wanamega* maeneo ambayo yanatusaidia sisi kuzalisha wanasema waendelee kufuga tembo. Tembo wale bahati nzuri kama ingekuwa wanakaa kwenye maeneo hayo ambayo sisi tumewatengea, tusingekuwa na ugomvi nao. Lakini wanatoka kwenye maeneo hayo tuliyowatengea Mwambesi, wanakwenda kusmbambulia mazao ya wananchi, kiasi kwamba, wananchi wale ambao wamejikita sasa katika kuzalisha, ili waondoe umaskini, wanashindwa kwa sababu, ya vurugu za tembo.

Mheshimiwa Spika, tumepeleka taarifa Serikalini, hakuna anayeshtuka. Watu wanauawa, tukipeleka taarifa hakuna anayeshtuka, kiasi kwamba, wanauliza tumewakosea nini? Kila tulichowakosea watwambie ili na sisi tuweze kujirekebisha, ili tuweze kusaidiwa kama wanavyosadiwa wengine. Nitatoa mifano ya dhahiri hapa kutokana na bajeti hii na bajeti zilizotangulia.

Mheshimiwa Spika, juzi juzi hapa imefanyika *operation*, naiita *operation* ya kihuni kwa sababu, yaliyofanyika yale sidhani kama yangefanyika kwenye Wilaya zingine, mtikisiko ungetokea wa namna gani? Nikamwomba Waziri wa Maliasili, aje Tunduru, aje awasikiewatuwaliodhalilishwa na kudhulumiwa. Akasema nitakwenda, hadileo tunavyozungumza hajakwenda. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa tatizo ambalo sio zito kama lilitotokea Tunduru, limetokea kule Loliondo, Waziri wa Maliasili amekwenda mara nne, ametoa ushuhuda katika Bunge hili wakati anahutubia kwenye Bajeti yake. Amekwenda Loliondo mara nne, lakini Tunduru ambako watu wanakuwa, wanadhulumiwa, hajakwenda hata mara moja; tumewakosea nini mtwambie? Au tatizo ni kuwa katika maeneo, maana Tunduru ndio Kusini ya Kusini, sasa kosa letu kuamua kuishi Kusini ya Kusini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, haya, barabara; sijawahi kusikia hata siku moja katika nchi hii Mkandarasi wa barabara akawa Mhindi, lakini Tunduru tumeletewa Wahindi. Matokeo yake ndio hayo barabara hakuna kilichoonekana. Tunduru hiyo, wale wenye sifa ya kula pilipili na kutafuna vitunguu ndio wanapelekwa Tunduru kwenda kujenga barabara. Matokeo yake ndio hayo mpaka leo hii hata kilometra moja hajajengwa barabara, tumewakosea nini Tunduru, mtwambie? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaliwa na simba hamjali, tunauawa na tembo hamjali. Mazao yetu yanaliwa na tembo hamjali, tukaishi wapi? Haya, tumepeata mradi wa barabara, mabilioni ya fedha, mnatuletea Wahindi, wala pilipili na vitunguu? Mheshimiwa Lukuvi, majibu ya swali hili atuletee.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza kwa uchungu sana juu ya *operation* ile iliyofanyika Tunduru, baada ya wiki tatu, naandikwa kwenye gazeti kwamba, bunduki tatu za Mbunge Mtutura, zimekamatwa ziko Polisi.

Mheshimiwa Spika, kabla ya hapo nilikuletea kopi ya barua ya namna ya watendaji hawa wanavyoniandama na kunizushia mambo mbalimbali. Barua ile mpaka leo sijapata majibu, toka mwezi wa Nane mwaka jana; wanasema bunduki za Mtutura tatu; hivi kweli, Serikali, yetu inaweza ikaruhusu mtu mmoja anunue *Rifle* tatu, Mbunge! Za nini?

Mheshimiwa Spika, haya, wanasema Katibu wake amekamatwa anaua tembo *Selou*, wakati juzijuzi tumeona mtu mmoja amefungwa miaka 10 jela kwa kuwa amekutwa anakula ugali na kitoweo cha paa. Leo bunduki ya Mtutura, inaua tembo, halafu yule mtu aliyeshikwa nazo anafungwa kifungo cha nje miaka miwili, hivi inaingia akilini? Halafu na Mbunge mwenyewe, bado anaendelea kuishi Dodoma, inaingia akilini?

Mheshimiwa Spika, lakini hiyo yote dhamira yake ni kunidhoofisha, ili nisitetee haki na dhuluma wanazofanyiwa wananchi wa Tunduru, nasema sitasita katika hilo. Nitaendelea kuongea, leo mniambie jangili, kesho mtaniambia gaidi, lakini bado nitaendelea kuwatetea wananchi wa Tunduru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, najua mengi zaidi yatanikuta, lakini sitasita kwa sababu, wale watu wonyonge kwa kipindi kirefu wamejitolea kutumikia nchi hii, kutumika katika mapambano ya ukombozi wa Afrika; leo badala ya kuwasaidia wanadhalilishwa, haiwezekani na hatuwezi kukubali. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nitoe tu ufanuzikwamba, Watanzania waelewe Mtutura, ambaye sasa hivi anazungumza, hilo jino la tembo kuliona kwa macho kama sio kwenye picha ya magazeti au kwenye *TV*, sijawahi kuliona. Sasa leo, nawahakikisha kwamba, sijawahi kujihusisha kwa namna yoyote na ujangili na sifiki kufanya hivyo na ndio maana mpaka leo hawajanifikisha Mahakamani, Murji yule, mbona ye ye yuko ndani? (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi mtoto wa mkulima wa korosho mbona hamjanifungulia mashtaka kama mimi jangili? Murji, mbona leo yuko ndani? Mhindi tena tajiri? Mimi maskini mbona hamjanifungulia mashtaka? Dhamira yenu ni kunidhoofisha na nawaambieni katika hilo hamjalamba dume, mmelamba galasa, nitaendelea kuwatetea wananchi wa Tunduru kwa kadiri Mwenyezi Mungu atakavyoniongoza. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, bado nasisitiza Waziri Mheshimiwa Kagasheki, aje Tunduru ajithibitishie ule uwongo ambao amedanganywa na wale Watendaji wake kwamba, Tunduru kuna majangili. Hivi madawa mangapi ya kulevy ya yanapita Tanzania, hivi Tanzania tuna kiwanda cha madawa ya kulevy?

Mheshimiwa Spika, yale meno ya tembo yanatoka Msumbiji, Tunduru ni kama *transit*, sasa mnatwambia kwamba, sisi wote ni majangili. Silaha 300 zimekamatwa wanasema za majangili, majangili gani? Bastola mbili za wafanyabiashara zimekamatwa, bastola zinaweza zikau tembo? Bastola inaweza ikaua tembo? Zimekamatwa na bastola ziko Wizara ya Mambo ya Ndani, wale Maliasili zinawahusu nini? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba bunduki zetu mturudishie kwa sababu, tunakufa na simba, tunakufa na tembo, hatuna namna nyingine ya kujitetea na kinyume cha hivyo tutapeleka

kwenye Tume ya Haki za Binadamu. Hamwezi mkatuacha tunakufa tu, wakati kumiliki bunduki ni haki ya mtu. Kama wale waliomiliki bunduki wameonekana kwamba, wana hatia wafikishwe Mahakamani, lakini sio kuwafunga kifungo cha nje na kuwachukulia bunduki zao; wapelekeni Mahakamani kama kweli wana hatia.

Mheshimiwa Spika, siku moja niliuliza hapa swalii kwamba, kwa nini tusijaribu kutumia mfumo mwingine wa utawala katika ule muungano wetu? Waziri, akaniambia kwamba, Serikali yetu haifanyi kazi ya kubahatisha; sasa katika hili, Serikali, mbona mnabahatisha? Kwa nini tubahatishe? Namwomba Waziri Kagasheki, aje Tunduru na aje awape pole watu ambao ndugu zao wameuawa na Askari wa Maliasili. Nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ingawa katika bajeti hii fedha za Maliasili ambazo sikuziunga mkono zipo. Naunga mkono kwa sababu ya Kanuni zenyewe zilivyo. Huyu Mheshimiwa Lukuvi, asije akanipiga ile bakora ya *Chief Whip* ya fimbo tatu, lakini kinyume cha hivyo, nisingeunga mkono bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. haya, mara Lukuvi mara Kagasheki, sasa sjui yupi?

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, namheshimu sana Mheshimiwa Mtutura. Anasema kwamba, Serikali, inatoa barabara kwa Wahindi. Naomba nimpe Taarifa kwamba, Serikali, haitoi barabara kwa Wahindi, inatoa kwa Wakandarasi. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Aah, bwana acheni ubishi, ndio hao hao tu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Henry Shekifu, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kukaribia kufunga dimba leo. Kwanza nichukue nafasi hii kuwapongeza sana na kuwapa pole sana wananchi wa Arusha, kwa mkasa uliotokea. Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Tanga na hususan, wananchi wa Wilaya ya Muheza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni shahidi katika mambo haya ambayo yanatokea sasa, kamahayatadhibitiwa kwelitutakuwa mahali pabaya sana. Sisi tulikuwa na uchaguzi pale Muheza, kwa bahati nzuri tumeweza kushinda bila fujo lakini iko bahati mbaya sana inayojengeka ya tabia za uharakati katika kutafuta uongozi. Tabia hii inaweza kujengeka katika nchi yetu, inafika mahali wananchi wanagonganishwa, vijana wanaandaa makundi ya fujo na fujo zinafanyika bila kujali hatma ya amani nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge niwaombe wananchi, walikemee hili na kwa kweli wasidanganyike maana kama *Traffic Police* wanavyosema utii wa sheria bila shuruti na ifike mahali wananchi kama wanaopanda basi waseme kwamba, wewe dereva unaendesha gari vibaya, simama na ikiwezekana wamnyang'anye funguo. Niseme sasa imefika mahali Serikali ichukue hatua kali, hawa madereva wanaotaka kutufikisha pabaya, wanyang'anywe funguo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwashukuru wananchi wa Muheza sasa nije katika uchangiaji. Nitajielekeza katika mambo machache kwa sababu tumechangia kwa mwezi mzima na zaidi. Pengine nitoe tu ushauri katika mambo ambayo yamezungumzwa kwa kirefu na nitoe mapendekezo kiasi. Kwanza nizungumzie kuhusu vipaumbele sita, naomba sana Waheshimiwa Wabunge vipaumbele vile sita tumeanza navyo na nina uhakika tukibadilika tutachanganyikiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma tulikotoka tulifika mahali tukazona Halmashauri hazifai, tukazifuta, baada ya muda

tukazirejesha. Tulifuta Vyama vya Ushirika, tukarudia mahali tukasema virudi, lakini ni kukosa *consistency*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi naomba vipaumbele sita viendelee lakini basi tutafute sababu, hivi ni kwa nini tunayumba. Kwanza niseme, katika vipaumbele sita, vyote ni vizuri na ni muhimu kwa Taifa letu, lakini tatizo letu kubwa ni uwezo wetu na tabia yetu ya kutosimamia mambo vizuri.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa, tunaamua mambo, lakini usimamizi haffifu. Utendaji katika ngazi mbalimbali kuanzia juu mpaka chini, kwa kweli ni mbovu, sasa tuchukue hatua. Pili, uwazi na uadilifu mambo yanafanyika sawa lakini uwazi haujafikia viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji wa viongozi, uwajibikaji wa watendaji wote katika ngazi zote haupo. Pili, ubunifu wa ziada katika kubuni vyanzo vingine vya mapato, kuondoa kipaumbele hakutusaidii, kikubwa ni kutafuta njia nyingine za kupata mapato ili tuweze kutekeleza vipaumbele.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilitoa mapendekezo mengi, badala ya kuondoa vipaumbele, hebu nendeni ikifika baada ya miezi sita, tuangalie njia tulizojiwekea kupata mapato zipo, zinafa, kama hazifai twendeni upande mwingine. Ni jambo la kawaida kufanya *midyear review* ya bajeti kitu cha kawaida. Kwa hiyo, nafikiri tujiwekee, ikifika mwezi wa 12, hatuendi vizuri, Kamati yetu ya Bajeti ituambie vyanzo vingine vya bajeti ni hivi na tuviweke ili nchi iendelee.

Mheshimiwa Spika, nimeshazungumzia matatizo ya utendaji, sasa nije kuchangia kidogo katika hiyo bajeti yenyewe na wengine wamechangia na sitaki kurudia sana. Suala la kilimo, Waziri wa Fedha hajatueleza kwa undani jinsi mazao haya mchanganyiko hasa ya vyakula yanavyoweza kutumika katika kushusha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, sioni fedha za kutosha zilizotengwa kwa ajili ya ununuzi wa mazaokama mahindi, maharage, mpunga na mazao mbalimbali, yale ya chakula ambayo tukubali tusikubali

hivi sasa mfumuko wa bei umeshuka kwa sababu mazao haya yako sokoni na yameshuka bei. Yakishaondoka sokoni utakuta bei itapanda sana na mfumuko wa bei unakua juu sana na wananchi wanahangaika sana.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini tusiamue kwa makusudi, tununue mazao yote ya ziada yaliyoko katika soko, tuyaweke katika maghala, wakati ukifika kwamba, chakula hakipo kwa wananchi, kinatolewa kiende kusaidia. Lakini sasa tunasubiri, hivi sasa ninavyozungumza maeneo mengine wameshaanza kuuza mazao, Bodi ya Mazao haipo na *SGR*haijulikani iko wapi. Matokeo yake tutafika kwenye soko, ushindani umekuwa mkubwa, hatuwezi kununua, tunarudi nyuma na huu ni ugonjwa wa kila mwaka. Sasa nashauri, tujaribu kuona uwezekano wa kwenda haraka katika ununuzi wa mazao.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuwa Uingereza juzi juzi alizungumzia suala la uwezekano wa Tanzania kupeleka nje mazao ya mboga mboga na matunda. Mazao ya mboga mboga na matunda kwa Kenya yanachangia mapato ya nchi ile kwa asilimia karibu sita; maua, matunda yenyewe, mbogamboga na mazao haya yanachohitaji ni kuwekeza tu, soko lipo.

Mheshimiwa Spika, hivi Serikali kwa nini haitengi fedha za kutosha kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kuwapa pembejeo, viatilifu, mbolea na dawa za kupulizia ili tupate matunda na mbogamboga zenye viwango tuweze kuingia katika soko, tushindane na wenzetu wa Kenya, kila siku tunawapigia makofi, lakini hakuna uchawi katika hili kama hukuwekeza huwezi ukapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili, kwa leo ambalo nalionna ni upungufu mkubwa kwenye bajeti ya Waziri wa Fedha, ni suala la fedha za kigeni. Hakuna nchi itakayoweza kupata maendeleo kama haijaweka taratibu na sera za kuingiza fedha za kigeni

na kuzisimamia. Sijaona mkakati, *bureau de changes* za hapa nchini unaweza ukaondoa fedha wakati wowote na kiasi chochote. Leo ukifika *South Africa* ukidanganya tu una *rand* 2,000 kumbe siyo 2,000, kwa nini sisi udhibiti wetu ni dhaifu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, haya mengi niliyoshauri ni mambo ambayo yatatusaidia kama tutayadhibiti na tutaweka katika utendaji, yatuletee fedha za kutosha, tuwe wabunifu, tutafute mbinu za kuongeza vyanzo vya mapato na tuepuke kupunguza vipaumbele maana vyote ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Dalaly Kafumu, ndiye mchangiaji wetu wa mwisho jioni hii.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho. Namshukuru Mungu tena kwa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu na naomba nianze kwa kumpongeza kijana wangu, aliye karibu yangu hapa, kwamba amerudi tena, naona sisi ni Wabunge wa Mahakama, karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Wabunge wengine walivyosema, naomba nimpongeze Waziri kwa bajeti nzuri na kwa kweli utaratibu huu ni mpango mpya, mpango ambao mapendekezo ya Wabunge yanaingizwa kwenye bajeti kwa kuitia Kamati ya Bajeti, nadhani tumeanza vizuri na kwa bajeti hii nimeona Waziri wa Fedha ameongeza fedha kwenye maeneo mengi ambayo tuliomba yaongezwe, kwa mfano, kwenye umeme vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nina uhakika sasa ahadi niliyopewa kupeleka umeme Igunga kule Itunduru, Mwabudele, Mwagala, Gurubi, Itumba na Mbutu nitapata. Pia nashukuru kwamba, Wizara ya Maji nayo imepewa nyongeza ya fedha na sisi wana Igunga kilio chetu kikubwa ni maji. Wilaya yetu ni Wilaya ya mbugani hakuna maji ya chini. Tunaomba bwawa, nilisema kipindi kilichopita nilipokuwa Mbunge, naomba tena

tupate bwawa ili wananchi wetu waweze kupata maji katika Wilaya ya Igunga.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo, sasa naomba nichangie kidogo kuhusu bajeti. Jambo la kwanza ambalo ningependa kusema ni kwamba, kwenye bajeti hii nimeona mambo ya ukusanyaji mapato, nimeona matumizi lakini kwa namna ya pekee sijaona mipango madhubuti ya kukuza uchumi. Inawezekana Mheshimiwa Wassira amesema, lakini nilitegemea kwenye bajeti hii kubwa kuwe na mipango madhubuti ya kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nilipokuwa Mbunge na sasa ni Mbunge, nilisema hivi, ili tuweze kuhakikisha kwamba, fedha yetu inakuwa na nguvu ni sharti tuanze sasa kutunza fedha pamoja na dhahabu kwenye Benki Kuu yetu. Dhahabu ni fedha na bei ya dhahabu inapanda kila siku, tutakapokuwa na dhahabu katika hazina yetu, tunaweza ku-*stabilise currency* yetu vizuri zaidi kama nchi zingine zinazofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii sijasikia, japokuwa tuliomba sana na Wabunge wengi walishasema, naomba basi Waziri aliangalie hili. Aangalie huu mpango, Sheria inaruhusu. Sheria ya *BOT* inasema tunatunza dola na tunatunza dhahabu kwa nini hatutunzi na wakati tuna dhahabu nyingi sana? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nilikuwa nalifkiria na Wabunge wengine wamesema ni juu ya kukuza uchumi kwa kuhakikisha tunakuwa na mabilionea wengi katika nchi yetu. Tukipata mabilionea wengi au mamilionea wengi, tutakuza shughuli hizi za uchumi katika nchi yetu na tunaweza kuwa na ajira nyingi na tutaweza kuzalisha bidhaa nyingi, tuka-*export* na uchumi wetu ukakua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nchi ya Vietnam kwa mfano, walivyomaliza vita na Marekani nchi hii iliamua kwa makusudi kutengeneza mabilionea watano kila mwaka na Serikali ilikuwa inatoa fedha kwa watu binafsi hawa kuwasaidia waendeleze viwanda vyao, wajasiriamali wote wazuri, wafanyabiashara

wazuri walisaidiwa na Serikali. Kwa nini sisi tusifanye tuwe na mabilionea wengi tuweze kupata ajira, wataalam tupo tupate ajira, nchi yetu iweze kuendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kusema, ni ukusanyaji wa mapato. Kweli Serikali imejitahidi kukusanya mapato, Mheshimiwa Waziri anatuambia wamekusanya zaidi ya 93% ya walichotegemea kukusanya, ni jambo zuri sana. Lakini kuna matumizi mabaya katika kukusanya mapato haya, naomba nitoe mfano, Serikali imekuwa ikiunda Wakala na Mamlaka mbalimbali kuisaidia Serikali kukusanya mapato na kusimamia shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, lakini wakati mwingine tumeunda Wakala ambazo zinachukua fedha zaidi kuliko zinavyokusanya na nydingine sasa zinachukua hizo fedha zinatumia, kwa hiyo haziendi tena kwenye Mfuko wa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tunakusanya, tunakula. Tunatakiwa tupunguze Wakala za namna hii, Wakala hizi nydingi tuzipunguze, kazi ifanywe na *institution* ndogo ili tuweze kupata mapato vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ukaguzi wa Madini, ni Wakala ambao umetengenezwa, lakini unafanya kazi zinazofanana sana na kazi za *TRA*, unafanya kazi zinazofanana sana na za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu (*CAG*), unafanya kazi zinazofanana sana na *NEMC* na unafanya kazi zinazofanana sana na Idara ya Madini. Matokeo yake sasa tunachokusanya tunapeleka kwenye Wakala itumie, lakini tunachopata ni kidogo pamoja na sifa zote zinazotolewa kwa ajili ya Wakala huu kuna matatizo katika kufanya kazi zile zile kwenye migodi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ikutane tu na wadau hawa niliowataja, ijaribu kutengeneza utaratibu ambao kazi moja ifanywe na mtu mmoja, usifanye kazi moja na watu wengi unatumia hela vibaya. Nimetoa mchango huu kwa maandishi na nasema hapa kidogo ili Serikali itazame jambo hili. Wakala ule tunauhitaji, lakini haujaka sawa, tuupeleke mahali pazuri ili kazi zile zifanyike kwa tija zaidi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kusema, matatizo ya wananchi wa Igunga kama nilivyosema ni maji na naomba tena Mheshimiwa Waziri katika kutekeleza jambo hili aitazame Igunga vizuri. Pia tatizo kubwa lingine licha ya kujenga mabwawa, naomba ule mradi wa kuchukua maji kutoka *Lake Victoria* utekelezwe kama llani ya Uchaguzi inavyosema. Mradi huu ukitekelezwa wananchi wa Igunga watakuwa na nafasi ya kuweza kupata maji kama wenzao ambao wako karibu na maziwa, wapo karibu na mito sisi tupo mahali pakame kweli kweli.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niunge mkono hoja. Nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niwe mchangiaji wa mwisho. Naomba nisiwachoshe ili tuwahi kwenda huko tunakokwenda. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante. Kwanza, naomba niwashukuru kwamba, tumefanikiwa kupata idadi kubwa tu ya wachangiaji kwa siku ya leo. Pia ningependa mkumbuke, mkinibadilishia tarehe kuna wengine mwishowe watakosa kuchangia. Kwa hiyo, tarehe tunazopanga ni vizuri mkazizingatia kwa sababu wewe utasema siku hiyo na sisi wachangiaji wakiisha tunafunga mjadala, kwa sababu siyo lazima tumalize siku zile, kanuni inasema, siku zisizozidi. Kwa hiyo ikitisema zisizozidi zikipungua siyo vibaya, kwa hiyo vizuri wale wanaotaka kuongea wawepo.

Halafu kwa sababu utaratibu huu ni mgeni, wengine walipojaza fomu pale mwanzoni hawakuja hata wanajaza kwa ajili ya nini. Kwa hiyo, kama wapo ambao wanataka kuzungumza, lakini hawakujaza fomu kwa maana ya bajeti, waende kwa Katibu kule kule wakachukue fomu wajaze, halafu tutaziingiza tena kwenye *computer*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa maelezo ya Hoja ya Kutengua Kanuni za Bunge, chini ya kifungu cha Kanuni ya 153(1) ya Kanuni za Kudumu, Toleo la 2013.

KWA KUWA Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge wa kushughulikia Bajeti ya Serikali pamoja na shughuli nyingine za Bunge zilizopangwa, umepangwa kumalizika tarehe 28 Juni 2013;

NA KWA KUWA ratiba ya shughuli zote zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu wa Kumi na Moja zimepangwa kwa kuzingatia kanuni ya 99(1) ya Kanuni za Kudumu, Toleo la 2013;

NA KWA KUWA moja ya shughuli zilizopangwa kufanyika katika Mkutano huu ni kujadili na kuitisha Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2013 ambapo ni lazima shughuli hii ikamilike kabla ya tarehe 30 mwezi wa Sita;

NA KWA KUWA utaratibu mpya wa mzunguko wa bajeti (*budget circle*) unataka Bajeti ya Serikali isomwe mwishoni mara baada ya Bajeti za Wizara zote kukamilishwa

NA KWA KUWA baada ya usomaji wa Bajeti ya Serikali ambayo pamoja na mambo mengine huelezea vyanzo mbalimbali vya mapato ya Serikali kwa mwaka huu wa fedha, Serikali huchapisha na kutangaza Muswada wa Sheria ya Fedha kwa mwaka husika;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa kanuni ya 80(2) Muswada unatakiwa kumfikia Katibu wa Bunge katika muda usiopungua siku 21 baada ya tangazo la kwanza la Muswada na kabla ya Muswada huo haujaingia Bungeni;

NA KWA KUWA kutokana na mabadiliko ya uwasilishaji wa hotuba za bajeti yaliyoanzwa kutekelezwa katika Mkutano huu wa Kumi na Moja ambapo hotuba ya Bajeti ya Serikali imesomwa mwishoni. Tangazo la kwanza la Muswada wa Sheria ya Fedha haujakidhi masharti ya kanuni ya 80(2) kulingana na ratiba ya shughuli za Bunge.

NA KWA KUWA ili kuliwezesha Bunge kuweza kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa katika Mkutano huu kwa kuhakikisha kuwa Sheria ya Fedha inatungwa kabla ya tarehe

30 mwezi wa Sita, ni lazima Bunge litengue kanuni ya 80(2) ya kanuni za Bunge kwa mujibu wa kanuni ya 153(1);

HIVYO BASI Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huu wa Kumi na Moja Kanuni ya 80(2) itenguliwe kama ifuatavyo:-

Kanuni ya 80(2) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, tangazola kwanza la Muswada wa Sheria litatolewa na kumfikia Katibu katika muda usiopungua siku 21 kabla Muswada huo kusomwa Bungeni kwa mara ya kwanza itenguliwe na badala yake Muswada wa Sheria ya Fedha usomwe Bungeni kesho na kugawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge ili kutoa fursa kwa Kamati ya Bajeti na wadau mbalimbali kuufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja illiamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kilichotokea ni kwamba, kwa miaka mingine Waziri wa Fedha akishasoma na akaonesha mipaka ya kodi mbalimbali inakotaka kukusanya fedha wakati wa hotuba yake, basi siku ya pili anatoa Muswada wa Fedha. Sasa amesoma juzi, kwa hiyo akatoa, ametoa siyo kwamba hajatoa, lakini sisi tunajadili hii kwa siku zisizopungua saba halifu ule Muswada wa fedha pia tunajadili kwa siku nne.

Kwa hiyo, zile siku 21 ambazo zilitakiwa kama Muswada mwingine wowote wa Serikali sisi hatuna kwa maana hii. Kwa sababu asingeweza kutoa hii mipaka yake ya kodi wakati anaanza, kwa sababu kawaida inakuwa ni siri, hata Mawaziri huwa hawajui, mpaka siku hiyo wanaposoma, saa nane wanakaa wanaambiwa kodi itakaa hapa, kodi itakaa hapa, ndivyo inavyokuwa labda mpaka baadaye litakapobadilika hilo pia, lakini hivyo ndivyo ilivyotokea.

Kwa hiyo, kwa maana hii ni kwamba, hatukuwataka walete *certificate of urgency* kwa sababu siyo kosa lao, ni mfumo tulioubadili sisi. Kwa hiyo, ni sisi wenyewe tuuangalie tuweze kwenda nao. Kama lingekuwa tatizo lao, wangeleta chini ya hati ya dharura maana ingebidi wajieleze, lakini kwa sababu sisi ndiyo tuliobadilisha mfumo. Kwa hiyo, ndiyo maana tumewezesha kesho Muswada wa Fedha kusomwa kwa mara ya kwanza.

Ukisomwa mara ya kwanza, maana yake umekwenda *public*, mtu yejote anaweza kusoma na watu wanaweza kuchangia na kupitia Kamati yetu ya Bajeti wanaweza kualika watu mbalimbali wakaja kuchangia. Nina hakika kwa mtindo wa kazi wa Kamati ya Bajeti utawahi siku zinazostahili. Kwa hiyo, hili ndilo lilikuwa maana ya badiliko hilo.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa kuahirisha Bunge, karibu unafika, niwashukuru sana kwa jinsi mlivyojadili kwa makini kabisa bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha na wale ambao hawajapata nafasi kama nilivyosema na hawakuomba, waende kwa Katibu wa Bunge kwa kutumia zile fomu zao, wataingiza majina yao pale kwa sababu tunataka kujua *on an average* ni Wabunge wangapi katika Bunge zima la Bajeti wanaweza kupata nafasi.

Hapa sasa hatujali umechangia mara kumi au mara ngapi, msianze kujisikia aibu, hii hoja tunayojadili, tunatakiwa kuwa na wachangiaji kama 200 na walioomba ni kama 101, kwa hiyo nafasi ipo, kwa wale ambao hawakujaza fomu waende kujaza.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba niahirishe kikao cha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.40 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne,  
Tarehe 18 Juni, 2013, Saa 3.00 Asubuhi)*

17 JUNI 2013

17 JUNI 2013